# Nipashe

Jumatano Oktoba 12, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581096

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



JACKPOT BABA LAO!

TZS. 367,741,460

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Mwalimu** wa madrasa jela miaka 30 kwa kumdhalilisha mtoto

UKURASA 7



CHELSEA WAPAMBANA KUMBAKIZA MOUNT

UKURASA 30

KUELEKEA SIKU YA NYERERE

# Utafiti wabaini maadui watatu bado tatizo

UKURASA 2





UMASKINI



MARADHI



UJINGA

## UN yampa kongole Samia usawa kijinsia

UKURASA 7

## Wasiojulikana walivyovamia wakazi, kuwajeruhi

UKURASA 2


The Guardian Nipashe

KUMBUKIZI YA HAYATI MWALIMU NYERERE



MIAKA 23 1999-2022

Kampuni ya uchapishaji ya The Guardian Ltd kupitia magazeti yake, 'The Guardian' na 'Nipashe' itatoa Toleo Maalum Oktoba 14, 2022 ya kumbukizi ya Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Nyerere (1922-1999).

Kupata nafasi kwa matangazo, wasiliana nasi kwa namba 0782253676, 0745 700 710

Wahi kwa kuweka ujumbe wako leo!


MICHEZO SERIKALI YAIGEUKIA YANGA UK.32




Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Francis Michael (kushoto), akizungumza wakati akifungua kongamano la kitaaluma la kumuenzi Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, lililojadili mapambano dhidi ya adui ujinga, katika Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere Kigamboni, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wasiojulikana wavamia kijiji, wapora na kujeruhi

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

WATU 10 wanadaiwa kujeruhiwa na kundi la watu wasiojulikana baada ya kuvamiwa na kupora mali katika makazi yao kwa kukatwa mapanga usiku wa kuamkia juzi katika Kijiji cha Tambani, wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani.

Katika tukio hilo nyumba nane zilivamiwa kwa kuvunjwa milango na kupora simu na pesa huku wakiwaacha na majeraha ya mapanga wananchi katika sehemu mbalimbali za miili yao.

Ramadhani Kipengele, mkazi wa eneo hilo ni kati ya waathirika wa tukio hilo ambalo alisema watu hao walipofika kwenye nyumba zao kauli ambayo walikuwa wanaitaja ni kutaka fedha na mtu akibisha anapigwa mapanga.

Mwananchi mwingine aliyekumbwa na tukio hilo, Fatuma Hamis, alisema walipofika nyumbani kwake walivunja milango na kuchukua simu mbili pamoja na fedha na kuwashambulia kwa kuwapiga.

Viongozi wa kijiji hicho na baadhi ya wananchi wamelaani vitendo hivyo na kuliomba Jeshi la Polisi kuwasaidia kukamilisha ujenzi wa jengo la polisi waliloanza kujenga kwa nguvu za wananchi ili kusaidia kuongeza ulinzi katika kijiji hicho.

Wamesema endapo ulinzi hautaimarishwa kuna hatari ya uvamizi kufanyika mchana kwa wananchi wanaoshinda nyumbani na kujeruhiwa zaidi.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji, ambaye ni Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Protus Mutayoba, amekiri kupata taarifa za tukio hilo ambaye alifika na kutoa pole kwa majeruhi.

Akiwa katika eneo hilo alisisitiza suala la ulinzi shirikishi kwa wananchi huku akiwaomba kuwa na ushirikino na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa za uhalifu unapotokea kwenye maeneo yao.

# Utafiti wabaini maadui 3 bado tatizo nchini

**Na Romana Mallya**

WAHADHIRI wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), Kampasi ya Kigamboni mkoani Dar es Salaam, wamesema bado maadui watatu waliotangazwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, hawajaondoka nchini kwa asilimia 100.

Wamesema kwa kushirikiana na taasisi nyingine katika kumuenzi Hayati Mwalimu Julius Nyerere, wamefanya utafiti zaidi ya 30 unaolenga kukabiliana na maadui hao ambao ni ujinga, maradhi na umaskini.

Akizungumza kwenye Kongamano la Kitaaluma la siku mbili, lililoanza jana, Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Shadrack Mwakalila, alisema taifa limepambana na maadui hao, lakini bado halijafanikiwa kuwashinda kwa asilimia 100.

Akifungua kongamano hilo, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Francis Michael, alipongeza hatua iliyochukuliwa na chuo hicho na vingine kwa kufanya utafiti ambao alisema husaidia kuleta maendeleo.

Kongamano hilo limebebwa na kaulimbiu, 'Mchango wa Mwalimu Nyerere katika kuimarisha ustawi wa maendeleo ya jamii ya Kitanzania.'

Dk. Michael alisema taasisi za taaluma ni pamoja na kufanya utafiti utakaosaidia kutatua matatizo na kuleta maendeleo kwa taifa.

Alisema upo uhusiano mkubwa anachotaka Rais Samia Suluhu Hassan, kifanyike kwenye sekta ya elimu na ambacho Mwalimu Nyerere alikuwa anakihubiri.

"Hayati Baba wa Taifa alisisitiza elimu ya kujitegemea ambayo ina lengo kubwa makhsusi la mtu yeyote akimaliza elimu katika daraja lolote iwe elimu ya msingi, sekondari au chuo kikuu, aweze kutoka akiwa na uzoefu, ubobevu wa kujiajiri.

"Elimu yetu imekuwa ikitolewa na kuwanyima nafasi na haki Watanzania wengi hasa pale tulipokuwa tunaendelea kutoa elimu yenye lengo la mtu asome, aelimike, akaajiriwe, tunatakiwa tubadilike tutoe elimu iliyojaa ubobevu, huko ndiko tunakotaka kuelekea," alisema.

Dk. Michael alisema Rais Samia amesisitiza kupitia upya mitaala na sera ya elimu, ili taasisi zitoe elimu ambayo itamwezesha asisubiri kuajiriwa, aweze kujiajiri.

"Tunapotoa elimu ya watu kuajiriwa tunatengeneza bomu, kwamba unapotaka watu wote wakaajiriwe wakati nafasi za ajira ni chache na kila mwaka vyuo vinatoa wahitimu, tunatengeneza bomu.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Mwakalila alisema: "Chuo cha Mwalimu Nyerere ni taasisi ya elimu ya juu, ni wajibu wetu kuhakikisha tunaisaidia jamii na taifa kupambana na adui ujinga, tunapotoa mafunzo na kuendesha warsha yote hayo ni sehemu ya kupambana na adui ujinga.

"Kongamano la mwaka huu kwa kutambua kwenye jamii kuna changamoto mbalimbali za kiuchumi, afya, maendeleo, ambazo zinahitaji majibu ya kuzitatua, ili upate majibu sahihi na kwa njia sahihi yakukabiliana nazo ni lazima ufanye utafiti.

"Tumekuwa na janga la UVIKO-19 na sasa ebola na mambo mengine yanayohusu uchumi, katika kongamano hili kutakuwa na uwasilishwaji wa mada mbalimbali zilizofanyiwa utafiti.

"Wana taaluma wamefanya utafiti mbalimbali, tuna utafiti zaidi ya 30, ambao unatokana na watafiti wahadhiri wa Chuo cha Mwalimu Nyerere pamoja na watafiti kutoka taasisi nyingine," alisema.

Prof. Mwakalila alisema wanategemea mwisho wa kongamano hilo watajua namna gani watakuwa na mchango wa kupambana na adui ujinga na nini kifanyike ili kumshinda.

Mhadhiri chuoni hapo, Dk. Edna Mtoi, aliwasilisha kujikinga na maradhi kwa njia tofauti na kuonesha mama anavyoweza kusaidia mtoto kuwa na afya njema.

Alisema Mwalimu Nyerere alikuwa akisisitiza mambo mengi ikiwamo afya ya jamii na maendeleo ya jamii huanzia mtoto anapozaliwa mpaka anapofikia umri wa miaka mitano.

"Utafiti wangu umelenga kuona namna kuanzia mtoto anapozaliwa, mama anavyojilinda katika afya yake na malezi na ukuaji wake mpaka kufikia baada ya miaka mitano," alisema.

Mkuu wa Idara ya Uongozi chuoni hapo, Dk. Philip Daninga, pia ni katibu wa kamati ya maandalizi ya kongamano hilo, katika wasilisho lake lililoangalia sekta ya viwanda, alisema Mwalimu Nyerere alianzisha viwanda vingi na baadaye havikufanya vizuri mpaka sasa msisitizo upo katika eneo hilo.

Dk. Daninga alisema ili kutorudia makosa ya awali katika sekta hiyo, lazima uwekezaji ufanyike katika maeneo matatu ambayo ni teknolojia, kuwezesha katika elimu na wananchi.



Baadhi ya wahitimu wa Shahada ya Kwanza ya Biashara wakiwa katika mahafali ya 52 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, yaliyofanyika chuoni hapo jana. Kutoka (kushoto) ni Mariam Nguzo, Salome Mchembe, Aisha Mpochi na Nala Richard. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## NMB yanyakua tuzo tisa Afrika Mashariki

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imenyakua tuzo tisa wakati wa tuzo za Accenture 10th Gender Mainstreaming Awards zilizofanyika jijini Nairobi, Kenya kutokana mchango wake wa uwezeshaji wa wanawake ndani ya Ukanda wa Afrika Mashariki.

Tuzo hizo huzawadiwa mashirika na watu binafsi ambao wako mstari wa mbele katika kuendeleza biashara tofauti tofauti kwa kuzingatia ajenda ya usawa wa kijinsia barani Afrika.

Ziliitambua Benki ya NMB na Ofisa Mtendaji Mkuu wake, Ruth Zaipuna kwa kuanzisha mabadiliko yanayochochea maendeleo na ushirikishwaji ndani ya kanda.

Wakati wa hafla ya utoaji tuzo, Benki ya NMB ilitangazwa kuwa Bingwa wa Utawala wa Jinsia Afrika Mashariki, Mshindi wa Afrika Mashariki; Uwezeshaji wa Wanawake katika Jumuiya na Mshindi wa kipengele cha Uwezeshaji wa Wanawake katika Jumuiya.

Benki hiyo pia iliibuka mshindi wa pili, Uwezeshaji Kiuchumi, mshindi wa tatu, Uwezeshaji Wanawake Mahali pa Kazi na mshindi wa tatu, Uwakilishi Sawa na Ushiriki.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna aliibuka mshindi katika vipengele vya Kiongozi Jumuishi nchini Tanzania; Mfano wa Kuigwa Tanzania na Mshindi katika Sekta ya Huduma za Kifedha.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa tuzo hizo, Mkuu wa Miamala ya Kibenki wa NMB, Linda Teggisa alisema tuzo hizo ni matokeo ya jitihada za pamoja za benki hiyo kuweka kipaumbele katika usawa wa kijisia kupitia mfumo wa 'NMB Balance'.

"Katika Benki ya NMB, tunaamini kuwa usawa wa kijinsia unaweza kupatikana kwa kuchukua hatua. Ndiyo maana tunaendeleza dhamira yetu ya kuunda masuluhisho ya kifedha ambayo yanajumuisha na kushughulikia mahitaji ya makundi yote - ikiwa ni pamoja na wanawake katika jamii zetu," alisema.

Aliongeza kuwa benki yake inakaribia kufikia uwiano wa kijinsia wa 50/50 na kuthibitisha dhamira ya benki yake ya kuendeleza usawa wa kijinsia mahali pa kazi.

Teggisa alisema kuwa mwaka huu, Benki ya NMB imetoa hati fungani, maarufu kama NMB Jasiri Bond, ambayo inalenga biashara zinazoongozwa na wanawake kama sehemu ya dhamira yake ya kuongeza mikopo kwa wanawake.

# Jela maisha kwa kumlawiti mtoto

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

MKAZI wa Kitongoji cha Kashai, mjini Sumbawanga, Alex Augustine, amehukumiwa kifungo cha maisha jela baada ya kukutwa na kosa la kumlawiti mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka tisa.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Sumbawanga, Uutor Bigambo, baada ya kusikiliza pande zote na kujiridhisha na ushahidi uliotolewa pasipokuacha shaka.

Alisema mshtakiwa alitenda kosa hilo kati ya Novemba 2020 hadi Novemba 27, 2021, katika kitongoji cha Kashai, mjini humo.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa mtuhumiwa ambaye alikuwa ni dereva bodaboda alikuwa na utaratibu wa kumpokea mtoto kutoka katika moja ya basi la shule na kumpeleka nyumbani.

Alisema mara kadhaa baada ya mshtakiwa kumpokea mtoto huyo alikuwa akimpeleka katika moja ya nyumba ambayo bado haijaisha (pagale) na kuanza kumwingilia kinyume na maumbile huku akimtishia asiseme kwa wazazi wake kwa madai akithubutu kufanya hivyo atamuua.

Hakimu huyo alisema wakati mshtakiwa akiendelea kufanya kosa hilo, ilibainika kwamba mtoto akilalamika maumivu makali ndipo walipomuhoji na kueleza kile anachofanyiwa na kijana huyo.

Wazazi wa mtoto huyo walimchukua mtoto na kutoa taarifa polisi na kwenda kupimwa hospitali, ambako ilibainika analawitiwa na sehemu yake ya haja kubwa imeanza kuharibika.

Mshtakiwa Augustine alikimbia kuelekea mkoani Katavi alikokaa kwa miezi kadhaa, lakini polisi walimkamata.

Upande wa mashtaka ulipeleka mashahidi wanane ambao walithibitishia Mahakama namna kijana huyo alivyomtendea mtoto huyo ukatili.

Awali, Mwendesha Mashitaka, Marietha Maguta akisaidiwa na Ashura Ally, waliomba Mahakama itoe adhabu kali ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hizo.

Mguta alisema vitendo hivyo vya ukatili dhidi ya watoto vinapaswa kukemewa kwa kuwa vimekuwa vikiwaletea athari za kiafya na kisaikolojia watoto wanaowafanyia vitendo hivyo.

Akitoa utetezi wake wa mwisho, Augustine alidai yeye ni tegemeo katika familia na kuiomba mahakama impunguzie adhabu.

Hata hivyo, Hakimu Bigambo alisema kutokana na maelezo ya pande zote mbili inathibitisha alitenda kosa hilo na utetezi wake (Agustino) hauna mashiko Mahakama inamhukumu kifungo cha maisha jela.

# 'Jamii imlinde mtoto wa kike dhidi ya unyanyasaji'

**Na Jenifer Gilla**

MKURUGENZI wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben, amesema jamii inapaswa kuendelea kuibua na kuchukua hatua dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa mtoto wa kike, ili kumsaidia kutimiza ndoto zake.

Dk. Rose aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati chama hicho kwa kushirikiana na Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT-T) kilipoadhimisha Siku ya Mtoto wa Kike Duniani.

Alisema wamebaini licha ya vyombo vya dola kuchukua hatua na kupinga vikali vitendo hivyo, bado matukio hayo yanazidi kushamiri huku watuhumiwa wengi wakiwa ni wazazi, walezi, walimu na watu wao wa karibu waliopewa jukumu la kulinda watoto hao.

Alitaja baadhi ya matukio hayo kuwa ni rushwa ya ngono, ubakaji, vipigo na ndoa za mapema kwa mtoto ambayo kwa kiasi kikubwa yanachangia kurudisha nyuma maendeleo ya mtoto wa kike. "Kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, mwaka huu, kumeshuhudiwa kuwapo kwa matukio kadhaa ya ukatili wa kijinsia kwa mtoto wa kike hali inayoleta wasiwasi kuwa huenda elimu ya kulinda haki ya mtoto wa kike bado haijawafikia wengi," alisema.

Alitaja moja ya matukio hayo kuwa ni mwanafunzi wa darasa la saba, Shule ya Msingi Shahede, Geita Helen Mashaka (13) anayedaiwa kuchomwa moto mikononi na mama yake hali iliyosababisha kushindwa kufanya mitihani yake ya darasa la saba.

Vilevile alisema kuwa Chama hicho kwa kushirikiana na WFT-T mwaka 2021 walifanya utafiti na kubaini wanahabari wanakabiliwa kwa kiasi kikubwa na rushwa ya ngono na ukatili mwingine ndani ya vyombo vya habari.

"Hivyo basi kwa kuzingatia umuhimu wa siku hii, TAMWA kwa kushirikiana na WFT-T tunaikumbusha jamii, wadau na serikali kuwa bado matukio ya ukatili wa kijinsia kwa watoto wa kike yanaendelea kushika kasi nchini," alisema.

Mkurugenzi wa Mtendaji wa WFT-T, Rose Marandu, alipongeza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa kufanya mabadiliko ya kifungu cha 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na 11 ya Mwaka 2007 ikiwa na dhamira chanya ya kushughulikia uovu huo nchini.

Hata hivyo, Mkurugenzi huyo aliiomba taasisi hiyo kuondoa kifungu kidogo namba 2 cha sheria hiyo kinacholeta utata kati ya neno rushwa ya ngono na ukahaba.

"Tunaiomba serikali kupitia TAKUKURU kuendelea kujikita katika mapambano haya wakishirikiana na wadau ili jamii iwe na taarifa za kutosha kuhusu usalama wa watoto wa kike," alisema Rose.

Naye Ofisa wa Polisi kutoka Dawati la Jinsia na Watoto Kanda Maalum ya Polisi Dar es Salaam, Doris Gweba, alisema changamoto iliyopo katika jamii ni utoaji wa taarifa sababu kuu ikiwa ni uoga hasa kwa watoto, kwa kuwa wanaofanya vitendo hivyo ni watu wao wa karibu.

Utafiti uliofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia watoto (UNICEF) umebaini kuwa wasichana milioni 120 duniani wamewahi kulazimishwa kufanya ngono bila ridhaa yao.

Siku ya mtoto wa kike duniani inaadhimishwa Oktoba 11, kila mwaka ili kukumbuka nafasi ya mtoto wa kike katika nyanja mbalimbali za kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni, kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Muda wetu ni sasa, haki zetu, mustakabali wetu'.

RIPOTI MAALUM -2

# Bwana harusi alivyouawa kwa risasi akivua samaki mgodini

**Na Mwandishi Wetu,** aliyekuwa KISHAPU

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana ilikuwa na ufafanuzi kuhusu mauaji ya kijana Hamis Mayunga (19), aliyepigwa risasi na walinzi wa mgodi na kuzima ndoto za wazazi wake kumwozesha. Endelea kupata undani wa hatua zinazojiri.**

**UONGOZI KIJIJINI**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Dulisi, Mosses Nshimba, anakiri wamekuwa wakifuatilia hatima ya suala hilo, lakini hakuna kinachoendelea katika hatua zinazopaswa kuchukuliwa na polisi.

"Tunaviomba vyombo vya habari vitusaidie kupaza sauti ili familia ya kijana huyu ipate haki juu ya kifo cha kijana wao," anashauri.

Ibara ya 8(1)(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inatamka: "Wananchi watashiriki katika shughuli za serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba". Je, wananchi wa vijiji vinavyozunguka migodi ya almasi wilayani Kishapu wanatimiza wajibu huu katika kulinda uwekezaji?

Katika hilo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Dulisi, Nshimba, anasema kutokana na kushamiri matukio hayo ya mauaji, hatua mojawapo waliyochukua ni kutoa elimu kwa umma kupitia mikutano ya hadhara kijijini, ili kudhibiti uingiaji migodini kuchimba madini na kuvua samaki.

Hatua hiyo ya serikali ya kijiji inapata ufafanuzi na uungwaji mkono kutoka kwa Diwani wa Sekebugolo, Frednand Mpogomi, anayesema elimu hiyo iliyotolewa kwa vijiji vyote 12 vinavyoizunguka migodi hiyo, imesaidia kudhibiti matukio ya mauaji migodini.

"Tumewapa elimu na tahadhari wananchi kwamba wakiingia ndani ya mgodi ni kosa kwa sababu mgodi upo kisheria, hivyo watafute vyanzo vingine vitavyowaingizia mapato," Diwani Mpogomi anasema.

**USALAMA WA SAMAKI**

Nipashe ilipohoji kwa Ofisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Sabinus Chaula, kama samaki waliomo kwenye bwawa la mgodi ni salama kuliwa na binadamu, alijibu hawajajiridhisha kuhusu suala hilo.

"Nikiri tu kwamba hatujafanya utafiti ili kujiridhisha kuhusu usalama wa samaki walioko kwenye bwawa la Mgodi wa El-Hilali. Kuna haja kufanyika utafiti ili kujiridhisha usalama wake," Chaula aliiambia Nipashe wilayani Kishapu Septemba 28, mwaka huu.

Hata hivyo, Msimamizi wa Mgodi wa El-Hilali, Hemed Hamdani, anadai samaki wanaovuliwa kwenye bwawa la mgodi wao, ni salama kiafya kwa kuwa hawatumii kemikali katika kuzalisha almasi.

"Samaki waliopo kwenye bwawa letu ni salama kuliwa na binadamu kwa sababu migodi ya almasi haitumii kemikali zinazotumika kwenye uzalishaji wa dhahabu," anafafanua.

Hamdani anayekiri kutokea mauaji ya vijana wawili mgodini kwao mwaka huu, anasema moja ya hatua walizochukua kudhibiti matukio hayo ni kutoa eneo kwa ajili ya wananchi kufanya shughuli za uchimbaji madini.

Anasema vijana wamekuwa wakivamia kwenye mgodi huo kwa ajili ya kuiba mchanga wa madini ya almasi na kuvua samaki kwenye bwawa ili wakauze na kupata fedha.

"Kuingia kwenye mgodi bila kibali ni kosa kisheria na ndiyo maana husababisha malumbano na walinzi na kufikia hatua ya kuumizana.

"Tumetoa elimu kwa walinzi wetu wa mgodi kuacha matumizi ya nguvu pale watakapokuwa wanawakamata vijana wanaoingia mgodini kinyume cha taratibu. Kwa sasa wamepunguza kuingia kwa wingi, kuna wachache ambao ni vichwa ngumu," Hamdani anabainisha.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi.

**DC KISHAPU**

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, anaifafanulia Nipashe kwamba baada ya kupokea taarifa ya mkasa huo, mara moja aliichukua safu nzima ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya kwenda eneo la tukio kupata ukweli wa kilichojiri na kuvuma.

Mkude anayekiri pia kufahamu tukio lingine kama hilo la mwezi Machi, mwaka huu, anaeleza walipata ufafanuzi wa kina toka uongozi wa mgodi ambao nao anasema ulikiri kulifahamu.

Anasema baada ya hapo, waliagiza polisi kuchukua hatua za kisheria mara moja, na wakati huo huo uongozi wa mgodi kuchukua hatua za ziada kutenga eneo maalum lenye ukubwa wa ekari 2,000 kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

**KUTOKA POLISI**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, anakiri kutokea kwa mauaji ya Hamis, akiwa na ufafanuzi kwamba kijana huyo aliuawa kwa kupigwa risasi kifuani na mlinzi wa kampuni ya Samu Securty, Emmanuel Chacha.

Anasema mlinzi huyo alimuua Hamis kwa kutumia silaha aina ya Shotgun na alitoroka kazini baada ya mauaji hayo, akitelekeza silaha kwenye lango la mgodi. Alisema jeshi hilo linaendelea kumtafuta ili limkamate na kumfungulia mashtaka ya mauaji hayo.

Nipashe ilipokwenda kupata ufafanuzi kutoka Kampuni ya Samu Security mjini Shinyanga kuhusika kwao na mkasa huo, ofisa wake, Salum Nkana alikiri mlinzi wao kuhusika na mauaji hayo.

Nkana anaeleza kwamba mlinzi huyo baada ya tukio hilo alitoweka na silaha aliyoitelekeza kwa sasa inashikiliwa na polisi kwa hatua za kiuchunguzi.

Hata hivyo, ofisa huyo hakuwa tayari kutoa ufafanuzi kuhusu kampuni hiyo kutoa Sh. 200,000 kuwezesha maziko ya mwili wa Hamis.

**RIPOTI YA HOSPITALI**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, Dk. John Luzila, anakiri kuupokea mwili wa kijana Hamis Mei 21, mwaka huu, akiwa tayari amefariki dunia katika maelezo yasiyopishana na ya polisi.

Kwa mujibu wa daktari huyo, uchunguzi wa kitabibu unaonesha kuwa Hamis aliumizwa kifuani na walitoa kibali cha kumzika Mei 24, mwaka huu.

Nipashe imekiona kibali hicho chenye namba 046/21/5/022, kikibainisha kifo cha Hamis kilitokea Mei 20, 2022, chanzo kikiwa majeraha ya kifuani.



BURIAL PERMIT
NAME Hamis Mayunga NO. 046/21/5/2022
AGE 19 yrs SEX M NATIONALITY TRIBE Sukuma
(if unknown, state child, adult or aged person).
DATE OF DEATH 20/5/2022 RELIGION ... CAUSE OF DEATH (1) Chest injury
Certified/ notified by DR
HEALTH OFFICE
SRRH
Medical officer of health
Section 44 of the TOWNSHIP Rules, 1923-(4) no person shall burry, cremate of otherwise dispose of the corpse of any person who has died within the township without a permit signed by the medical officer of health or if there be no medical officer of health by a government medical officer or in default by and administrative officér.

Kibali cha kuuzika mwili wa Hamis Mayunga kilichotolewa na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga.

**JICHO LA KISHERIA**

Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inatamka: "Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria".

Kwa kuzingatia ibara hiyo, Wakili wa Kujitegemea, Frank Chacha, anaeleza mkasa wa mauaji yaliyofanywa kwenye Mgodi wa El-Hilali, ulivyoshughulikiwa unakinzana na sheria.

Anafafanua: "Mwananchi anapoingia mgodini kwa lengo la kuchimba madini kinyemela, polisi au walinzi wa mgodi hawapaswi kumuua, bali wanapaswa kumkamata na kumpeleka kituo cha polisi, ili hatua zingine za kisheria zichukuliwe dhidi yake.

"Kumuua ni kwenda kinyume cha sheria, kwa sababu mtu anakuwa mkosaji pale tu inapothibitika mahakamani kwamba ametenda kosa kwa mujibu wa sheria."

Mkurugenzi wa Shirika la Agape linalojihusisha na utetezi wa haki za binadamu mkoani Shinyanga, John Myola, anachangia hoja hiyo, akilaani mauaji katika mgodi huo kwa kuwa yanapoteza nguvu kazi ya taifa.

Anafafanua kwamba kuwapo kwa mgodi huo kisheria, hakutoi uhalali kuwapiga risasi washukiwa wa makosa wakati wanataka kuwakamata, kwa kuwa ni tukio linalokiuka haki za binadamu.

Anapendekeza watu wanaovamia mgodini wakamatwe na kufikishwa mahakamani ili kuchukuliwa hatua za kisheria na sio walinzi wa mgodi kujichukulia sheria mkononi kwa kuwapiga risasi na kuwaua.

"Ndani ya mwaka huu kwenye Mgodi wa El-Hilali yametokea matukio mawili ya vijana kuuawa kwa kupigwa risasi. Mauaji haya yadhibitiwe," Myola anasisitiza.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, analaani matukio hayo na kutoa tamko rasmi la kituo hicho, akisema:

"LHRC tunakemea na kulaani mauaji yanayofanywa na askari wanaolinda Mgodi wa El-Hilali. Mauaji hayo yamekiuka haki za binadamu kwani haki ya kuishi imeathiriwa, na askari hao wasipodhibitiwa wataendelea kufanya matendo hayo.

"Jeshi la Polisi liwajibike kutekeleza jukumu lake la kikatiba la kulinda usalama wa raia na mali zao, lihakikishe washukiwa wa matukio hayo ya mauaji wanatafutwa na kufikishwa mbele ya sheria.

"Vilevile, serikali iangalie kwa umakini leseni na mwenendo wa kampuni hiyo kwani imekuwa ikihusishwa na vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu, hasa haki ya kuishi.

"Kila mtu ana haki ya kuishi na kufurahia rasilimali za nchi yake kwa manufaa ya Watanzania. Rasilimali tulizonazo zikawe tija kwenye maendeleo ya nchi na sio chanzo cha kupokwa kwa uhuru binafsi na haki ya kuishi. "

# TANGAZO

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF WATER**

**REQUEST FOR EXPRESSIONS OF INTEREST**
**(CONSULTING SERVICES – FIRMS SELECTION)**

## DODOMA RESILIENT AND SUSTAINABLE WATER DEVELOPMENT AND SANITATION PROGRAM, PHASE I

## CONSULTANCY SERVICES FOR PREPARATION OF CATCHMENT PROTECTION AND MANAGEMENT PLAN

**MINISTRY OF WATER**
Financing Agreement Reference: **2100150042943**
Project ID No.: **P-TZ-E00-011**

**REFERENCE NO.: ME-011/2022-2023/C/15**

1. The **UNITED REPUBLIC OF TANZANIA** has received financing from the African Development Bank toward the cost of Dodoma Resilient and Sustainable Water Development and Sanitation Program Phase I and intends to apply part of the agreed amount **for this loan to payments under the contract for preparation of catchment protection and management plan.**

2. The services included under this assignment are:
   a) Facilitate Demarcation and Protection of Water source areas.
   b) Investigation and recommendation of the right conservation measure(s) to be undertaken.
   c) Facilitate planting of 75 hectares of trees for watershed and soil conservation
   d) Facilitate establishment of catchment committees and training in conservation and climate change and adaptation

3. The estimated input time for the preparation of the catchment protection and management plan is twenty- four (24) calendar months.

4. The Ministry of Water (MoW), the executing agency of this project now invites eligible consulting firms to express their interest in providing the above services. The Consulting firm must provide information indicating that they are qualified to perform the services (brochures, description of similar assignments, experience in similar conditions, availability of appropriate skills etc.). Consultants may constitute joint-ventures to enhance their chances of qualification.

5. Eligibility criteria, the establishment of the short-list and the selection procedure shall be in accordance with the African Development **Bank's Bank's Policy Framework dated October 2015, which** is available on the Bank's website at **http://www.afdb.org.**

6. Interested consultants may obtain further information at the address below during office hours from 8:00 to 15:30 hours, Monday to Friday inclusive, except on public holidays.

7. Expressions of interest must be delivered to the address below in person, or by courier by Friday 11th November, 2022 at or before 14:00 hour local time and clearly marked **EXPRESSION OF INTEREST FOR CONSULTANCY SERVICES FOR PREPARATION OF CATCHMENT PROTECTION AND MANAGEMENT PLAN. Electronic Submission is not acceptable.**

   **Physical Address is:**
   The Secretary Ministerial Tender Board
   Ministry of Water,
   Kolon Building adjacent to DUWASA Head office, PMU Offices,
   Chimwaga Road,
   **Dodoma,** Tanzania
   E-mail: pmu@maji.go.tz

**Permanent Secretary**
**Ministry of Water**

217085502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**

## TAARIFA KWA UMMA

## HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA SERIKALI KATIKA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO YA WALIOKUWA WAFANYAKAZI WA KAMPUNI YA BARRICK

Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, imekuwa ikipokea na kushughulikia malalamiko ya waliokuwa wafanyakazi wa Kampuni ya Barrick ambao waliachishwa kazi kwa nyakati tofauti kuanzia mwaka 2007. Malalamiko hayo yalihusiana na wafanyakazi kutopimwa afya wakati wa kuachishwa kazi, kutopatiwa huduma ya matibabu na kutopewa malipo ya fidia kutokana na ajali au magonjwa waliyoyapata kutokana na kazi.

Malalamiko hayo yameshughulikiwa katika hatua mbali mbali, kupitia Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi (OSHA), Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) na Idara ya Kazi. Hata hivyo, wafanyakazi hao waliendelea kuwasilisha malalamiko katika mamlaka mbalimbali za Serikali wakidai kutoridhishwa na hatua zilizochukuliwa.

Kutokana na hali hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ilichukua hatua mbalimbali za kiutawala (administrative measures) ili kuyapatia ufumbuzi malalamiko hayo. Hatua hizo ni pamoja na kuunda Timu Maalum mwaka 2021 na 2022 zilizojumuisha wataalam kutoka katika Taasisi mbalimbali za Serikali, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) kwa lengo kufanya uchambuzi wa kina wa malalamiko ya wafanyakazi hao na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuyahitimisha.

Timu husika zimeshughulikia jumla ya walalamikaji **427,** kati yao walalamikaji 150 walishughulikiwa mwaka **2021 na 277 mwaka 2022.** Hata hivyo, kati ya walalamikaji **277** wa mwaka 2022, walalamikaji 47 walishashughulikiwa na Timu ya mwaka 2021. Aidha, mwaka 2022, kabla ya Timu kuanza kazi, mwezi Mei, 2022 Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ilitoa tangazo kupitia Vyombo vya Habari kuwataka waliokuwa wafanyakazi wa Kampuni ya Barrick wenye malalamiko ambayo hayajawahi kuwasilishwa na kutolewa maamuzi na vyombo vya Serikali, kuwasilisha malalamiko yao ili yafanyiwe kazi.

Timu iliyoundwa imekamilisha uchambuzi na kuwasilisha taarifa kwangu. Katika taarifa hiyo imeainishwa kuwa wapo walalamikaji waliobainika kuwa na magonjwa yanayotokana na kazi na hivyo mwajiri atawajibika kuwapatia matibabu, wapo wenye magonjwa yatokanayo na kazi na wamefikia ukomo wa kuimarika afya zao na hivyo mwajiri atatakiwa kuwafanyia taratibu za kuwalipa fidia. Vilevile, wapo waliobainika kuwa na magonjwa yasiyotokana na kazi.

Kwa kuzingatia matokeo hayo, walalamikaji wote waliowasilisha malalamiko yao watapatiwa majibu yao kwa barua ndani ya siku kumi za kazi baada ya kutoka tangazo hili. Barua hizo zitatolewa kupitia Ofisi za Idara ya Kazi za Mikoa au Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama kwa kutumia anuani walizobainisha katika barua zao za malalamiko. Aidha, yeyote ambaye atapenda kupata barua kwa njia tofauti na zilizoelezwa, awasiliane na Ofisi ya Kamishna wa Kazi kupitia namba ya simu **0655 544 489.**

Ninapenda kutoa taarifa kuwa nimemtaka mwajiri kuweka Dawati/Ofisi maalum kwa ajili ya kusikiliza na kutatua malalamiko na kero za wafanyakazi. Nimearifiwa kuwa Mwajiri ameshatekeleza agizo hilo, ambapo amefungua Ofisi maalum katika eneo la Boomgate Bulyanhulu (Nje ya mgodi). Hivyo, niwatake wale wote wenye malalamiko dhidi ya Kampuni ya Barrick kufika katika Dawati/Ofisi hiyo kuwasilisha malalamiko yao ili yaweze kufanyiwa kazi. Aidha, Uongozi wa Kampuni uandae utaratibu wa namna ya kupokea malalamiko kwa kutoa namba ya simu maalum na watumishi ambao watashughulikia malalamiko.

Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Idara ya kazi, Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) zitaendelea kushughulikia malalamiko ya wafanyakazi nchini kwa mujibu wa Sheria za Kazi.

Aidha, Ninapenda kuchukua fursa hii kuwakumbusha Waajiri wote nchini kuwa Wakala wa Afya na Usalama Mahali Pa Kazi (OSHA) ndiyo yenye mamlaka kwa mujibu wa Sheria ya Usalama na Afya Mahali Pa Kazi Na. 5 ya 2003 ya kupima afya za wafanyakazi ili kubaini endapo wana madhara yaliyosababishwa na kazi wanazofanya.

Ninatoa rai kwa waajiri na wafanyakazi katika Sekta ya Madini kutekeleza wajibu na majukumu yenu kwa Uadilifu na kufuata misingi ya kitaaluma kwa lengo la kudumisha Mahusiano mema pahala pa kazi na hivyo kuepuka kuwepo kwa malalamiko na migogoro isiyo ya lazima ili kujenga nguvu kazi shindani na Maisha bora.

**Imetolewa na:**

**Prof. Jamal A. Katundu**
**KATIBU MKUU**

**11 Oktoba, 2022**

217087302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mtoto wa kike alindwe, asikatishwe ndoto zake

**MAADHIMISHO** ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani na kaulimbiu yake ya 'Sauti Yangu, ni Usawa wa Baadaye' ni muhimu katika kumthamini na kumwezesha kufikia malengo aliyojiwekea katika maisha yake.

Changamoto kubwa wanayokabiliana nayo watoto wa kike ni vikwazo vya safari yao ya kuelekea utu uzima, huku mimba na ndoa za utotoni zikiwalazimisha kuacha shule na kukatisha ndoto zao za elimu.

Hivyo ni jukumu la kila mtu kuchukua hatua na kuwapa fursa watoto wa kike kutimiza ndoto zao na kuimarisha maisha yao.

Kitu kibaya kinachosikitisha ni kuona watoto wengi wa kike hukatishwa ndoto zao na watu wa karibu tena kutoka ndani ya familia.

Takwimu kwa upande wa Tanzania Visiwani zinaonesha kwamba jumla ya matukio 1,222 ya udhalilishaji yaliyoripotiwa kwa mwaka 2021 kati ya hayo 846 ni wasichana sawa na asilimia 79.2.

Kwa mwaka huu wa 2022 kuanzia Januari hadi Agosti jumla ya matukio 695 ya udhalilishaji yameripotiwa, kati ya hayo 481 ni wasichana.

Kiwango hicho ni kikubwa ikilinganishwa na idadi ya watu waliomo visiwani humo na hiyo ni miongoni mwa changamoto zinazokwamisha mwelekeo wa ndoto za watoto.

Udhalilishaji wa watoto wa kike hujitokeza kwa wingi visiwani humo kutokana na ripoti za matukio yanayoripotiwa mara kwa mara kwenye vyombo vya habari na hata kesi zinazowasilishwa mahakamani.

Watoto wa kike wanakabiliwa na vipingamizi vingi ndani na nje ya familia kwa kufanyiwa vitendo vinavyowasababisha washindwe kufikia ndoto zao za malengo waliyojiwekea.

Katika baadhi ya familia mtoto wa kike hutumika kama kitega uchumi cha kuiletea familia fedha. Mfano mzazi anaweza kuamuru mtoto huyo asiende shule ili aolewe kwa kutegemea mahari ambayo wakati mwingine huwa mifugo au fedha.

Mtoto huyo hupatiwa mume ambaye kiumri hupishana sana na kusababisha mtoto huyo kupata madhara hasa anapopata ujauzito kutokana na viungo vyake kutokomaa.

Wazazi hao wanashindwa kuelewa kuwa mtoto wa kike anapopatiwa fursa ya kuendelea kielimu anakuwa mkombozi mkubwa si kwa familia pekee bali hata kwa jamii inayomzunguka.

Kuna mifano tosha inayoonekana katika jamii mbalimbali watoto wa kike waliopewa fursa ya kuendelea kielimu wanavyoweza kuikomboa familia na vile vile kusaidia wengine kufikia ndoto zao.

Mtoto wa kike akijengewa uwezo ni mlezi mkubwa wa familia na mifano ipo ya kutosha katika baadhi ya familia, watoto wa kike ndio wanaotunza wazazi wao kwa asilimia kubwa.

Mtoto wa kike ameumbwa kuwa na huruma hata anapokuwa na familia yake ni lazima atakumbuka jukumu la kuwatunza wazazi wake.

Dunia sasa hivi inashuhudia watoto wa kike waliowezeshwa wanavyoweza kufanya maajabu na kuwapita hata wenzao wa kiume. Sasa hivi kuna marais wanawake jambo ambalo hapo zamani lilikuwa gumu kutokana na mfumo dume uliojengeka.

Mtoto wa kike ni lazima athaminiwe na kuwezeshwa kutimiza ndoto yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Halfani Chusi

# Elimu itolewe kuepusha kuua watoto kwa vipigo

**KUNA** haja wazazi na walezi kupewa elimu ya malezi ili kupunguza vifo vya watoto wao wanaowaua kwa kuwapa adhabu kubwa au hata ulemavu, kuwaachia makovu na majeraha moyoni kwa kuwapiga kupindukia wakiamini wanawaonya.

Matukio mengi ya wazazi na walezi kuwapiga watoto hadi kuwajeruhi zama hizi yameongezeka na inawezekana ni kutokana na baadhi yao kuwa na hasira, kukereka na hata kuchoshwa na mtoto anayotenda lakini pia wakikosa uelewa wa namna ya kulea hasa unapokasirika.

Katika matukio hayo ukitazama makosa, yanamhusu mtoto wa miaka minne kadokoa mboga au amevunja glasi au wakati mwingine kafanya kosa ambalo halistahili hata adhabu lakini mtoto anaadhibiwa hadi kufariki.

Ili kupunguza mikasa hiyo serikali na wadau wengine wafikirie namna ya kutoa elimu kwa wazazi na walezi hasa kuhusu malezi ya watoto ili kuwaongezea uelewa katika kujua namna bora ya kumdhibiti mtoto akifanya kosa kinyume na kipigo kikali kinachotolewa.

Au hata kama kosa lake linahitaji viboko wataelekezwa maeneo yapi ni sahihi kuwapiga ili yasitokee madhara ikiwamo kuwapa ulemavu au kuwaua.

Siku chache zilizopita tumeripoti matukio mengi wanayofanyiwa watoto na wazazi wanapoadhibiwa kitu ambacho kinabeba tafsiri kwamba yawezekana wengi wao hawana uelewa juu ya kuadhibu na kulea au wamechoshwa au kukerwa na mambo, hivyo kuhamishia hasira kwa watoto wao.

Ikumbukwe kuwa kumwadhibu mtoto si njia pekee ya kumfunza bali zipo nyingi za kutumia kumfundisha mtoto pale anapokuwa amekosea kinyume na kumwadhibu kupindukia.

Mtoto ni mtu anayekariri haraka zaidi kuliko mtu mzima hii ni kutokana na kutokuwa na mrundikano wa mambo mengi kichwani kwa hiyo akili yake hupokea na kupitia hali hiyo inawezekana akaelekezwa na akaelewa na kutii mapema.

Ni dhahiri kwamba taasisi nyingi za kiserikali na binafsi hazijaanza kufikiria upande wa pili wa sarafu kuwa wazazi na walezi wengine wana uelewa mdogo au wanatumia hasira zaidi kuadhibu watoto ili wajiandae kuwapatia elimu kama ilivyo kwenye mambo ya haki za watoto, ukatili wa kijinsia, semina za magonjwa, pamoja na masuala ya rushwa ya ngono ili kuhakikisha haki ya mtoto.

Hivyo kuna haja ya kuandaa mikakati na kulimaliza jambo hilo, ili kuipeleka elimu hiyo mbali hadi kupunguza vifo vya watoto vinavyotokana na kipigo cha wazazi pale wanapowaadhibu.

Kitendo cha mtoto aliyeadhibiwa na mama yake au mlezi kwa kudokoa dagaa na kuiba Sh. 250 hadi kufariki ni adhabu inayojaa fedheha na kuacha kovu kwenye familia.

Lakini katika kuchunguza inabainika kuwa hata wazazi ambao wamejikuta wakiingia kwenye kashfa ya kuua wakiadhibu watoto wao ni wale ambao walipata changamoto kwenye uzazi na huenda ni kupata watoto katika umri mdogo.

Hali iliyowasukuma kuingia katika majukumu bila kujua namna ya kuishi ndani ya majukumu hayo, mambo kama haya yameenea sehemu nyingi hali inayofananishwa na mtotto kulea mtoto mwenzake. Bila shaka katika muktadha huo siyo rahisi huyo mzazi kujua namna bora ya kutunza, kuadhibu na kufunza mwana.

Kivyovyote vile lazima itakuwa tofauti kwa hiyo ili kukikomboa kizazi kijacho kwa manufaa ya kutengeneza taifa bora na lenye watu waliokuzwa kwa usawa kuna haja ya kulibeba hili na kulifanyia kazi kikamilifu, serikali kwa maana ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii ikilipa uzito.

Pamoja kuandaa sheria na kanuni za kuadhibu wazazi na walezi wanaoadhibu kupindukia hata kuua tena kinyume cha sheria kwa vile wengi wao wanafanya bila kujua nini madhara ya baadaye.

HABARI KITAIFA

# Mwalimu madrasa jela miaka 30 kwa udhalilishaji

**Na Mwandishi Wetu**

MWALIMU wa madrasa Kibiti, Twalaha Hassan, aliyehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela amegonga mwamba kujinasua kwenye adhabu, baada ya rufani yake kutupwa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani.

Uamuzi wa Mahakama ya Rufani ulitolewa juzi mbele ya jopo la majaji watatu, Mwanaisha Kwariko, Rehema Kerefu na Jaji Issa Maige baada ya kupitia maombi ya kufanya mapitio.

Ilidaiwa Desemba 16, 2017, Kijiji cha Kikale Kibiti mkoani Pwani, Twalaha alimnajisi binti wa miaka 14.

Siku ya tukio, ilidaiwa binti huyo alikwenda madrasa kumwombea ruhusa mdogo wake kuwa hatafika kusoma kutokana na majukumu ya nyumbani.

Ilidaiwa mwalimu huyo alimlazimisha binti huyo kuingia chumbani na kumziba mdomo na kumnajisi.

Katika Mahakama ya Wilaya ya Rufiji, mrufani alihukumiwa miaka 30 jela, lakini alikata rufani Mahakama ya Rufani na kutupwa.

Mrufani hakukubaliana na uamuzi huo na kukata rufani katika Mahakama ya Rufani akiwa na hoja tisa, ambako pia aligonga mwamba kwa rufani yake kutupwa.

Aliwasilisha tena maombi ya mapitio Mahakama ya Rufani akiambatanisha na kiapo chake akiwa na sababu tatu ambazo ya kwanza ni maamuzi ya Mahakama yaliegemea katika makosa, hayakuzingatia utetezi wa mrufani.

Alidai ushahidi wa mwathirika haukuwa na nguvu ya kuifanya Mahakama imtie hatiani na kumpa adhabu iliyompa.

Muombaji hakupewa nafasi ya kusikilizwa na kujibu hoja za ziada wakati wa usikilizwaji wa rufani.

Alidai hoja zake za maandishi na kesi alizozirejea hazikuzingatiwa na maamuzi ya Mahakama tangu mwanzo yalikuwa batili kwa sababu hukumu ya Mahakama ya chini ilikuwa batili na ilikuwa inakinzana na Katiba.

Jopo hilo la majaji baada ya kupitia hoja za mrufani liliona kwamba muombaji ameshindwa kuthibitisha hoja zake kwa ajili ya kufanyiwa mapitio.

Kutokana na sababu hizo mahakama iliona maombi hayana sifa na kutupilia mbali.



Rais mstaafu Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, akimsikiliza Ofisa Utawala wa Kampuni ya Uundaji wa Magari ya GFA, Patrick Semiono (kushoto), alipotembelea banda la kampuni hiyo katika maonyesho ya viwanda, Kibaha, mkoani Pwani hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# UN yampongeza Rais Samia usawa kijinsia

**Na Salome Kitomari**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake (UN Women), limempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kukuza usawa wa kijinsia nchini, huku kukiwa na fursa za kuwanufaisha wanawake kiuchumi.

Aidha, wamefurahishwa na ujasiri wa kiongozi huyo kukubali kuwa mwenyeji mshiriki wa mkutano wa Jukwaa la Usawa wa Kijinsia kwa Kizazi utakaofanyika mwakani, baada ya kuzinduliwa rasmi Paris, Ufaransa.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa UN Women, Sima Bahous, baada ya kupokewa katika Ubalozi wa Ufaransa nchini, ikiwa ni ziara ya kikazi na kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike.

Alisema Serikali ya Tanzania imekuwa mshirika wa kipekee kwa kuwa mmoja wa kiongozi mwenza katika hatua za muungano wa haki na haki za kiuchumi na hivi karibuni imekuwa mwanachama wa jukwaa hilo muhimu katika kufikia usawa wa kijinsia.

"Tunaipongeza Tanzania kwa ahadi zake za kijasiri kwa kuona nguvu iliyoko na kutambua umuhimu wa kuwekeza kwa wanawake na wasichana kupitia fursa mbalimbali ambako kutafungua maeneo mengi kiuchumi, pia tunawapongeza kwa kuanzisha kamati ya kitaifa ya ushauri ya kusimamia utekelezaji wa usawa wa kizazi," alisema.

Alisema hatua nyingine kubwa iliyopigwa na Tanzania ni kwenye ushirikishwaji wa sekta binafsi na hivi karibuni Benki ya NMB ilitoa ahadi ya kushiriki kikamilifu kuinua usawa wa kijinsia, mafanikio ambayo ni makubwa na ya kuigwa.

Bahous alisema Tanzania inakuwa mfano wa kuigwa na kiongozi ndani ya jumuiya ya kimataifa katika kuweka wazi ahadi yake ya usawa wa kijinsia na kuleta mabadiliko.

Awali, Kaimu Balozi wa Ufaransa nchini, Axel Guilon, alisema ajenda ya kimataifa ya Ufaransa inatoa kipaumbele cha kukuza usawa wa kijinsia na utekelezaji wa diplomasia ya wanawake na kwa miaka mingi.

"Serikali ya Ufaransa imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na UN Women, ili kupambana na ukosefu wa usawa wa kijinsia na kukuza uwezeshaji wa wanawake na ndio maana Julai mwaka jana, ilishiriki katika Kongamano la Usawa wa Jinsia mjini Paris," alisema.

Alisema zaidi ya watu 400,000 walishiriki na nchi hiyo iliweka mpango wa kimataifa wa kuongeza kasi ya usawa wa kijinsia wa miaka mitano uliolenga kuwekeza Dola za Kimarekani bilioni 40 ulitangazwa.

Vile vile, alisema Tanzania na Ufaransa zimekuwa na mijadala ya kina kuhusu mambo yaliyopendekezwa na jukwaa hilo na yalianza baina ya Rais Macron na Rais Samia, Februari 14, mwaka huu.

Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), limewekeza Euro milioni 900 mwaka 2021 kwa ajili ya miradi inayolenga usawa wa kijinsia katika maeneo ya ukatili dhidi ya wanawake, afya ya ngono na uzazi na uongozi wa wanawake na ushiriki wa kisiasa.

Ufaransa ilitangaza mchango wa Euro bilioni 1.6 kwa ajili ya Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Ukimwi, kifua kikuu na malaria na zilitengwa Euro milioni 255 kwa mashirika mawili yanayotoa programu za uboreshaji huduma kwa wananchi Tanzania.

Mwakilishi huyo alisema miradi ya ubalozi wa Ufaransa inalenga kuwezesha wanawake kwenye ngazi zote kifedha kupitia ushirikiano wa Euro milioni 77 kati ya Proparco (tawi la AFD lililenga kusaidia sekta binafsi), na CRDB kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa wajasiriamali wanawake.

Mingine ni afya, kupitia ushirikiano na UNITAID wenye lengo la kusaidia kinamama wanaoishi na VVU. Pia kiutamaduni kupitia ushirikiano na taasisi za kitamaduni za Kitanzania zinazoshughulikia tofauti za kijinsia katika tasnia ya utamaduni na kukuza wasanii wanawake.

Alisema mwaka 2020 na 2021 Ubalozi uliandaa miradi kadhaa ya pamoja na UN Women Tanzania kwa kukaa pamoja kuangalia mahitaji ya wanajamii.

Naye Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Doroth Gwajima, alisema Tanzania imeingia kuwa nchi kiongozi katika usawa wa kijinsia kutokana na hatua zilizochukuliwa ikiwamo kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu.

## KABWELA



# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

## UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED
## VIWANGO VYA CHINI VYA ADA NA TOZO

| NA | KIPENGELE/MUAMALA | | |
|---|---|---|---|
| SEHEM | AKAUNTI ZA AKIBA | REJAREJA | KAMPUNI/SHIRIKA |
| 1 | AKIBA HURU | | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 15,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | SH 2,000 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | Tozo ya papohapo ni 1,000 | |
| 2 | AKIBA ZA JUMLA | | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 20,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | SH. 5,000 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | SH. 1,000 | |
| 3 | AKIBA ZA MWAJIRIWA | | |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 15,000 USD 15 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | SH. 2,000 USD 10 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa dirishani | SH. 1,000 | |
| 4 | AKAUNTI ZA AKIBA ZA WATU BINAFSI | | |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 15,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | SH. 5,000 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa dirishani | SH. 1,000 | |
| 5 | AKAUNTI YA AKIBA YA MSHAHARA | | |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH.15,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | SH. 5,000 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa kwa dirishani | SH. 1,000 | |
| 6 | AKAUNTI YA FEDHA ZA KIGENI | | |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | USD 10 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | USD 5 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | 1% kwa muamala | |
| 7 | AKAUNTI YA AKIBA YA WATOTO YA U-CARE | | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | USD 15 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | USD 15 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | SH. 1,000 au kiasi kinacholingana na hicho | |
| 8 | AKAUNTI YA MALAIKA | | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 20,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | HAKUNA | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | HAKUNA | |
| 9 | AKAUNTI YA JANJA | | HAKUNA |
| | /Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 20,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | HAKUNA | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | HAKUNA | |
| 10 | AKAUNTI YA KIZAZI KIPYA | | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 20,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | HAKUNA | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | HAKUNA | |
| 11 | AKAUNTI YA HAZINA | | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 20,000 | |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | SH. 20,000 | |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | |
| | Tozo za kutoa pesa | HAKUNA | |
| SEHEM | AKAUNTI YA HUNDI | | |
| 1 | AKAUNTI BINAFSI YA HUNDI | | |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | SH. 30,000 | SH. 100,000 |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | SH.10,000 | SH. 100,000 |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | SH. 10,000 | SH. 12,000 |
| | Kutoa pesa taslimu kwa dirishani | 1 KWA KILA 1,000 | Akaunti SH. 1 KWA KILA 1, 000 |
| | Adhabu ya kutoa pesa zaidi ya kiwango kinachotakiwa | Kiwango cha kuanzia+ 5% | Akaunti ya SH. Kiwango cha kuanzia + 10% |
| 2 | AKAUNTI ZA KIDIPLOMASIA | | |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | USD 100 | HAKUNA |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | USD 100 | HAKUNA |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | HAKUNA | HAKUNA |
| | Kutoa pesa taslimu kwa dirishani | HAKUNA | HAKUNA |
| | Kufunga Akaunti | HAKUNA | HAKUNA |
| | Adhabu ya kutoa pesa zaidi ya kiwango kinachotakiwa | HAKUNA | HAKUNA |
| | Utumaji wa Fedha Nje ya Nchi (TTs) | Kwa kiwango cha chini ni USD 50 kati ya 0.25%, kiwango cha juu USD 200 | HAKUNA |
| | Utumaji wa Fedha Ndani ya Nchi | HAKUNA | HAKUNA |
| | Ubadilishaji wa Fedha za kigeni | Viwango vya bei nafuu vitatumika | HAKUNA |
| 3 | AKAUNTI YA HUNDI YA FEDHA ZA KIGENI | | |
| | Kiasi cha chini cha kufungulia | USD 100/ YURO100/PAUNDI 100 | USD 100/ YURO/PAUNDI 100 |
| | Kiasi cha chini cha uendeshaji | USD100/ YURO100/PAUNDI 100 | USD 100/ YURO 100/ PAUNDI 100/ |
| | Ada ya utunzaji ya kila mwezi | USD 12 au kiasi kinachoendana na hicho | USD 15 au kiasi kinachoendana na hicho |
| | Kiasi cha chini cha kutafutia | USD 25/ YURO 25/PAUNDI 25 | USD 25/ YURO 25/PAUNDI 25 |
| | Kutoa pesa taslimu | 1% kwa muamala | 1% kwa muamala |
| | Kitabu cha Hundi – cha karatasi 25 | USD 10 au kiasi kinacholingana na hicho | HAKUNA |
| | Adhabu ya kutoa pesa zaidi ya kiwango kinachihitajika | Kiwango cha kuanzia + 2%/ Riba ya Mikopo Mikubwa + 2% | Kiwango cha kuanzia+ 2% /Riba ya Mikopo Mikubwa + 2% |
| | TZS Kuhamisha kutoka akaunti ya SH kwenda akaunti ya fedha za kigeni | HAKUNA | HAKUNA |
| SEHEM | AKAUNTI ZA KUWEKA FEDHA | | |
| 1 | Akaunti za Uwekezaji | | Akaunti za Uwekezaji |
| | Kiasi/Kima cha chini cha kufungulia | SH.1,000,000 | SH.10,000,000 |
| | Kiasi/Kima cha chini cha uendeshaji | SH.1,000,000 | SH. 10,000,000 |
| | Kiwango cha Salio linalotakiwa kuwa | Kulingana na makubaliano | Kulingana na makubaliano |
| | Viwango vya Riba | Kulingana na makubalianio | Kulingana na makubaliano |
| 2 | AKAUNTI ZA MUDA MAALUMU | | AKAUNTI ZA MUDA MAALUMU |
| | Kiasi cha chini kuweka - fedha za ndc | SH. 500,000 | SH. 10,000,000 |
| | Kiasi cha chini cha kuweka fedha –US | USD 1,000 | USD 10,000 au kiasi kinacholingana na hicho |
| | Viwango vya Riba | Kulingana na makubaliano | Kulingana na makubaliano |
| SEHEM | HUDUMA ZA BENKI KIELEKTRONI | | |
| 1 | Huduma za Benki Kielektroni | | Huduma za Benki Kielektroni |
| | Ada ya kila mwezi ya huduma za ben | SH 2,000 kwa Mwezi. | SH.10,000 kwa Mwezi |
| | Huduma za Benki za kimtandao (Uto | BURE | BURE |
| | Mfumo wa Benki Kiektroni (Kurejesha | BURE | BURE |
| | Taarifa za kifedha kielektroni (kupakul | BURE | BURE |
| | Manunuzi POS (ndani ya nchi) | BURE | HAKUNA |
| | Manunuzi ya POS (Kimataifa) | BURE | HAKUNA |
| | Utoaji wa fedha kwa POS | SH.1500 | SH. 1500 |
| | Kurejesha muamala wa Mashine ya k | BURE | HAKUNA |
| | Uhamishaji wa fedha/kiwango kwa k | SH.1,000 kwa muamala | SH. 1,000 kwa muamala |
| | Kiwango kwa Kadi | SH.1,000 kwa muamala | SH. 1,000 kwa muamala |
| | /Ubadilishaji wa nywila kwa mkono | SH. 1,500 kwa muamala | SH.1,500 kwa muamala |
| | Huduma za kibenki kwa simu (hudum | SH. 1,000 (0 - 200,000/=) na SH. 2,000 (200,001 - 400,000/=) | HAKUNA |
| | Uhawilishaji wa fedha kutoka kadi mo | SH. 1,500 kwa muamala | SH. 1,500 kwa muamala |
| | Kutoa fedha kwenye benki kupitia wakala | | |
| | 1,000-9,999 | SH. 500 | SH. 500 |
| | 10,000-49,999 | SH. 900 | SH. 900 |
| | 50,000-99,999 | SH.1,200 | SH. 1,200 |
| | 100,000-299,999 | SH. 2,000 | SH. 2,000 |
| | 300,000-499,999 | SH. 3,500 | SH. 3,500 |
| | 500,000-1,000,000 | SH. 4,500 | SH. 4,500 |
| | Kutoa fedha kielekrtoni | 2% ya fedha zote zinazotolewa | 2% ya fedha zote zinazotolewa |
| | Kuweka fedha kielektroni | 1.5% ya fedha zote zinazowekwa | 1.5% ya fedha zote zinazowekwa |
| | Africash /Fedha taslimu za Kiafrika | SH. 6000 + 1.5% ya kiasi chote kilichotumwa/UDS 4.45 + 1.5% ya kiasi chote kitakachotumwa | HAKUNA |
| 2 | Kadi ya Mkopo ya Visa | | HAKUNA |
| | Ada za kutolea | SH. 10,000 | |
| | Ada za kutoa tena | SH. 10,000 | |
| 3 | Kadi za Visa za Malipo ya Kabla | | HAKUNA |
| | Ada za utoaji wa kadi papohapo | SH.12,000 | HAKUNA |
| | Ada za Utoaji wa kadi binafsi | SH. 16,000 | HAKUNA |
| | Ada za utoaji tena | SH. 12,000 | HAKUNA |
| | Ada ya kutoa upya nywila mtandaon | SH. 1,500 | HAKUNA |
| | Ada ya kutoa upya nywila ya mashin | SH. 1,500 | HAKUNA |
| | Ada ya uchakataji | SH.1,000 | HAKUNA |
| | Ada ya ununuzi katika maduka ya mt | BURE | HAKUNA |
| | Ada za manunuzi ya mtandaoni/Tovuti malipo ya mtandao | BURE | HAKUNA |
| 4 | Utoaji wa Fedha kwenye Mashine za Kutolea Fedha | | HAKUNA |
| | Kwenye ATM za UBA (Kwetu) | SH. 1000 | HAKUNA |
| | Kujua/Kuomba Salio kwenye ATM ndc | SH. 200 | HAKUNA |
| | Kuomba Salio kwenye ATM (Kimataifa | SH. 1000 | HAKUNA |
| | Kwenye ATM za benki zingine za ndar | SH. 2,500 | HAKUNA |
| | Kutoa fedha kwenye ATM za Kimataif | SH. 6000 | HAKUNA |
| | Kutoa fedha kwenye ATM za 'Umoja | SH.1,300 | HAKUNA |
| | | | |
| | MIKOPO KWA WATEJA | | |
| | Ada ya uchakataji | 2% | HAKUNA |
| | Ada ya Bima | | HAKUNA |
| | | | |
| | MIKOPO | | |
| | Ada ya kushughulikia mkopo | Kulingana na majadiliano | 2% |
| | Bima binafsi kwa ajili ya mkopo | 1.50% | 1.50% |
| | Ada za kisheria | 0.5% ya kiasi cha chini cha SH. 300,000 | 0.5% 0.5% ya kiasi/ cha chini cha SH. 300,000 |
| | DENI LA OVADRAFTI | | |
| | Ada ya ushughulikiaji | 2% | 2% |
| SEHEM | BIASHARA YA FEDHA | | |
| 1 | Dhamana | | Dhamana |
| | Kamisheni ya Huduma | 2% kwa mwaka (0.5% kwa robo mwaka. Kima cha chini ni USD 250 kwa robo. | 2% kwa mwaka (0.5% kwa robo mwaka. Kima cha chini ni USD 250 kwa robo. |
| | Ada ya huduma | 2% | 2% |
| | Kiasi kilicholipwa | 0.5% kwa robo Kima cha chini ni 250 kwa robo mwaka. | 0.5% % kwa robo mwaka. Kima cha chini ni 250 kwa robo mwaka. |
| | Marekebisho | USD 100.00 tu | USD 100.00 tu |
| | Nyongeza katika robo inayofuata | 0.5% 05% kwa robo (Au % ya kiasi kilichokubaliwa) | 05% kwa robo (Au % ya kiasi kilichokubaliwa) |
| | Ongezeko la kiasi | 0.5% / robo ya 0.5% kwenye tofauti (Au % ya kiasi kilichokubaliwa) | 0.5% /qtr robo ya 0.5% kwenye tofauti (Au % ya kiasi kilichokubaliwa) |
| | Barua za Mopo – Maduhuli | | Letters of Credit – Imports/ Barua za Mopo – Maduhuli/Biasharandani |
| | Kamisheni ya Utoaji | 0.5% kwa robo. Kima cha chini ni USD 250 | 0.5% kwa robo. Kima cha chini ni USD 250 |
| | Ada za uhifadhi | USD 100 tu | USD 100 tu |
| | Tozo za Haraka? | USD 50 tu | USD 50 tu |
| | Marekebisho | USD 100.00 tu | USD 100.00 tu |
| | Barua za Mopo – Mahuruji | | Barua za Mopo – Mahuruji |
| | Kamisheni ya Ushauri ya Barua ya Mkopo | USD 200 tu | USD 200 tu |
| | Marekebisho ya kamisheni ya Ushauri | USD 100 tu | USD 100 tu |
| | Tozo za Haraka za Ulinganifu | USD 50 tu | USD 50 tu |
| | Ada ya uchunguzi na utunzaji wa nyaraka | 0.5% ya kiasi cha Ankara, kima cha chini cha USD 200 | 0.5% ya kiasi cha Ankara, kima cha chini cha USD 200 |
| | Tozo za msimamizi | USD 100 tu | USD 100 tu |
| | Tozo zilizothibitishwa za Barua ya Mkopo | 1.5% kwa robo (kwa barua za utoaji mkopo zilizothibitishwa) | 1.5% kwa robo (kwa utoaji wa barua za mkopo zilizothibitishwa) |
| | /Barua za Ugharamiaji upya wa Mkopo | | Barua za Ugharamiaji upya wa Mkopo |
| | Riba kwenye ugharimiaji upya | /Kiwango cha msingi cha riba + thamani ya 8% kwa mwaka. Kima cha chini ni USD 100 | Kiwango cha msingi cha riba + thamani ya 8% kwa mwaka. Kima cha chini ni USD100 |
| | Kamisheni ya ugharimiaji upya | USD 50 tu | USD 50 tu |
| | Punguzo kwenye Barua ya Mkopo/Ankara/Hundi | | |
| | Riba kwenye upunguzaji | Kiwango cha msingi cha riba + thamani ya 8% kwa mwaka. Kima cha chini ni USD 100 | Kiwango cha msingi cha riba + thamani ya 8% kwa mwaka. Kima cha chini ni USD100 |
| | Riba kwenye upunguzaji | USD 50 tu | USD 50 tu |
| | Punguzo la Bili(Bili za kubadilisha ikiwa ni pamja na Hundi) | | |
| | Punguzo kwenye riba | Kiwango cha kuanzia + 3% ya nchini; Kiwango cha msingi cha riba ya Kimataifa + 8% | Kiwango cha kuanzia + 3% ya nchini; Kiwango cha msingi cha riba ya Kimataifa +8% |
| | Ukusanyaji nyaraka- Mahuruji | | |
| | Ada za uhifadhi | 0.25% ya Ankara ya kima cha chini cha USD100 tu | 0.25% ya Ankara kima cha chini cha USD 100 tu |
| | Tozo za Msimamizi | USD 100 | USD 100 |
| | Kamisheni ya Ulinganifu | USD 50 kwa kila mfuatiliaji | USD 50 kwa kila mfuatiliaji |
| | Ukusanyaji wa Nyaraka – Maduhuli//Biasharandani | | |
| | Kamisheni ya kuhifadhi | 0.25%. Kima cha chini cha USD100 | 0.25%. Kima cha chini cha USD100 |
| | /Tozo za Haraka Zinazolingana | USD 50 | USD 50 |
| | Bili za Nje kwa ajili ya (Makusanyo stahiki & Kodi Zinazolipwa na Mnunuzi) | | |
| | Kamisheni ya Kuhifadhi | 0.25%. ya thamani, kima cha chini USD 75 au kinachofana na hicho | 0.25%. ya thamani, kima cha chini cha USD 75 au kinachofana na hicho |
| | Tozo za DHL | USD 75 tu | USD 75 tu |
| | Hundi za Kigeni Zilizorejeshwa | Tozo zinazodaiwa + Tozo za ndani ambazo hazijalipwa. | Tozo zinazodaiwa + Tozo za ndani ambazo hazijalipwa. |
| | Bili za Ndani kwa Ajili ya Makusanyo | | |
| | Kamisheni ya kuhifadhi | USD 50 tu kwa kila makusanyo | USD 50 tu kwa kila makusanyo |
| | Iliyotozwa Haraka | USD 40 tu kwa kila makusanyo | USD 40 tu kwa kila makusanyo |
| | Miamala ya Ukusanyaji wa Ndani | | Miamala ya Fedha za Ndani |
| | /Malipo ya Uhamishaji wa Nje(TISS) | SH. 10,000 kwa muamala | SH.10,000 kwa muamala |
| | /Marekebisho ya Ada kwa ajili ya uhamishaji wa nje /wa Haraka/ Uhamishaji wa Telegrafu na mteja au benki | HAKUNA | HAKUNA |
| | Uhamishaji wa Haraka wa Ndani (TISS) | HAKUNA | HAKUNA |
| | Miamala ya Fedha za Kigeni | | Miamala ya Fedha za Kigeni |
| | Malipo ya uhamishaji wa Nje /wa Haraka/ wa Telegrafu | Kima cha chini cha USD 50 katikati ya 0.25% ya kima cha juu cha USD 200 | Kima cha chini cha USD 50 katikati ya 0.25% ya kima cha cha juu cha USD 200 |
| | Tozo za Telegrafu za Nje ya nchi/KWETU | Kima cha juu cha USD /YURO/PAUNDI 35-50 TU (KWETU) | Kima cha juu USD/YURO/PAUNDI 35-50 TU (Zinazolipwa kabla) |
| | Marekebisho ya Ada kwa ajili malipo ya ya uhamishaji wa Nje wa Fedha/ wa Haraka/ wa Telegrafu unaofanywa na mteja au benki | USD 10 TU | USD 10 TU |
| | Uhamishaji wa Haraka wa Ndani | USD 5 TU | USD 10 TU |
| | Hawala ya Fedha ya KImataifa | USD 30 kwa Hawala ya fedha ya kimataifa | USD 30 kwa Hawala ya fedha kimataifa |
| | Makusanyo kwa ajili ya Hundi za Kigeni | 0.25% ya thamani. Kima cha chini cha USD75; kima cha juu cha USD 250; | 0.25% ya thamani. Kima cha chini cha USD 75; kima cha juu cha USD 250; |
| | | | |
| 1 | Maelezo | | Maelezo |
| | Kwa mwezi | BURE | BURE |
| | Maombi Maalumu | SH. 1,000/UKRASA | SH.1,000/UKRASA |
| 2 | Utoaji wa Vitabu vya Hundi | | Utoaji wa Vitabu vya Hundi |
| | -Vitabu vya karatasi- 25 | SH. 15,000; USD 10 | HAKUNA |
| | - Vitabu vya karatasi – 59 | SH. 30,000; USD 20 | HAKUNA |
| | - Vitabu vya karatasi – 100 | SH. 45,000; USD 30 | SH. 45,000; USD 30 |
| | Maombi ya Kulipwa kwa hundi | SH. 20,000; USDI 10 | SH. 20,000; USD 10 |
| | Maelezo ya Kusitisha Malipo ya Hundi | Upotevu wa karatasi: SH. 20,000; Upotevu wa kitabu SHTZ 40,000; | Upotevu wa karatasi: SH. 20,000; Upotevu wa kitabu SH. 40,000; |
| | Utoaji wa Hundi ya Meneja | SH. 25,000; USD 20 kwa kipengele. | SH. 25,000; USD 20 kwa kipengele. |
| | Ufutaji wa tozo za Hundi za meneja | BURE | BURE |
| | Kanuni Kuu | | Kanuni Kuu |
| | Uanzishaji wa kanuni kuu | SH. 10,000; USD 10 au kiasi kinachofanana na hicho | SH.10,000; USD 10 au kiasi kinachofana na hicho |
| | Utengenezaji wa Kanuni Kuu | HAKUNA | HAKUNA |
| | Kanuni kuu/ Benki za Kigeni (Tozo za TT) | Kima cha chini cha USD 50; 0.25% ya kima cha juu cha USD 200 | Kima cha chini cha USD 50; 0.25% ya kima cha juu cha USD 200 |
| | Kurekebisha/Kusitisha Kanuni kuu | SH.10,000; USD 10 au kiasi kinachofanana na hicho | SH. 10,000; USD 10 au kiasi kinachofanana na hicho |
| | Kanuni kuu zisizolipiwa | SH. 40,000; USD 40 au kiasi kinachofanana na hicho | SH. 40,000; USD 40 au kiasi kinachofanana na hicho |
| 4 | Fedha kidogo/athari hazipo wazi | | Fedha kidogo/athari hazipo wazi |
| | Fedha Kidogo (Mwone mtoafedha) | SH. 50,000; USD 50 | SH. 50,000; USD 50 |
| | Huduma/Tozo Zingine | | |
| | Kuzirejesha Nyaraka za Nyuma (miezi 2-6) | SH.10,000; USD 10 | SH. 10,000; USD 10 |
| | Kuzirejesha Nyaraka (miezi 6 na kuendelea) | SH. 15,000; USD 15 | SH.15,000; USD 15 |
| | Hati ya Uthibitisho/Ukaguzi/ Cheti cha salio | SH. 30,000; USD 20 au kiasi kinachofanana na hicho | SH. 50,000; USD 20 au kiasi kinachofanana na hicho |
| | Maombi ya hali/Barua ya Kumbukumbu/ | SH. 25,000; USD 25 au kiasi kinachofanana na hicho | SH. 25,000; USD 25 au kiasi kinachofanana na hicho |
| | Uthibitishaji wa hundi nje | USD 500 | USD 500 |
| | Ada za uchakataji wa mshahara | SH. 1,500; USD 1 au kiasi kinachofanana na hicho | SH. 1,000; USD 1 au kiasi kinachofanana na hicho |
| | Uamilishaji wa Akaunti isiyofanyakazi | BURE | BURE |
| | Ada ya Uhifadhi wa fedha taslimu –SARAFU PEKEE | 9% ya fedha iliyowekwa | 9% ya fedha iliyowekwa |
| 6 | Noti chakavu | 3% ya kiasi chote | 3% ya kiasi chote |
| 7 | Sarafu | 3% ya kiasi chote | 3% ya kiasi chote |
| | | | |
| | **approved by:** | | |
| | **Signature:** | **(Signed)** | **Signature: (Signed)** |
| | | | |
| | **Flavia Kiyanga** | | **Benson Msangi** |
| | **Mkuu wa uendeshaji** | | **Mkuu wa Fedha** |
| | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** | | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** |

**Disclaimer: All fees are VAT exclusive.**

217087702

## HABARI KITAIFA

### Viongozi Machinga watakiwa weledi kutumikia nafasi zao

**Na Steven William,** MUHEZA

VIONGOZI wa Bodi ya Shirikisho la Umoja wa Wamachinga (SHIUMA) Wilaya ya Muheza, wametakiwa kutumikia nafasi zao kwa weledi kwa faida ya wanachama na serikali.

Rai hiyo imetolewa na Ofisa Biashara wa Halmashauri ya Muheza, mkoani Tanga kwenye kikao cha wajumbe wa Bodi ya Shirikisho la Wamachinga kilichokutana kupitisha maadhimio mbalimbali ikiwamo maslahi ya wamachinga kwenye wilaya hiyo.

Alisema viongozi wakisimamia misingi vyema itasaidia kupunguza migogoro baina ya wafanyabiashara hao na serikali na kusaidia kukuza maendeleo ya kiuchumi kwenye jamii.

Kaimu Ofisa Maendeleo ya Jamii wilayani humo, John Kwingwa, alitoa ufafanuzi wa mfumo mpya wa kuomba kupata mikopo ya asilimia kumi ambayo hutolewa na halmashauri ikiwa ni agizo la serikali.

Alisema ili kuepusha malalamiko ya utoaji wa mikopo, serikali imeanzisha mfumo mpya wa kuomba kwa kutumia simu janja na kuwataka kwenda kutoa elimu hiyo kwa wamachinga wenzao ili kunufaika na mikopo hiyo isiyo na riba.

Aidha, Mwenyekiti wa wamachinga ngazi ya wilaya, Ally Juma, aliziomba idara za Maendeleo ya Jamii na Biashara kuwapatia elimu na miongozo mbalimbali ambayo itasaidia kwenda kutoa elimu ya kuendesha biashara zao.

Katika hatua nyingine mwenyekiti huo alitoa shukrani kwa serikali kwa niaba ya wafanyabiashara kwa jinsi inavyo shughulikia mchakato wa kuwapatia eneo rasmi la kufanyia kazi zao.

# Serukamba atoa siku 7 waliotafuna mamilioni ya wananchi kurejesha

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ametoa siku saba kwa watumishi wa idara ya fedha ya Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, kurejesha Sh. milioni 365 zinazodaiwa kutafunwa na watumishi na mawakala waliozikusanya kama ushuru na kodi kutoka kwa wananchi.

Watumishi na mawakala hao wanadaiwa badala ya kupeleka fedha hizo benki kwenye akaunti za serikali waliamua kuzitafuna na tatizo linalodaiwa kujitokeza kila mwaka.

Akizungumza na wakuu wa idara, wahasibu na watendaji wa vijiji na kata jana, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ndiyo inayoongoza kati ya halmashauri saba za Mkoa wa Singida kwa watumishi wake kukusanya fedha na kuzitafuna bila kuzipeleka benki.

"Mmeenda kwenye masoko wananchi wema wamelipa ushuru na kodi, lakini mtumishi tuliyekupa jukumu la kukusanya fedha baada ya kuzikusanya badala ya kuzipeleka benki unaamua kuziweka mfukoni maana yake ni kama halmashauri tumekupa mtaji, hili jambo haliwezekani," alionya.

Alisema katika kipindi chake kama kuna mtumishi anadhani hawezi kukusanya fedha za serikali na kuzipeleka benki au halmashauri basi aache kazi hiyo haraka.

Serukamba alisema katika ufisadi huo kuna mambo mawili yanayojitokeza inawekezekana ni njama kati ya wakuu wa idara na wakusanyaji wa fedha hizo kugawana na serikali kukosa mapato.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, alisema tatizo hilo limekuwa sugu katika wilaya hiyo na kutoa mfano kwa mwaka jana watumishi na mawakala walikuwa wanadaiwa zaidi ya Sh. millioni 200, lakini mwaka huu deni limeongezeka na kufikia zaidi ya Sh. milioni 300.

Mwenda alisema wakuu wa serikali walishafika katika wilaya ya Iramba akiwamo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na kuagiza fedha zilizotafunwa na watumishi zirejeshwe, lakini utekelezaji wake umekuwa hafifu. "Jambo hili limekuwa la muda mrefu, mwaka jana watendaji walikuwa wanadaiwa zaidi ya Sh. milioni 200 pamoja na serikali kuchukua hatua kwa watumishi waliohusika, cha kushangaza ufujaji umeongezeka na kufikia Sh. milioni 300 sasa," alisema.

Serukamba baada ya taarifa hiyo alianza kusoma majina ya watumishi na mawakala wanaodaiwa mamilioni hayo ya fedha na kila mmoja kutakiwa kujieleza lini atalipa deni lake.

Hata hivyo, alishtuka na maelezo ya utetezi yaliyokuwa yanatolewa na wadaiwa na kubaini kuna mchezo mchafu (njama) iliyokuwa i metengenezwa kati ya wadaiwa na watumishi wa idara ya fedha.

Aliamua kuwaagiza watumishi wa idara ya fedha kuwafuatilia wadaiwa wote na fedha hizo kuzirejesha ndani ya siku saba na kuahidi kufika katika wilaya hiyo Jumatatu ijayo kuangalia kama fedha hizo zimerejeshwa.

Aidha, alimwagiza Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, Michael Matomora, kufuatilia suala hilo ili fedha hizo zirejeshwe ndani ya siku saba.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba (kushoto), akiwahoji watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba jana, wanaodaiwa kutafuna fedha zaidi ya Sh. milioni 365. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# NGO tano zaiomba serikali kuharakisha mifumo kisheria

**Na Elizabeth Zaya**

MASHIRIKA matano yasiyo ya kiserikali yameiomba serikali kuharakisha kushughulikia mifumo ya kisheria inayozuia upatikanaji wa elimu kwa wasichana na kuruhusu kuolewa wakiwa wadogo.

Wakizungumza katika kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Kike Duniani iliyofanyika Dar es Salaam, walisema bado wasichana wanakumbana na vikwazo vingi vinavyokwamisha ndoto zao.

Nancy Kalembo ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Watoto Tanzania, alisema miongoni mwa mambo yanayokwamisha wasichana wengi kufikia ndoto zao za kielimu ni Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, inayoruhusu mtoto wa miaka 15 kuolewa kwa ridhaa ya wazazi na kuiomba serikali kuharakisha kuifanyia mabadiliko.

Pia alizungumzia gharama kubwa ya taulo za kike kuchangia msichana kushindwa kuhudhuria shuleni kwa siku tatu hadi tano anapokuwa katika hedhi kila mwezi.

"Tutafurahi sana kama serikali italiangalia hili la kuharakisha mabadiliko ya Sheria ya Ndoa na pia kupunguza gharama za taulo za kike. Wasichana wengi wanashindwa kupata fedha ya kununua taulo hizo na hivyo kulazimika kutokwenda shuleni kwa siku tatu hadi tano katika kipindi chote cha hedhi kila mwezi, kwa hiyo tunaomba serikali ilifanyie kazi," alisema Nancy.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Msichana Initiative, Rebeca Gyumi, alisema ni vyema serikali ikafanyia kazi kwa uharaka changamoto zinazowakabili wasichana nchini ikiwamo sheria hiyo ya ndoa ili kuwasaidia kutimiza ndoto zao za kielimu, kuwalinda kiafya na kuwa na furaha.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema tayari timu inakamilisha kazi ya kukusanya maoni kwa ajili ya mapitio ya sheria hiyo ya ndoa na kwamba kazi hiyo itakamilika hivi karibuni.

Kuhusu suala la taulo za kike, Dk. Gwajima alisema wanashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na wadau wengine namna ya kuhakikisha kwamba upatikanaji wake unakuwa rahisi usio na gharama.

"Taulo za kike nalo limeibuka kuwa tatizo linalokwamisha watoto wa kike kuhudhuria masomo, kukosa masomo kwa siku tatu hadi tano si jambo dogo, kwa hiyo tunalifanyia kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara," alisema Dk. Gwajima.

# TTCF yaiomba serikali umakini kilimo cha tumbaku

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa Chama cha Kudhibiti Matumizi ya Tumbaku Tanzania (TTCF), Lutigard Kagaruki, amesema serikali haina budi kufikiria kwa umakini ili kuokoa afya za Watanzania wanaotumia bidhaa za tumbaku.

"Madhara ya kilimo na matumizi ya tumbaku ni makubwa kuliko faida ambayo serikali inapata," alisema Kagaruki.

Alionya kuwa wataalamu wa afya wamebaini kuwa tumbaku ni moja ya sababu kuu za magonjwa yasiyoambukiza kama vile kisukari, mishipa ya damu na moyo, saratani, afya ya kinywa, kupungua kwa nguvu za kiume na matatizo ya akili.

"Mchakato mzima wa kilimo cha tumbaku ni sawa na mtu anayevuta sigara 50 kwa siku," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alisema Shirika la Afya Duniani (WHO) limeweka suala la matumizi ya tumbaku kuwa ni jambo linalopaswa kuchukuliwa hatua kwa kuainishwa kama moja ya haki za binadamu.

Alisema hali hiyo inatokana na matumizi ya tumbaku kuwaathiri watumiaji na wanaoishi karibu nao na hata wanaotumia vitu vinaowazunguka.

Aliyasema hayo wakati wiki iliyopita, Bodi ya Tuambaku nchini ilitangaza mkakati maalumu wa kuhamasisha kilimo cha tumbaku nchini kwa maelezo kuwa kuna kampuni ambazo zimetangaza kuwa tayari kununua kiwango chochote kitakachozalishwa na wakulima nchini.

Kagaruki alitaja madhara mengine ya tumbaku kuwa ni uharibifu wa mazingira kama kufyeka misitu ili kupata kuni, kuongeza kiasi cha sumu kwenye ardhi na kusababisha mazao mengine kushindwa kustawi.

Matatizo mengine alisema ni ukame, ajira kwa watoto na hata kuwanyima haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Alisema anashangaa kuona Tanzania inahimiza kilimo cha tumbaku wakati nchi nyingine za Afrika Mashariki kama vile Kenya na Uganda wamekuwa na sheria zinazodhibiti matumizi ya tumbaku.

Alisema kuna muswada wa sheria ya kudhibiti matumizi ya tumbaku ambao tayari upo Wizara ya Afya lakini umekuwa ukikwamishwa kutokana na ushawishi wa kampuni za tumbaku duniani.

"Na hili ni kwa Tanzania tu. Nchi nyingine zimeshatoka huko. Watanzania tunazidi kuwa hatarini kwa msukumo wa watu wasiowatakia Watanzania kiafya, kimazingira na ustawi wa jamii," alionya Kagaruki.



Mmoja wa mabalozi wa kilevi cha Captain Morgan, akionyesha ishara ya kuzindua kilevi kipya cha 'Captain Morgan Gold', kinachozalishwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Royal Tour yaendelea kuleta watalii nchini

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), limesema kuwa baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuzindua filamu ya Royal Tour kumekuwa na mafuriko ya watalii kwenye maeneo ya hifadhi.

Kamishana wa Uhifadhi wa TANAPA, Willium Mwakilema, alisema hayo juzi alipokutana na wadau wa utalii, wawekezaji na viongozi wa serikali akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, kujadili namna vijana wa Kanda ya Kaskazini wanavyoweza kunufaika na fursa zilizoko kwenye sekta hiyo.

Alisema idadi ya watalii imeongezeka hadi 649,654 kutoka 557,763 kabla ya UVIKO-19 huku mapato yakiongezeka hadi Sh. bilioni 178.4 kutoka Sh. bilioni 165.9.

"Hiki ndicho kiwango kikubwa TANAPA tulichangia kwenye serikali yetu kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, na hili ni jambo kubwa sana ambalo Rais Samia ametutendea Watanzania," alisema Mwakilema.

Aliongeza kuwa baada ya kuingia kwa UVIKO-19 hali ya utalii nchini ilibadilika na walipata wageni 95,012 kutoka 557,763, na kuingiza Sh. bilioni 11.3 pekee, jambo ambalo lilikuwa ni anguko kubwa kwa sekta hiyo.

Mongela, alisema mkoa huo ndio kitovu cha biashara ya vito Afrika Mashariki, na kwamba walipata mtikisiko, lakini kwa sasa wamerudi kwenye nafasi nzuri.

"Tunaambiwa ukiondoa Brazil, kwa maana ya vivutio vya asili, Tanzania tunafuatia, tunaona kabisa hiyo fursa iko wazi, leo ukienda Uwanja wa Ndege wa Kimataifa (KIA) pale, wakati watalii wanashuka pale hakuna kitu ambacho hata mimi mwenyewe nimefurahia kama kuwa huru, bila kuwa na barakoa, unakuta dereva, 'tour guide' (mwongozo utalii) wamechanja, na yeye anakuwa huru," alisema Mongela.

# Kanisa Anglikana lalaani ukatili wa watoto

**Alphonce Kabilondo,** GEITA

KANISA la Anglikana Dayosisi ya Victoria Nyanza, limelaani matukio ya kikatili yanayoendelea kujitokeza nchini, likiwamo la mtoto kuunguzwa mikono na mzazi wake na kushindwa kufanya mitihani yake ya kuhitimu darasa la saba akituhumiwa kuiba kiasi cha Sh. 30,000.

Akizungumza juzi katika ibada ya kipaimara, katika Kanisa la Kristo Mfalme mjini Geita, Askofu Zephania Amos alisema, kanisa hilo linaelimisha waumini kutoa taarifa za matukio ya ukatili kwa vyombo vya dola ili yadhibitiwe.

Askofu huyo alisema maeneo mbalimbali yanatokea matukio makubwa ya ukatili wa jinsia na kwamba ni vyema viongozi wa dini kutimiza wajibu wao kuhimiza waumini kutoa taarifa.

"Ukatili huu unasababishwa na migogoro mingi ya ndoa na mambo mbalimbali likiwamo la hali mbaya ya uchumi katika jamii, hivyo elimu tunayoitoa pamoja na kuliombea taifa sisi kama kanisa tunaomba matukio haya yaripotiwe," alisema.

Aidha, aliwataka waumini kusafisha njia zao kwa kutenda matendo mema yanayompendeza Mungu pamoja na kudumisha amani ndani ya familia, kanisa na taifa kwa ujumla.

Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Kristo Mfalme, Joseph Kitwe, alisema wataendelea kutoa elimu kwa waumini wao kutokana na maelekezo ya kiongozi huyo, na kwamba wapo baadhi ya wanaume wanatendewa ukatili, lakini hawatoi taarifa.

James Mtalitinya, muumini katika kanisa hilo alisema ukatili mwingine unasababishwa na wazazi na walezi kutowalea watoto wao katika misingi ya maadili na kumcha Mungu.



## Ahukumiwa jela miaka 30 kwa kunajisi binti

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara imemhukumu Mkazi wa Kijiji cha Magugu, Shaban Jumanne (20) kwenda jela miaka 30 kwa kosa la kumnajisi binti (16) (jina limehifadhiwa) ambaye ni bubu.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Babati, Victor Kimario, baada ya kusikiliza pande zote mbili.

Alisema Jumanne alikutwa akifanya mapenzi na binti huyo ambaye ni bubu bila ridhaa yake wakiwa chooni Julai 28 mwaka huu nyumbani kwa binti huyo.

Kimario alisema mwathirika wakati anatoka chooni wadogo zake walimsikia analia, kumwona Jumanne akiruka ukuta na wadogo zake na binti huyo wakaanza kupiga kelele.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na binti aliyefanyiwa unyama huo pamoja na wadogo zake ulithibitisha pasi na shaka kuwa mshtakiwa alimbaka binti huyo akiwa chooni.

Kimario alisema mshtakiwa huyo alijitetea mwenyewe.

Alisema mshtakiwa alikiuka kifungu cha 130(1)(2)(e) na kifungu cha 131(3) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 ya Mwaka 2019 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Wakili Peter Utafu akisaidiana na Mwendesha Mashtaka wa Polisi Mkaguzi Msaidizi, Emmanuel Jumbe, walisema licha ya mshtakiwa kutokuwa na rekodi ya matukio ya uhalifu waliiomba Mahakama itoe adhabu kali.

Mshtakiwa Shaban Jumanne alipopewa nafasi ya kujitetea aliiomba mahakama kumpunguzia adhabu kwa kuwa bado ni kijana mdogo na ana familia na wazazi wanamtegemea.

# Wananchi 800,000 Arusha wapata chanjo ya corona

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WANANCHI zaidi ya 800,000 wa Mkoa wa Arusha, wamejitokeza kuchanja chanjo ya UVIKO-19 katika vituo 324 vya kutolea huduma.

Mratibu wa UVIKO-19 wa mkoa huo, Dk. Wilson Boniface, aliyasema hayo juzi wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi wa dini, mila na serikali, kueleza kuwa idadi ya wananchi waliochanja ni sawa na asilimia 69.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Shirika la Kimataifa la Kusaidia Vyombo vya Habari la Internews.

"Lengo letu ni kuchanja wakazi wa Arusha na kufikia asilimia 100 ya walengwa walioko. Asilimia 70 ya watu wenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea wako milioni 1.2, lakini kutokana na idadi ya watu milioni 2.2 walioko mkoani Arusha, waliochanja ni wachache,"alisema.

Alisema ili kuhakikisha wanafikia malengo ya serikali ya watu wote kupata chanjo hiyo, wanaendelea kuhamasisha wananchi kupitia vyombo vya habari, viongozi wa dini, mila na taasisi mbalimbali ili waendelea kujitokeza kwenye vituo vya kutolea huduma kwenda kuchanja.

Kiongozi wa Mila wa Jamii ya Kifugaji ya Kimasai, Amani Lukumay, alisema wamekuwa wakishirikiana na serikali kuhamasisha wananchi kuchanja kwa kuwa chanjo hizo hazina madhara.

"Kupitia vikao vyetu vya kimila, tumeshatoa hamasa na watu zaidi ya 400 walijitokeza kuchanja, hivyo tunawashauri Watanzania wengine wajitokeze kwenda kuchanja na wasitumie dawa ambayo haijathibitishwa na wataalamu wa afya,"alisema.

Shekhe Shaban Juma kutoka Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Arusha alisema wananchi walipitia katika kipindi kigumu kwa kuwa wengi wao hawakuwa na elimu ya ufahamu wa umuhimu wa chanjo hiyo.

Alisema: "Tuliwahamasisha waumini wetu kwenda kuchanja kwa kuwa hakuna sehemu yoyote kwenye vitabu vya dini vimeonyesha kuwa chanjo au kuchanja kuna madhara kwa watu".




Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Alan Kombe (wa nne kulia), akizungumza na wafanyabiashara wa soko la getini Songambele, baada ya kuwakabidhi vifaa vya kuhifadhia taka, wakati wa Wiki ya Huduma kwa Wateja, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wapitisha azimio la kujenga barabara ya changarawe

**Na Allan Isack,** MBULU

WAKAZI wa Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara, wamepitisha azimio la kujenga barabara ya Endamiran hadi Bonde la Heshikesh kiwango cha changarawe, yenye urefu wa kilomita 13.

Wamelazima kuchukua uamuzi huo baada ya serikali kutoikarabati kwa muda mrefu.

Akizungumzia azimio hilo jana, Diwani wa Endamiran, Gesso Bajuta, alisema wananchi wa kata hiyo, wamejitolea kujenga barabara hiyo mpya kwa kiwango cha changarawe.

"Huu ujenzi umegharimu shilingi milioni 120, barabara hii itakuwa mkombozi kwa wananchi wa Endamiran, kwa kuwa awali walikuwa wakipita kwenye miundombinu isiyokuwa rafiki, kwa kutembea umbali wa kilomita 140 kwenda kufuata huduma muhimu za kijamii kama zahanati na soko katika Mji Mdogo wa Hydom," alisema.

Akifafanua zaidi kuhusu azimio hilo, mmoja wa wazee wa mila wa Kijiji cha Endamiran, Anania Hamnay, alisema baada ya ujenzi huo kukamilika, itakuwa fursa kubwa kwao ya kukuza uchumi na kipato cha wakazi wa eneo hilo.

Alisema adha ya ubovu wa miundombinu hiyo, ulisababisha wakazi wa kijiji hicho hasa wajawazito kushindwa hospitalini na kwenye vituo vya afya kuudhuria kliniki au kwenda kujifungua. "Wananchi walikuwa wanateseka sana kwa kukosa huduma muhimu za kijamii kutokana na ubovu wa barabara, lakini kukamilika kwa ujenzi itakuwa sehemu ya kukuza uchumi wa kata yetu na kuongeza kipato kwa mwananchi mmoja mmoja kwa kuwa watakuwa na uhakika wa kupeleka mazao yao kuuza sokoni," alisema.

Aidha, alitumia fursa hiyo kumshukuru diwani huyo kwa kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza ujenzi huo na mashine ya kutengeneza barabara baada ya wananchi kuanza kufyeka pori kwa kutumia zana za jadi.

Diwani wa Kata ya Endamiran, Gesso Bajuta, alisema ameguswa na kutengeneza kwa barabara hiyo kwa kuwa wakazi wa kata hiyo, hawakuwa na miundombinu rafiki na ya uhakika tangu Tanzania ilipopata uhuru.

"Siyo kwamba nina pesa nyingi za kutoa ila nimeona watu wanavyoteseka hasa wanawake waliyokuwa wanatembea zaidi ya kilomita 100 kwenda na kurudi wanapokwenda kutafuta huduma za kijamii imenigusa kwa kufanya hivi nitakuwa nimewasaidia kuondokana na hali hiyo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Sezalia Makota, alisema barabara hiyo, imetengenezwa kwa muda mwafaka katika eneo hilo, kwa kuwa kuna utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo ikiwamo ya elimu.

"Sisi kama serikali hatuna pingamizi kwa kazi hii ya maendeleo iliyofanywa na diwani huyu kwa kushirikiana na wananchi na tutaendelea kuwaunga mkono, pia tunaomba viongozi na wadau wengine kujifunza kupitia kwa wananci hawa," alisema Makota.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, aliwaonya baadhi ya watu wanaofanya siasa za kubeza kazi za maendeleo zinazofanywa na wadau mkoani humo.

Alisema nchi zote zilizoendelea duniani kumekuwapo na ushirikikiano kati ya serikali na sekta binafsi, hivyo kitendo walichofanywa na wananchi hao kwa kushirikiana na mdau huyo ni cha kizalendo na kinapaswa kuigwa na watu wote.

Baada ya kuzindua barabara hiyo, Makongoro, aliikabidhi kwa Wakala wa Barabara za Mjini na Vijiji (TARURA).





# Wanafunzi Shule ya Msingi Pongwe waomba msaada

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WADAU wa sekta ya elimu ndani na nje ya Mkoa wa Tanga wameombwa kujitokeza kuisaidia Shule ya Msingi Pongwe yenye watoto wenye mahitaji maalumu ili kuboresha miundombinu ya elimu.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba, alitoa ombi hilo juzi wakati akikabidhiwa shule hiyo baada ya kumalizika kwa ukarabati wa miundombinu uliofanywa kwa msaada na Taasisi ya Lady Feteemah Trust kutoka Uingereza, ambayo imegharimu Sh. milioni 220.

"Miundombinu hii bado inahitajika sana kwa sababu uhaba wake ni mkubwa sana hasa ukilinganisha na wingi wa wanafunzi walioko shuleni hapo, hivyo nitoe wito kwa wadau wote wa elimu na wengine kuja kutoa msaada katika shule hii kwani ni mahali sahihi," alisema.

Mgumba alisema kwa upande wa vyumba vya madarasa shule hiyo haina uhaba kabisa kwa kuwa ni miongoni mwa shule chache ambazo zimepatiwa mradi wa ujenzi wa vyumba.

"Pamoja na kuwa na wanafunzi 1,213 wanaohitaji madarasa 16 tu, lakini hapa tumejenga madarasa 22, lakini kabla ya ukarabati huo tulikuwa na uhaba mkubwa kwa sababu madarasa mengine yalikuwa yameshapoteza sifa ya kusomeshea watoto wetu," alisema.

"Serikali inawashukuru kwa ukarabati mkubwa wa madarasa 16, bwalo la chakula na jiko, chumba cha huduma ya kwanza, ujenzi wa madarasa mawili, kisima kirefu cha maji, sehemu ya kuchezea watoto wenye ulemavu na matundu matano ya vyoo vya walimu," alisema.

Alisema serikali inatambua msaada huo na kuomba miundombinu hiyo itatunzwe ili iweze kudumu kwa kipindi kirefu, huku akitoa wito kwa viongozi wa Wilaya na Halmashauri ya Jiji la Tanga kuhakikisha wanatekeleza agizo hilo.

"Natoa wito kwa viongozi wa Wilaya na Halmashauri ya Jiji la Tanga pamoja na jamii yote ya shule ya msingi kuhakikisha tunaitunza vyema miundombinu hii, ili iweze kudumu watoto wetu wasome katika mazingira mazuri," alisisitiza.

Shule ya Msingi Pongwe ina wanafunzi 1,213, ni miongoni mwa shule kongwe nchini na ilianzishwa mwaka 1946.

# Naibu Waziri: Wadau tumieni matamasha kukuza utalii

**Na Woinde Shizza** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Pauline Gekul, amewataka wadau wa utamaduni na utalii nchini kuyatumia kimkakati matamasha ya utamaduni yanayoendelea nchini kwa lengo la kukuza utalii.

Gekul aliyasema hayo juzi wakati akizindua Tamasha la Maasai Festival linalotarajia kufanyika Agosti mwakani jijini Arusha, pia aliipongeza taasisi hiyo kwa ubunifu wa kukuza utalii.

Alisema wakati huu ni muafaka kwa wadau kuungana na serikali katika kuongeza mazao ya utalii hapa nchini kwa kuongeza thamani ya shughuli mbalimbali za utamaduni na sanaa zenye upekee ikiwamo za utamaduni wa Kimaasai kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.

"Serikali inathamini juhudi za wadau mbalimbali za kutumia shughuli za utamaduni na sanaa kwa ajili ya maendeleo ya sekta nyingine ndiyo maana Rais Samia alielekeza Januari 22 akiwa Moshi serikali na wadau kuyatumia matamasha kimkakati kukuza utalii," alisema.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana, alisema kwamba Maasai Festival ni bidhaa muhimu ya utalii katika soko la hapa nchini na waandaaji wamethibitisha hilo kwa vitendo kwamba utamaduni na utalii ni kama bidhaa moja.

Aidha, aliwashukuru waandaaji hao kwa kuendelea kukuza na kuimarisha sekta mtambuka kwani Tanzania ni moja ya mataifa yaliotajwa kuwa na utajiri wa kipekee katika sekta ya utamaduni na malikale.

Mkurugenzi wa Wonderland Afrika na View Point Adventures Safaris LTD, Said Maulid alisema zaidi ya wageni 1,500 kutoka mataifa ya Ulaya wanatarajiwa kishiriki tamasha hilo litakaloenda na matukio manne.

Aliyataja matukio hayo ni pamoja na warsha, ukimbiaji wa mbio, onyesho la mavazi na Maasai Festival CSR yote hayo yatakuwa ni matukio yatayofanyika katika Tamasha la Maasai Festival Agosti mwakani.

Alisema: "Natoa wito kwa wadau mbalimbali kuendelea kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kwani tunaona Royal Tour imejibu hivyo tuanzishe na kujenga ubunifu wa kuanzisha matamasha na bidhaa za utalii na utamaduni zitakazosaidia kutangaza nchi yetu kama alivyofanya Rais wetu".




Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Jairy Khanga (kulia), akizungumza na wanafunzi kutoka shule mbalimbali za Manispaa ya Moshi juzi, kuhusu masuala ya afya ya akili wakati wa maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili Duniani, yaliyoandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Akili Chanya Initiative Tanzania (ACIT) kwa kushirikaina na wadau mbalimbali. **PICHA: JAMES LANKA**

# IJA, Mahakama Kuu watoa somo makosa dhidi ya wanyamapori

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

CHUO cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), Mahakama ya Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi inayojihusisha na Uhifadhi wa Mazingira na Usalama wa Wanyamapori (PAMS) kimekutanisha wadau wa haki jinai na kuwanoa juu ya makosa dhidi ya wanyamapori.

Akizungumza jana jijini Arusha wakati akifungua mafunzo ya siku tano ya uendeshaji wa mashauri ya makosa dhidi ya wanyamapori ikiwamo ujangili na makosa yanayohusiana na hayo, Mkuu wa IJA, Jaji Dk. Paul Kihwelo, alisema amezindua mtiririko wa mafunzo hayo ambayo pia yanafanyika kwa makundi mengine.

Alisema mafunzo hayo yamejumuisha majaji wa Mahakama Kuu, waendesha mashtaka waandamizi na wapelelezi waandamizi.

"Kundi la pili litahusu mahakimu, waendesha mashtaka na wapelelezi ambao watapata mafunzo kwa siku tano na kufuatiwa na kundi la tatu la mahakimu, waendesha mashtaka na wapelelezi," alisema.

Alisema wawezeshaji wa mafunzo hayo ni maofisa wa Mahakama ya Tanzania wakiwamo majaji na mahakimu na watumishi kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Mashtaka ya Taifa, Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA).

Alisema lengo lingine ni kuwawezesha kuwa na uandishi bora wa hukumu, utoaji wa adhabu, utekelezaji wa amri za mahakama katika mashauri ya makosa dhidi ya wanyamapori na makosa yanayohusiana na hayo kama usafirishaji wa binadamu na dawa za kulevya.

Kamishna wa Polisi Zanzibar, Amani Hamisi alisema mafunzo hayo yatawajengea uelewa wa pamoja juu ya kusaidia kulinda rasilimali za wanyamapori nchini ili zilete manufaa kiuchumi.



Ukurasa 16

**Mitaala mipya, ufadhili 'Samia Scholarship' unavyoakisi elimu**




Ukurasa 17

Tambo za mwanawe Museveni zinavyoishtua Afrika Mashariki


# siasa

JUMATANO OKTOBA 12, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 19

**MOHAMED MORSI WA MISRI**

**Msomi, mhadhiri vyuoni, mpiganaji shujaa aliyeanguka kufia kizimbani**

MWALIMU NYERERE 1922-1999

# Ndiye mzalendo aliyekataa lami nyumbani, kijijini kwake

• Unajua kwanini? TANRODS, TARURA msimwangushe sasa

**Na Sabato Kasika**



Stephen Wasira. **PICHA: MAKTABA**

WAKATI Watanzania wakiwa katika maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 23 ya kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, ifikapo Ijumaa Oktoba 14, wanakumbushwa kuwa njia bora ya kumuenzi ni kudumisha uzalendo, upendo kwa taifa bila kujali kanda, mkoa wala kijiji kiongozi ulipozaliwa.

Mwalimu anasifika kwa uzalendo na mtu mwadilifu anabakia kuwafundisha Watanzania kuacha kujipendelea, ubinafsi na kuwa wazalendo wa vitendo kwa taifa lao.

Mwanasiasa mkongwe Stephen Wasira, ndiye anayesema hayo katika mazungumzo yake na gazeti hili wiki hii kuzungumzia kumbukumbu ya maisha ya Mwalimu, huku akifafanua kuwa baadhi ya watu wakiwamo pia viongozi, hawafuati misingi aliojasisi, hasa ya kulitumikia taifa kwa uadilifu mkubwa.

"Baba wa Taifa alitaka maendeleo ya Watanzania, si kwa ajili yake ndiyo maana alikataa barabara ya kutoka Makutano hadi Butiama ijengwe kwa kiwango cha lami licha ya kwamba alikuwa na uwezo ,"anakumbusha Wasira.

Anafafanua kuwa ilikuwa ni mwaka 1974 aliombwa kujengewa barabara ya kutoka eneo la Makutano, yenye urefi wa kilomita 24 hadi nyumbani kwake Butiama lakini akakataa, akiwa na sababu moja kuwa yeye ni Rais wa Tanzania siyo wa Butiama.

Wasira anasema badala yake Baba wa Taifa alitaka barabara za lami kwa ajili ya kuunganisha mikoa, ili kuharakisha maendeleo, si sehemu moja ya mkoa kama kutoka eneo la Makutano kuishia nyumbani kwao Butiama pekee akieleza kuwa, ujenzi huo usingekuwa na tija kwa mamilioni ya wananchi waliokuwa hawana barabara katika mikoa hiyo.

"Baba wa Taifa alitamani hata yeye yupo au hayupo duniani, Watanzania wote waendelee kufurahia maendeleo ya nchi yao na si watu wa eneo moja la nchi ama Butiama na mkoa wa Mara kwa ujumla, kuwa na huduma mbalimbali kisa tu yeye amezaliwa huko.

Wasira anasema alitaka barabara ya lami isiishie Butiama, bali iende Nyamuswa, hadi Kijiji cha Sanzati na kisha iunganishwe na mji wa Mugumu wilayani Serengeti na kuwa kiungo kati ya mkoa wa Arusha.

Hata hivyo, anaongeza kuwa Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, sasa ni marehemu aliamua kujenga kilomita 24 za barabara lakini baada ya kifo cha Baba wa Taifa ili baadaye ujenzi zaidi uendelee hadi Mugumu, ili kuunganisha Mara na Arusha.

Katika moja ya mahojiano na wazee wa Butiama waliwahi kuieleza Nipashe kuwa wananchi wa Butiama waliwahi kumhoji kuwa akiwa mzaliwa wa mkoa wa Mara amewafanyia nini watu wa mkoa wake?

Wanasema kuwa Mwalimu aliwajibu kuwa yeye si Rais wa Wazanaki wala Butiama bali ni kiongozi wa Tanzania na kila mmoja anamtazama , akitaka amfanyie jambo, hivyo anawajibika kwa taifa zima siyo kijijini alipozaliwa.

**KUKAMILISHA UJENZI**

Mwanasiasa Wassira ambaye alifanyakazi wakati wa uongozi wa Baba wa Taifa, anasema, baadaye ujenzi wa barabara hiyo ili kutimiza lengo la Baba wa Taifa la kuunganisha mikoa ulianza, lakini anadai kuwa unasuasua na haijulikani utakamilika lini.

Ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kutoka Butiama kupitia Nyamuswa hadi Kijiji cha Sanzati, ulianza lakini kwa kusuasua.

"Umbali kutoka eneo la Makutano hadi Kijiji cha Sanzati, ni kilomita 50, lakini zilipungua baada ya kujenga barabara hiyo hadi Butiama, hata hivyo hizo kilomita 36 zilizobaki imeshindikana kuzimaliza kwa miaka saba," anasema Wasira.

Anadai mbali na ujenzi huo kuchukua miaka mingi, hauko kwenye kiwango na kwamba ipo haja kwa viongozi wa serikali kufuatilia kwa karibuni kubaini ni kasoro gani na kuchukua hatua.

Wasira anasema ubinafsi huchangia kwa kiasi kikubwa kuwapo kwa mfarakano kwa wananchi kati ya aliyekuwa nacho na asiyekuwa nacho, na kwamba Baba wa Taifa aliliona hilo na kulikemea kwa nguvu zake zote.

"Kama Baba wa Taifa angekuwa mbinafsi, Butiama isingekuwa kama ilivyo sasa, angelikuwa na sura nyingi kuanzia miundombinu bora, majengo, upendeleo wa kielimu, tiba na hata utajiri wa kutisha maana rasilimali zote za taifa zilikuwa chini yake na maamuzi yake yasingepingwa.


**INAENDELEA UK. 15**

# Mwinyi achora ramani ya Za
# ni yenye amani, umoja, msh

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

• Aahidi ya kale yamekwisha kuganga yanayokuja




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Rais Hussein Ali Mwinyi. **PICHA ZOTE: RAHMA SULEIMANI.**



RAIS wa Zanzibar Hussein Ali Mwinyi, anakumbusha kuwa anachotaka kuwatendea Watanzania ni kuwaonyesha dhamira ya kweli ya kujenga demokrasia ya maridhiano Zanzibar ili shughuli za kisiasa ziendeshwe katika hali ya amani, umoja, utulivu, mshikamano na maridhiano.

Anaongeza kuwa mambo muhimu ya kufikia maridhiano ya kisiasa na kuzika tofauti za kisiasa visiwani humu ni kuwa na dhamira njema na kukaa pamoja kama watu wa taifa moja na wanaoridhiana na kuheshimiana.

Akifungua,mkutano wa wadau wa demokrasia kujadili masuala mahsusi ya Zanzibar yanayohusu demokrasia ya vyama vingi, anasema tangu kurejea kwa mfumo wa vyama vingi mwaka 1992 Zanzibar imekumbana na changamoto kadhaa kabla, wakati na baada ya uchaguzi mkuu ambazo zimeambatana na uvunjifu wa amani hata kuathiri kasi ya maendeleo.

Mkutano huo unaofanyika mwishoni mwa wiki, Dk Mwinyi anaeleza kukerwa na vuguvugu la kisiasa linaloikumba Zanzibar hasa wakati na baada ya uchaguzi mkuu na baadhi ya watu huhasimiana kwa misingi ya kisiasa.

Katika kusanyiko hilo mada kadhaa zinawasilishwa na wataalamu wabobezi zikihusisha historia ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa Zanzibar, umuhimu wa uzalendo ,uadilifu, kuheshimu sheria na katiba na kudumisha amani katika mfumo wa vyama vingi vya siasa Zanzibar.

Mambo mengine ni masuala mahsusi ya Zanzibar yanayohusu vyama vingi vya siasa na uzoefu kutoka kwa wanasiasa wachambuzi wa mambo hayo mahususi yanayohusu demokrasia ya vyama vingi.

"Yaliyopita si ndwele tugange yajayo ni lazima tuvumiliane, kustahamiliana na kusahau yaliyopita" anakumbusha na kuongeza: "Maelewano ya kijamii hayawezi kudumu, iwapo kila siku watu wanakumbushana na kutishana kwa mambo yaliyopita, kiini cha maelewano na maridhiano ni ujasiri wa kuachana na ya zamani na kutoneshana vidonda maana vikitoneshwa haviwezi kupona."

Kadhalika anawaambia washiriki kuanza kuaminiana kwa sababu maelewano hayawezi kudumu kama wahusika watakua hawaaminiani na kila mara wanatafuta sababu za kulaumiana na kuibua kasoro.

Anawakumbusha umuhimu kukubaliana juu ya mgawanyo wa majukumu na namna bora ya kusuluhisha matatizo yanayojitokeza bila ya kuvunja maelewano na maridhiano yanayofikiwa.

"Mambo haya ni muhimu katika kufikia na kudumisha maelewano na maridhiano katika jamii, ni muhimu kuwa na uelewa wa pamoja jinsi ya kuendesha shughuli zetu za kisiasa, kijamii

> Wakati vyama vya kisiasa vinapofikia maridhiano suala la kuweka mbele uzalendo wa kupenda nchi pamoja na wananchi wake unatakiwa kuzingatiwa na kupewa kipaumbele muhimu.

na kiuchumi endapo tunataka kuwa na utulivu jambo ambalo ni sharti muhimu kwa maendeleo, "anasema Rais Mwinyi.

Akizungumzia kujiandaa na uchaguzi anakumbusha kuwa muhimu katika kuelekea katika uchaguzi mkuu, kukubaliana na lazima kulinda amani iliyopo na kwamba Tanzania imekua miongoni mwa nchi chache Barani Afrika iliyo na utulivu mkubwa wa kisiasa na yenye utamaduni wa kuvumiliana hivyo tofauti za itikadi za kisiasa zisidhoofishe udugu, amani, umoja na mshikamano huo.

Anasema ndiyo maana wanapotofautiana kisiasa wanakaa na kuzungumza na kuondoa tofauti ili kubaki wamoja, kudumisha amani na utulivu unaowezesha shughuli za kimaendeleo, kiuchumi na kijamii kushamiri na uchumi kukua.

"Watakapodumisha utulivu na ustahamilivu wataondoa shaka ya kutoaminiana baina yao na wakiimarisha dhamira ya maridhiano na maelewano ya kijamii wataona mema zaidi kuliko mabaya. Ni vizuri watu wakaishi kwa upendo na umoja na kukabili matukio yoyote ndani ya taifa letu tukijua sote ni wadau kamili wa hatma ya nchi yetu," anasema Rais Mwinyi.

"........wanasiasa tukumbuke kuwa watu wetu ni kama wengine duniani wanaweza kubadilika kwa mujibu wa mazingira yalivyo, hivyo tusiwafanye wakabadilika kwa mivutano isiyokuwa ya lazima na badala yake tuwawekee mazingira ya kimaendeleo na kujenga upendo kitaifa, "anasisitiza.

Rais Mwinyi awaasa viongozi wa siasa kuwa wanajukumu kubwa la kuifanya nchi kuendelea kudumu katika amani na kwamba serikali zote mbili zitaendelea kuyafanyia maazimio na mapendekezo yote watakayoyatolewa na wajumbe wa mkutano huo.

## KIWEPO CHOMBO

Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar ,Othman Masoud Othman, anashauri kuundwa chombo chenye wajibu wa kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya namna ya kuyafikia maridhiano ya dhati ya kisiasa Visiwani na kwamba kitasaidia kudumu kwa maridhiano ya kisiasa kabla, wakati wa na baada ya uchaguzi mkuu.

Othman anaungana na kauli ya Rais wa Zanzibar kuwa na dhamira ya dhati katika kufikia kwenye maridhiano ya kweli ambayo inapimwa na matendo ya kila mmoja, akisema: "Yote tuliyoyaazimia yanapaswa kuwekewa utaratibu wa namna bora ya kuyatekeleza. Kila Mzanzibari anastahili kufahamu kipi kitafanywa lini na nani. Ni kwa namna hii tutaondosha kulaumiana na kutiliana shaka kwani matendo ni fasaha zaidi kuliko maneno."

Othman ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo anasema ili kujenga Zanzibar moja ni lazima kila mmoja kuwa mkweli katika matendo yake akitaja mfano aliouacha Maalim Seif Sharif Hamad, (marehemu) wa kusimamia amani, umoja na mshikamano ni somo tosha kwa sababu alitekeleza hayo hata pale alipokua akipingwa na kutishiwa na wafuasi wake mwenyewe.

Anaongeza: "Maalim Seif aliamini kuwa hakuna mbadala wa amani na mshikamano, njia pekee ni nchi ifike mahala isimamishe utawala wa haki na uongozi bora.Dhamira ya kujenga umoja,amani na mshikamano isitikiswe wala kuyumbishwa na changamoto za ndani au nje ya mirengo ya kitikadi ili kuendelea kuvumiliana."

"Tunapenda sana wakati mwingine kulalamika mambo yetu ya Zanzibar kama kwamba ni ugonjwa tumeletewa na mtu. Tunayo mifano mizuri ya kuiga katika mageuzi ya kidemokrasia na utawala bora"anasema Othuman.

Anasisitiza kuacha kutoneshana vidonda kwa mambo yalitokea miaka ya nyuma hasa vuguvugu la kisiasa na badala yake vidonda hivyo vipatiwe dawa na kubaki kuwa makovu na kwamba kwa hakika wananchi wengi walioathirika kila wakati wa uchaguzi wamepoteza imani ya siasa na mfumo wa kuendesha chaguzi.

Anaongeza: "Hili si la kupuuza hata kidogo wao sio tu wamekuwa wakitoneshwa vidonda lakini

# anzibar anayoitamani hikamano, maridhiano



Washiriki wa Mkutano wa Wadau wa Kujadili Masuala Mahsusi ya Zanzibar, wakifuatilia mkutano huo.

wamekua wakipoteza viungo kila kukiwa na uchaguzi ni wakati wa kuwafanya kuwa na amani, tukawaaminishe kwa vitendo kuwa yaliyopita si ndwele sasa tugange yajayo".

**VIONGOZI WAHUSIKE**

Balozi Amina Salum Ali anasema kumalizika kwa mkutano huo ni historia kubwa ambayo itajenga Zanzibar hivyo wote wawe wamoja na kuzidi kuleta uelewano zaidi na kudumisha maridhiano ya kisiasa wanayoyatamani.

Anasema ili kuifikia dhamira ya kweli ya maridhiano yenye lengo la kumaliza siasa za chuki na uhasama ni jukumu la viongozi wa vyama vya siasa kujenga tabia ya uzalendo ambayo ni kupenda nchi na watu wake na kuitetea.

Kwa upande wa Zanzibar anasema zaidi ya mipango ya kufikia maridhiano ya kadhaa ya kisiasa Zanzibar hayajapata mafanikio mazuri kwa kukosa uzalendo na dhamira ya kweli ya kisiasa kubadilisha upepo mbaya.

Anasema wakati vyama vya kisiasa vinapofikia maridhiano suala la kuweka mbele uzalendo wa kupenda nchi pamoja na wananchi wake unatakiwa kuzingatiwa na kupewa kipaumbele muhimu.

**KUPENDA SUK**

Juma Duni Haji Mwenyekiti wa ACT Wazalendo anasema, siasa ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa Zanzibar ndiyo kiini cha jamii kugawika, kuvurugika, kudharau katiba na kusababisha wananchi kuuliwa bila makosa.

Na kwamba hali hiyo imeathiri sana mahusiano ya kijamii, ustawi na maendeleo ya uchumi mambo ambayo ni matunda ya utawala wa kidemokrasia ..."Majaribio ya kutafuta suluhu kwa njia ya muafaka wa kisiasa hatimaye yalizaa matunda Novemba 2009, kwa muafaka wa tatu kufikiwa, kati ya Rais Amani Abeid Karume na hayati Maalim Seif Sharif Hamad wakati huo akiwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi."

Duni anasema muafaka huo ndiyo ulizaa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) iliyodumu kati ya miaka 2010 -2015 chini ya Rais Dk. Ali Mohammed Shein. pamoja na chokochoko zilizokuwa zikitibua mahusiano baina ya washirika wa SUK, uchaguzi wa mwaka 2015 ulifanyika bila vurugu na kufika kiwango cha matokeo kutangazwa kabla ya kufutwa na hatimaye kuunda serikali kinyume cha ibara ya 91 (2) ya katiba ya Zanzibar.

Anasema uchaguzi wa 2020, ni kilele cha yale yaliyotokea tangu kurejewa kwa demokrasia ya vyama vingi mwaka 1992 na kwa busara na hekima za kiuongozi na kwa kulenga maslahi ya Zanzibar, Rais Mwinyi na hayati Maalim Seif Sharif Hamad baada ya mashauriano na vyama vyao, walikubaliana kushiriki tena katika kuunda SUK kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar.

Anasema makubaliano hayo yalilenga kuwa chachu ya kutafuta ufumbuzi wa kudumu na kubadili mwenendo wa hali ya siasa za Zanzibar ili kutoa fursa kwa taifa kujenga mstakabali mwema, kufikia maendeleo na kuhuisha ustawi wa Wazanzibari.

Anasema ni vyema kutambua kwamba wananchi wamechoka na maafa ya kiuchaguzi, hali yao duni ya maisha ndiyo ya kushughulikiwa na serikali ili kujenga ustawi wa raia.

**ZIKENI TOFAUTI**

Aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM, Vuai Ali Vuai ambaye kwa nyakati tofauti alipata kushiriki katika maridhiano ya muafaka wa kisiasa wa mwaka 2000 anasema misingi ya maridhiano inaundwa kwa kutekeleza siasa za kiungwana na kistaarabu zenye kuweka pembeni tofauti za kisiasa ziliopo.

"Nimefurahishwa na maridhiano yaliopo sasa kwa jinsi yanavyotekelezwa kwa vitendo ambapo matumaini yangu sasa tutafika tunapotaka kwenda ambapo ni kufunguwa ukurasa wa amani na utulivu wa kudumu"anasema Vuai.

Aidha, Katibu Mkuu wa CUF, Hamad Masoud anasema huu ni wakati muafaka wa kufunguwa ukurasa mpya wa kujenga siasa za kuvumiliana na kusahau yaliyopita kwa ajili ya kuvirithisha vizazi vya sasa na vijavyo na maelewano ya kudumu.

"Tunakabiliwa na mivutano ya kisiasa mara kwa mara kwa sababu hatujafanikiwa kusahau yaliyopita ambapo tumekuwa na tabia ya kutonesha vidonda mara kwa mara na ndiyo maana haviponi",anasema.

Msajili wa Vyama Vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, anaeleza kuwa amegundua kuwa Zanzibar, inapokuja jambo la kitaifa itikadi huwekwa pembeni na amefurahishwa na ushirikiano wa vyama vya siasa viliopo nchini ambavyo vimeshiriki kikamilifu kwa lengo la kutoa mchango unaolenga kuimarisha demokrasia.

## MWALIMU NYERERE 1922-1999

## Ndiye mzalendo aliyekataa lami nyumbani, kijijini kwake

**INATOKA UK. 13**

"Hivyo basi tumheshimu Mwalimu hata barabara hii aliyotamani iunganishe Mara na mkoa wa Arusha ingejengwa kwa viwango na kwa wakati, ili kumuenzi Mwalimu," anasema Wassira.

Anaeleza kuwa kwa sasa kiwango cha uzalendo kinaendelea kushuka kwa watu wengi na kwamba hali hiyo ni hatari, kwa kuwa raia wa aina hiyo kimsingi wanashindwa kumuenzi Baba wa Taifa kwa vitendo hasa wanapokuwa viongozi.

**MAONO ZAIDI**

Wasira anasema mbali na kuiunganisha Tanzania, anasema Baba wa Taifa alikuwa na maoni mengi na kwamba alipenda kuiona Afrika inaungana na kuwa moja. Lakini alipingana na Kwame Nkrumah wa Ghana katika suala hilo.

"Alitaka hatua ya kwanza iwe kuungana kwa nchi za Afrika Mashariki, Kusini, Kati na Magharibi na kuunda jumuiya za kikanda .

Wakati akiwa na fikra hizo , Rais wa zamani wa Ghana Kwame Nkrumah alitofautiana naye akipendekeza kuungana kwa nchi zote za Afrika kwa wakati mmoja na kushirikiana kwa kila hali.

Kwa kushirikiana wamekuwa viongozi wakuu wa Afrika kwani ndiyo waliounda Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) mwaka 1963.

Mwanasiasa huyo anafafanua kuwa katika harakati zake hizo, Baba wa Taifa alianzisha Ujamaa wa Afrika uliojaribu kujumuisha mfumo wa maisha wa Kiafrika wa kuishi kwa pamoja na siyo kila taifa lijiangalie lenyewe na kiubinafsi. Ni mfano wa mzalendo, asiyejali Butiama bali Tanzania kwa ujumla lakini pia akitazama pia maslahi ya Afrika nzima.

Wassira anakumbusha:"Alijadiliana na Jomo Kenyatta, na kuna wakati alikuwa tayari kumpa nafasi Kenyatta kuwa kiongozi wa Afrika Mashariki yote. Alikuwa tayari hata kuusogeza mbele uhuru wa Tanganyika, na kuzingojea nchi nyingine tatu za Afrika Mashariki kupata uhuru kwa matumaini ya kuungana pamoja baadaye kuwa na maendeleo makubwa wananchi wao waliyoyatamani."

Anaongeza kuwa juhudi zake hazikuungwa mkono na baadhi ya viongozi wenzake wa Afrika, akaelekeza nguvu katika kuyaunganisha makabila mbalimbali ya Tanzania kwa kutumia Kiswahili kama lugha ya taifa.

Maelezo ya Wasira yanazigusa Wakala wa Barabara wa Taifa (TANROADS) na Mijini na Vijijini (TANROADS) kuijenga na kuikamilisha barabara hiyo ambayo pamoja na kuunganisha Arusha, Mara na Manyara ni kazi aliyoianzisha na kuitamani Mwalimu Nyerere japo hakuweza kuijenga.

# Mitaala mipya, ufadhili 'Samia Scholarship' unavvyoakisi elimu



Mwalimu Nyerere akifurahi pamoja na wananchi kwenye harakati za kisiasa. **PICHA: MAKTABA**

**Na Sabato Kasika**

MAPITIO ya mitaala ili kuifumua na kuandaa mingine itakayobadilisha na kuboresha mbinu na mambo ya kujifunza ili kupata elimu bora zaidi yanayoendelea sasa, yanakumbusha juhudi za Mwalimu Julius Nyerere, Baba wa Taifa, kuwa kupata elimu bora kwa raia wake ndiko kutakakowawezesha kutumia rasilimali na mazingira yanayowazunguka kuboresha maisha na kujiletea maendeleo.

Umuhimu huo wa elimu ndiyo uliomfanya Rais wa awamu ya kwanza kutangaza vita dhidi ya maadui watatu ambao ni ujinga, maradhi na umaskini mara tu baada ya kupata uhuru mwaka 1961.

Katika vita hiyo, akawa anahimiza watu kupata elimu, kwa kuwa mtu akielimika anakuwa na uelewa na mbinu za kumwezesha kuondoa maadui wawili ambao ni maradhi au umaskini na kwamba zipo njia mbalimbali ambazo Mwalimu Nyerere alizitumia katika harakati zake za kuwaondoa Watanzania katika ujinga ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kila ambaye hakupata elimu katika mfumo rasmi, anaipata kivingine.

Tunapoadhimisha kumbukumbu ya miaka 23 ya kifo chake, Wizara ya Elimu inapitia upya mitaala na ni vyema kukumbuka njia iliyotumika watu kupata elimu kwa mfumo usio rasmi wakati huo miaka michache baada ya uhuru, ambao ni madarasa ya watu wazima.

Mitaala inapoboreshwa isisahau kutazama pia suala la watu wazima kuwa madarasani licha ya kuwa wasichana pamoja na wengine waliokatishwa masomo wamepewa nafasi ya kuendelea nayo hata kwa wale walioachishwa kwa ujauzito kujifungua na kurejea darasani.

> Taasisi ya Elimu ya Watu wa Wazima imekuwa ikiendelea kutekeleza jukumu la msingi la utoaji wa elimu ya watu wazima hadi katika ngazi ya wilaya, lengo likiwa ni hilo la kutokomeza adui ujinga.



Rais Samia Suluhu Hassan

Katika harakati hizo, mwaka 1964 Nyerere aliweka mkazo wa elimu kwa wote, kisha mwaka 1970 alitangaza elimu ya watu wazima kuwa suala la kuelimisha watu wazima ni jukumu la kila Mtanzania aliyekuwa anajua kusoma na kuandika.

Kutokana na dhamira yake ya kutokomeza adui ujinga, alianzisha kisomo cha watu wazima kilichoitwa ngumbaru, ambapo baadhi ya walimu wa shule za msingi waliopata mafunzo maalumu, walikuwa wakiwafundisha watu wazima muda wa jioni wakishatoka shuleni kufundisha wanafunzi wa mfumo rasmi.

Watu wazima walikuwa wakifundishwa chini ya miti kuanzia saa 10 hadi saa 12 jioni, lengo likiwa ni kuhakikisha kila Mtanzania anajua kusoma na kuandika badala ya kubaki mbumbumbu kama wakoloni walivyotaka. Hivyo ni jukumu la taifa leo kuona kuwa elimu inayotolewa asibaki mtu.

Hatua hiyo inaonyesha ni jinsi gani Baba wa Taifa alikuwa anajali umuhimu wa elimu kwa wananchi wake, hadi kuanzisha madarasa hayo ambayo yalizaa matunda kwa waliokuwa na nia ya kumwondoa adui ujinga japo leo kuna vijana wasiojua kusoma wala kuandika.

Licha ya kwamba kulikuwa na sintofahamu kutoka kwa baadhi ya walengwa, wakiwamo walioona aibu kwenda katika madarasa hayo, wakidai kuwa ni kujidhalilisha, kwamba wao si watoto hadi wafundishwe kusoma kuandika hayo yalikuwa ya zamani na kinachohitajika ni mwamko mpya.

Wengine hawakuwa tayari kuacha shughuli zao za kila siku na kwenda darasani, wakidai kuwa kusoma na kuandika na kuandika hakuwezi kuwasaidia lolote katika shughuli zao za kilimo.

Kila mmoja alikuwa na sababu zake, lakini katika mazingira hayo, wapo waliohudhuria madarasa hayo, ili kufuta adui ujinga kupitia mfumo huo wa elimu usio rasmi, ambao sasa unaendelea kwa utaratibu mwingine.

Jitihada hizo za Baba wa Taifa, zilisaidia kuifanya Tanzania kung'ara barani Afrika hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa kupunguza kwa kasi kubwa idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika mwaka 1970 na 1980.

### NGUMBARU HADI MEMKWA

Katika jitihada za kuendeleza kile ambacho Baba wa Taifa alikitaka cha kuhakikisha kila Mtanzania anajua kusoma na kuandika, kuna Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA), ulioasisiwa na Rais Benjamin Mkapa, katika juhudi za kuboresha elimu.

Lengo la mpango huo ni kutaka kupunguza ongezeko la watu wazima wasiojua kusoma na kuandika nchini ambapo viongozi wamekuwa wakifuatilia ili kuona kama elimu ya watu wazima inahuishwa ili kupunguza na hata ikiwezekana, kuondoa kabisa tatizo la kutokujua kusoma na kuandika nchini.

Taasisi ya Elimu ya Watu wa Wazima imekuwa ikiendelea kutekeleza jukumu la msingi la utoaji wa elimu ya watu wazima hadi katika ngazi ya wilaya, lengo likiwa ni hilo la kutokomeza adui ujinga.

Juhudi hizo za serikali za kupambana na adui huyo zinaifanya ishirikiane na wadau mbalimbali wa elimu wa ndani na nje ya nchi katika kutoa mafunzo ya elimu kwa watu wazima wanaohitaji kujiendeleza kitaaluma na kitaalam.

Lakini pia kuna Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi - MMEM pia upo mpango wa MMES uliozilenga Sekondari na MMEMWA ambao ni Mkakati wa Menejimenti na Maendeleo ya Walimu na MWAKEM yaani Mafunzo Kazini kwa Walimu wa Shule za Msingi.

Hatua hizo zote zinaonyesha jinsi gani kile ambacho Tanzania inaendelea kukiasisi katika kupambana na adui ujinga, kuboreshwa na kuongezewa nguvu kulingana na mazingira ya sasa ya sayansi na teknolojia.

### ADUI YUPO NCHINI

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika ilikuwa ni milioni 10, huku jitihada mbalimbali za kuondoa adui ujinga zikiendelea. Wakati kukiwa na idadi hiyo ya watu wazima wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu, taarifa ya utafiti ya kimataifa inasema bado kuna wengine milioni 750 duniani wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Hayo ni kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), ambapo linaweka wazi kuwa wengi watu hao wanaishi katika mabara ya Afrika na Asia, katika idadi hiyo, inaelezwa kuwa robo tatu ya watu wasiojua kusoma na kuandika ni wanawake, ingawa chanzo cha kuwafanya wawe wengi kuliko wanaume hakijatajwa.

Kwa Tanzania, serikali imeendelea kuweka mifumo na taratibu za kuwezesha kupata idadi kubwa ya Watanzania walioelimika na wanaopenda kujielimisha zaidi, ili wachangie katika maendeleo ya taifa, hivyo kumbukumbu ya maisha ya Nyerere inapoenziwa mitaala iwatazame pia watu wazima ili kutokomeza adui ujinga.

# Tambo za mwanawe Museveni zinavyoishtua Afrika Mashariki

- Ajitangazia uwezo wiki chache kuiteka Kenya
- Aondolewa jeshini, apanda kuwa jenerali

Na Ani Jozeni

KAINERUGABA Muhoozi Jenerali, mtoto wa Rais wa Uganda ambaye kwa njia tofauti anaanza kufanana na kiongozi wa Korea ya Kaskazini Kim Jong-un ni mtu mzoefu katika kushangaza kuanzia Uganda, nchi za Afrika na hata dunia katika 'posti' anazotuma mitandaoni.

Kupitia mtandao wa kijamii wa twitter wakati vita vya Russia na Ukraine vikipamba moto na taabu za kupanda bei za bidhaa kuanza, nafaka hasa ngano na kuvurugika soko la mafuta duniani, anaunga mkono kile Russia inachofanya.

Wapo walioshangaa kwa sababu inajulikana kuwa operesheni hiyo ya Russia, kuvamia jirani yake na kubadili mipaka na kumega majimbo ni tofauti na kanuni mahsusi za Umoja wa Mataifa na uhuru wa mataifa duniani.

Sasa jemadari huyo amefyatua mshtuko mwingine kupitia ukurasa wake wa twitter, wakati ambapo bado Uganda haijamaliza kazi ya kulifyeka kundi la Allied Democratic Forces (ADF) linalotokea Uganda na kufanya mauaji Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Uganda kwenyewe.

Anaandika katika mtandao huo , kwenye mustakabali wa mivutano ya kila wakati ya kibiashara kati ya Uganda na Kenya kuwa Jeshi la Uganda linaweza kuiteka Nairobi ndani ya muda mfupi usiozidi wiki mbili. Kuteka makao makuu ya nchi ndiyo kulitwaa taifa, kwa hiyo uwezo wake ni kuitwaa Kenya ndani ya muda huo.

Ulikuwa mzaha unaovuka mpaka, baba yake akachukua hatua, zinazochanganya watu na tayari Rais Yoweri Museveni, ameanza kumdhibiti kwa kumwondoa mwanae katika nafasi ya mkuu wa Jeshi la Ardhini (infantry), ambako alikuwa na cheo cha luteni jenerali, akampandisha kuwa jenerali na kumwondoa katika nafasi hiyo.

Hapo ndipo ulipo utata, kuhusu hatua zote mbili, kuwa nini katika suala hilo, yaani lengo na malengo yake. Mkanganyiko huo unaanzia katika sintofahamu kuhusu hisia za Rais Museveni kwa alichosema Kainerugaba, kwanza endapo alikifahamu awali, na kama alishtukizwa, hatua hizo mbili zinaashiria nini.

Unaweza kuona mgawanyiko kwa wazungumzaji kuhusu suala hilo katika makundi mawili, moja linaloona kuwa watu wawili au wanafamilia hao wana jambo lao na hivyo anayoyasema Kainerugaba ni yale yale ya baba yake japo asiyoweza kuongea kwa uwazi.

Wako wachunguzi wa mambo wanaodhani kuna uhalisia wa hisia hiyo, kwani katika miaka ya 1990 kufuatia kuondolewa madarakani kwa Rais Mobutu Seseseko huko Zaire (baadaye DRC) kwa ushirikiano wa Uganda na Rwanda, dhana ya 'himaya ya Wahima' ilisambaa eneo lote la Afrika Mashariki, Kati na Kusini. Walihitilafiana kwa kina baadaye.



Jenerali Kainerugaba Muhoozi. **PICHA: MTANDAO**

Kwa upande mwingine, unaweza kusema kuwa fikra ya kisiasa ya Rais Museveni, ambaye ni jenerali mstaafu wa Jeshi la Uganda, ngazi ambayo sasa mwanae ameifikia, inaendana na ile ya 'mpakwa mafuta wake Kanali Muammar Gaddafi, mtawala wa Libya kuanzia mwaka 1969 hadi alipoangamia vitani nchini humo 2011.

Alikuwa anatembelea Uganda na kuongea na machifu wakuu nchini humo ambao huitwa 'wafalme,' kuanzia Kabaka wa Buganda, na wengine wa Bunyoro na Toro kana kwamba ni makamu wa rais nchini humo.

Gaddafi kwanza alimsaidia Jenerali Idi Amin dhidi ya Tanzania, halafu inadaiwa kuwa akaisaidia National Resistance Movement (NRM) ya Museveni akishirikiana na Rwanda baadaye akaiteka Rwanda akaondoa utawala uliokuwepo wakati wa mauaji ya halaiki mwaka 1994. Kuteka nchi kujipanua kwao linaonekana kuwa ni jambo la kawaida.

Huwezi kusema kuwa Uganda ina mpango wa kuiteka Kenya kama Rwanda na Uganda zinavyodaiwa zinafanya Congo au Russia ilivyojitosa Ukraine, ila ni aina ya majigambo yenye sura ya kizalendo yanayoweza kusaidia kuhamasisha mihemko ya kisiasa nchini humo.

Ni kama kile cheo cha Mobutu mwaka 1977 akijiita 'Mobutu Seseseko Kuku Ng'bendu wa Zabanga,' ambako jarida la kila wiki la Newsweek nchini Marekani lilisema linamaanisha 'jogoo' asiyemwacha mtetea akabaki mwenyewe.

Ubalozi wa Zaire nchini Marekani ukang'aka kwa tafsiri hiyo, wahariri wakakazia uzi wakisema ni tafsiri sahihi.

Historia ilisahihisha majigambo hayo kwani akiwa tayari ni mgonjwa, utii kwa utawala wake ulikuwa umeanza kumeguka hivyo jeshi lake likashindwa kustahimili vishindo vya vikosi vya mizinga na vifaru vya Uganda na Rwanda.

Ushindi huo ulichochea hisia za msingi za Rais Museveni kama alivyokuwa 'mtiwa mafuta' wake, Gaddafi, za umuhimu kama si ulazima wa nchi za ukanda huo kuungana chini ya kiongozi mmoja mwenye nguvu.

Uwepo wa tawala mbili au tatu za Kihima ambao wana majina tofauti, ila kwa jumla ni wa kabila la Watutsi, unakuwa kianzio cha kupiga na kuunganisha nchi zote za ukanda huo. Ni 'ndoto japo inaibua 'bashasha,' raha.

Kwa vile mpango wa kuzipiga nchi za Afrika Mashariki ziungaishwe kuwa kitu kimoja kwa uongozi wa Wahima au Watutsi haupo, kuna mantiki ya kisiasa ambayo wachunguzi wa habari wanashuku inafuatiliwa na familia hiyo.

Ni kujaribu kumweka Kainerugaba katika macho na masikio ya watu kwa sababu yoyote ile, asisahaulike akawa raia wa kawaida hata ingawa anatoka familia ya rais. Ni mtaji muhimu kwa baba yake katika kuandaa mrithi, kuwa ajitahidi hadi Kainerugaba akiwa tayari ana misingi ya kutosha kukubalika kama kiongozi, si alazimishe halafu apinduliwe.

Ni rahisi zaidi kimantiki kuukubali mpangilio huo wa mawazo kuliko ule mwingine unaodhania kuwa Kainerugaba anajiongelesha kivyake na baba yake anachukua hatua dhidi yake, ila kwa tahadhari. Ndiyo mwelekeo wa baadhi ya wafuasi wa Rais Museveni, wakimwona Kaineruga kama kijana machachari na mwenye pupa kiasi fulani, hivyo labda hatafaa kuwa kiongozi wa nchi.

> Hivyo Jemadari Museveni ana kibarua kigumu kumwandaa Jemadari Muhoozi Kainerugaba kuwa mbadala wa 'Bobi Wine' kama kiongozi wa Uganda katika siku zijazo.

Rais Museveni haelekei kutaabishwa na hilo ila kuhakikisha kutosahaulika mwanae katika wimbi la siasa nchini humo, na hasa kwenye chama tawala.

Sababu mojawapo ni kuwa kinyang'anyiro cha urais nchini Uganda hasa ni cha kizazi cha vijana wa sasa (wasio na umri zaidi ya miaka 40 au 45) ambao kwa maana hiyo ni pamoja na Kainerugaba na mgomvi wa Museveni anayependwa na wengi, Robert Kyagulanyi Sentamu au 'Bobi Wine.'

Ni mbunge ambaye katika uchaguzi huru na wa haki anaweza kumshinda Museveni, na hana mshindani miongoni mwa vijana nchini Uganda. Hata wakongwe wa upinzani waliofuatana na Museveni, Kagame na wenzie kuondoa utawala uliofuata baada ya Amin, kama Kanali Dk. Kiiza Besigye, tayari wamemkubali kama kiongozi halisi mbadala upande wa upinzani.

Hivyo Jemadari Museveni ana kibarua kigumu kumwandaa Jemadari Muhoozi Kainerugaba kuwa mbadala wa 'Bobi Wine' kama kiongozi wa Uganda katika siku zijazo.

Kwa maana hiyo atajitambulisha kwa njia nyingi, na labda apewe dhamana za kisiasa baada ya kutumikia jeshi kwa miaka mingi jambo wafanyalo wafalme kabla ya kuchukua madaraka.

MKONO WA AFRIKA VITA 'UKRAINE'

# Wakati nchi za Afrika zikinuka umaskini rasilimali zake zinafanikisha vita Russia

• Mamluki 'Wagner' wadaiwa kuzipora, kuua raia



Baadhi ya maeneo ambayo watu waliuawa na kutupwa kwenye makaburi ya halaiki na sehemu ambazo mali kama mamia ya pikipiki zilichomwa moto  Machi mwaka huu katika mji wa Moura huko Mali. **PICHA: NEW YORK TIMES**

**Na Gaudensia Mngumi**

MAREKANI imeikoromea Russia na mamluki wake ikidai inatumia rasilimali za Afrika na kuinyonya Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), Mali na Sudan kufanikisha ufadhili wa vita vya Ukraine, mashtaka ambayo Russia imeyakanusha ikidai ni hasira dhidi yake.

Linda Thomas-Greenfield, Balozi wa Marekani katika Umoja wa Mataifa, anatoa madai hayo hivi karibuni akisema kundi la mamluki linaloitwa Wagner linatumika kusaka maliasili hizo na kuzitumia kufadhili vita vya Moscow katika mataifa ya Afrika, Mashariki ya Kati na Ukraine pia.

"Usifanye makosa: Waafrika wanalipa gharama kubwa kwa vitendo vya unyonyaji vya Kundi la Wagner la uporaji rasilimali na ukiukaji wa haki za binadamu," Linda, anauambia mkutano wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuhusu ufadhili wa makundi yenye silaha kupitia usafirishaji haramu wa maliasili barani Afrika.

Wagner, kundi linalofanya kazi na maveterani wa Jeshi la Russia, linadaiwa limepigana huko Libya, Syria, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Mali na nchi nyingine, likianzishwa mwaka 2014 baada ya Russia kutwaa rasi ya Crimea ya Ukraine na kuanza kuunga mkono watu wanaotaka kujitenga wanaounga mkono Russia katika eneo la Donbas mashariki mwa Ukraine.

Balozi wa Russia katika Umoja wa Mataifa, Vassily Nebenzia, akijibu anasema anasikitika kwamba Linda Thomas-Greenfield, anaibua suala la "msaada wa Urusi kwa washirika wa Afrika."

"Hii inafichua mipango na malengo yao halisi ya kile wanachohitaji hasa kutoka kwa mataifa ya Afrika," anasema Nebenzia, bila kufafanua.

> Ripoti pia zinadai kuwa wamejishughulisha na uhalifu katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Angola, Madagaska, Zimbabwe, na Sudan kwa mujibu wa The Africanews, ripoti ya Machi 2022.



Waziri wa Mambo ya Nje Russia, Sergey Lavrov. **PICHA: MTANDAO**

Uvamizi wa Russia uliofanyika Februari 24 mwaka huu dhidi ya Ukraine ulikuja wakati wa uhasama kati ya nchi za Magharibi, China na Russia kuhusu maliasili, biashara na uhusiano wa usalama wa Afrika. Maeneo mengine yana wasiwasi kuhusu kubanwa katikati ya ushindani mkali wa masuala ya siasa za kimahusiano.

Russia imekuwa ikijaribu kujiondoa katika kutengwa kwake kimataifa baada ya karibu robo tatu ya Baraza Kuu la Usalama la Umoja wa Mataifa kupiga kura ya kuikemea na kuitaka iondoe wanajeshi wake ndani ya wiki moja baada ya kuivamia Ukraine Februari mwaka huu.

## WAGNER NA AFRIKA

Wagner kundi la kigaidi lililodaiwa kuanza kazi rasmi kati ya 2014 na 2015 huko Crimea wakati wa utwaaji wa Russia wa peninsula hiyo ya Cremia ambapo wanamgambo wake wanadaiwa kufanyia kazi jeshi la Russia, ndiyo waliolinyang'anya Jeshi la Ukraine silaha na kuchukua udhibiti wake lakini bila kumwaga damu.

Taarifa mpya zinazotolewa na gazeti la The New York Times la Marekani zinalihusisha Kundi la Wagner lenye uhusiano na Jeshi la Russia kuwa linahusika na ghasia dhidi ya raia katika Jamhuri ya Afrika ya Kati CAR na Mali.

Wakati mamluki wa Russia kutoka kundi la kibinafsi la kijeshi la Wagner wamekuwa wakifanya kazi nchini Ukraine, wenzao wengine wanaripotiwa kuwa wapo barani Afrika licha ya kwamba hawajachunguzwa na wamewafanya raia kuwa shabaha yao kuu, kwa mujibu wa ripoti mpya iliyotolewa kuhusu shughuli zao katika nchi mbili za bara hilo linalotajwa kuwa dhaifu, linadai New York Times.

Katika Jamhuri ya Afrika ya Kati, Wagner inalenga raia katika zaidi ya nusu ya operesheni zao zote tangu 2018, kulingana na taarifa za Mradi wa Data za Mahali pa Migogoro na Matukio- ACLED (Armed Conflict Location & Event Data Project) au shirika la ufuatiliaji wa migogoro.

Ndani ya Jamhuri ya Afrika ya Kati, kwa mfano, mashambulizi 180 dhidi ya raia yakihusisha mamluki wa Wagner yameripotiwa tangu mwishoni mwa mwaka 2020, ikiwa ni asilimia 52 ya operesheni za kundi hilo nchini humo.

Kundi la Wagner, mtandao unaochanganya kikosi cha kijeshi na maslahi ya kibiashara na kimkakati kunuifaisha Russia, limedaiwa kufanya kazi nchini Mali, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Msumbiji na Libya, likishirikiana na viongozi na makamanda wa wanamgambo ambao wanaweza kulipia huduma zao.

Licha ya kwamba Russia inakanusha uhusiano wowote na Wagner, lakini maofisa wa Amerika na Ulaya wanasema ni zana isiyo rasmi ya nguvu ya Urusi, tena ikidaiwa kushirikiana na vikundi vya kigaidi na vyenye itikadi kali na kusababisha mauaji.

Nchini Mali na Jamhuri ya Afrika ya Kati vurugu zinazofanywa na mamluki wa Urusi sasa vinadaiwa kuwalenga raia na vikosi vya serikali, vikundi vya waasi au waasi wa Kiislamu, ACLED inasema.

Katika matifa ya Mali na Jamhuri ya Afrika ya Kati, vyombo vinavyofanywa na mamluki wa Russia sasa vinazidi kulenga raia na vikosi vya serikali, vya waasi au waasi wa Kiislamu, ACLED inadai.

ACLED inaongeza zaidi kuwa nchini Mali, ambako jeshi linapigana na waasi wenye mahusiano na Al Qaeda na Islamic State, mamluki wa Wagner wamehusishwa na vifo vya zaidi ya raia 500 mwaka huu na kusababisha majeruhi ambao katika miezi sita ya kwanza ya 2022 wanaelezwa kuwa ni wengi kupindukia vifo vya raia vingi pia.

"Machi mwaka huu Russia ilihusishwa na uporaji nyumba na kuwaua mamia ya wanaume katika kijiji cha Moura, kabla ya kuwalazimisha wenyeji kuchoma miili iliyotupwa kwenye makaburi ya halaiki, kwa mujibu wa uchunguzi wa New York Times.

Katika miaka ya hivi karibuni, Kundi la Wagner linadaiwa kushiriki kikamilifu katika migogoro katika nchi nyingi za Afrika na Mashariki ya Kati, ikiwa ni pamoja na Syria, Libya, Msumbiji na CAR.

Ripoti pia zinadai kuwa wamejishughulisha na uhalifu katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Angola, Madagaska, Zimbabwe, na Sudan kwa mujibu wa The Africanews, ripoti ya Machi 2022.

Aidha inadaiwa kuhusika na operesheni katika nchi 30 kote duniani (Kituo cha Mafunzo ya Kimkakati na Kimataifa, kilidai Septemba 2020.

JUKWAA LA VIONGOZI

## MOHAMED MORSI WA MISRI

# Msomi, mhadhiri vyuoni, mpiganaji shujaa aliyeanguka kufia kizimbani

• Hata leo kifo chake ni kitendawili

**Na Gaudensia Mngumi**

MOHAMED MORSI ni mwanasiasa wa Misri na rais wa tano wa taifa hilo aliyefanyakazi kuanzia Juni 2012 hadi Julai 2013, kisha kupinduliwa na Mkuu wa Majeshi Abdel-Fatah al-Sisi, Rais wa sasa kufuatia maandamano makubwa ya kupinga utawala wake.

Akiwa mahakamani alianguka na kufariki jambo lililoshangaza na kuibua mashirika ya kutetea haki za binadamu yakitaka kufanyika uchunguzi huru, kufahamu sababu halisi ya kifo chake kilichotokea katika mahakama ya kijeshi jijini Cairo, 2019.

Morsi, rais wa kwanza wa kiraia wa Misri, ambaye ni wa kwanza pia kuchaguliwa kwa njia ya kidemokrasia, alianguka kizimbani baada ya kujitetea na kuwahishwa hospitalini ambako ilitangazwa kuwa alikuwa amekata roho.

Alikuwa ametupwa gerezani tangu alipoangushwa katika mapinduzi ya kijeshi Julai 2013, na aliyekuwa waziri wake wa Ulinzi, Abdel Fattah al-Sisi, ambaye anadaiwa kuwa amefanya ukandamizaji dhidi ya wafuasi wa Morsi na wengine wakihukumiwa kifo.

Ni rais wa kwanza kuchaguliwa kidemokrasia katika historia ya taifa la Misri na msomi huyo wa shahada ya uzamivu (PhD) aliibuka kidedea akiwa mwanachama mwandamizi wa kundi la Udugu wa Kiislamu almaarufu 'Muslem Brotherhood', akichaguliwa kuwa mwenyekiti wa tawi la kisiasa la kundi - Chama cha Haki na Uhuru FJP, kilichoundwa na Udugu wa Kiislamu baada ya mapinduzi ya mwaka 2012, kufuatia Morsi na wengine kadhaa kutoroka gerezani.

Mursi aligombea urais na kushinda katika duru ya pili iliyompabanisha na Ahmed Shafik, Waziri Mkuu wa mwisho wa Rais Hosni Mubarak.

Kifo cha Morsi kilichotokea June 2019 kilihusishwa na mazingira mabovu na ya kutengwa aliyowekwa, kuteswa hali mbaya za wafungwa, taarifa ambazo serikali ya Misri inazipuuza zinazoihusisha na kusababisha msongo wa mawazo unaopelekea kuanguka kizimbani na kufariki dunia.

Mohammed Morsi amekaa jela kwa miaka mitano na mwaka 2015 alihukumiwa kifo, kwa hatia za ujasusi na kushirkiana na magaidi, yote hayo yakidaiwa kuongeza , presha, sonona, uchungu na majozi ambayo yamesababisha kifo cha mwanamapinduzi huyo.

### ALIKOTOKA MORSI

Akizaliwa mwaka wa 1951 katika jimbo la Al-Sharqiya kaskazini mwa Misri, amekuwa na kulelewa katika kijiji cha El-Adwa kwenye Delta ya Nile. Ni mtoto wa mkulima, na msomi wa Chuo Kikuu cha Cairo, mwenye shahada ya kwanza na ya uzamili katika uhandisi.



Profesa Mohamed Morsi. **PICHA: MTANDAO**

Kati ya 1975-76 hadi Morsi alihudumu katika jeshi la Misri, kwenye Idara ya Silaha za Vita vya Kemikali.

Mnamo 1979 Morsi alijiunga na kundi la Muslim Brotherhood, ambalo mara nyingi lilikandamizwa na serikali ya Misri, alipokuwa masomoni nchini Marekani. Elimu yake ilimpeleka Los Angeles, ambako alipata udaktari katika Chuo Kikuu cha Southern California mwaka wa 1982. Kutokana na ufadhili wa masomo alikaa katika taaluma hiyo akifanya kazi kama profesa msaidizi katika Chuo Kikuu cha California, Northridge, hadi 1985.

### KUREJA MISRI

Anaondoka Marekani na familia yake na kwenda kuongoza idara ya uhandisi katika Chuo Kikuu cha Zagazig cha Misri, karibu na mji wake, akiwa na watoto watano, wawili kati yao ni raia wa Marekani.

Morsi anapanda katika safu ya Udugu wa Kiislamu, na kuwa mjumbe wa chama mwenye nguvu ya uongozi mwaka 1995. Alichaguliwa kuwa mbunge mwaka 2000, akiingia bungeni kwa tiketi ya mgombea binafsi,baada ya chama cha Musilm Brotherhood kulipigwa marufuku rasmi, lakini alisimama na kuwa msemaji wa kundi hilo ndani ya bunge.

Mwaka 2006, Morsi alifungwa jela miezi saba kwa kushiriki maandamano ya kuwaunga mkono majaji waliokuwa wakidai uhuru wa mahakam, aidha, alikamatwa na kuzuiliwa kwa muda mfupi wakati wa maasi ya mwaka 2011 yaliyomuondoa madarakani Rais wa Misri Hosni Mubarak.

Baada ya Mubarak kuanguka, Muslim Brotherhood ilianzisha Chama cha Uhuru na Haki- 'Justice and Freedom Party' kama mrengo wake wa kisiasa na uchaguzi uliofuata wa bunge la katiba na bunge ulitawaliwa na Chama cha Uhuru na Haki kilichojipanga vyema.

> Aliimarisha mamlaka yake kwa kupunguza ya kijeshi kwani tangu 1952, kila kiongozi wa Misri hadi 2012 alikuwa 'mjeshi'.

Hapo awali chama kilimchagua Khairat el-Shater kugombea rais, lakini aliondolewa kijanja kutokana na figusu na Morsi alichaguliwa mbadala, na kusababisha baadhi ya watu kumtaja kama mgombea wa "tairi la akiba" (spare tyre candidate) wa Muslem Brotherhood.

### KUINGIA IKULU

Katika uchaguzi wa rais uliofanyika Mei 2012, alishinda karibu asilimia 25 ya kura zotekatika duru ya kwanza ya uchaguzi akizidi mgombea mwingine yeyote, akiwahakikishia wapiga kura wa Misri kwamba hatatawala kama mtawala wa kidini na kumbwaga Ahmed Shafiq - Waziri Mkuu wa mwisho Hosni Mubarak , katika duru ya pili ya mwezi uliofuata, kwa karibu asilimia 52 ya kura, zote na kuingia ikulu Juni 30, 2012.

Aliimarisha mamlaka yake kwa kupunguza ya kijeshi kwani tangu 1952, kila kiongozi wa Misri hadi 2012 alikuwa 'mjeshi', Agosti 2012, Morsi alimfukuza kazi Field Marshal Hussein Tantatawi, kiongozi wa Baraza Kuu la Wanajeshi, ambaye aliongoza Misri baada ya Mubarak kupinduliwa - ingawa alimteua kuwa mshauri wake.

Novemba 2012, Morsi alitoa amri yenye utata inayoweka maamuzi ya rais juu ya mahakama, kwa shinikizo, aliibatilisha mwezi uliofuata, lakini uchumi uliodhoofika, machafuko ya Sinai na maandamano ya mara kwa mara huku matatizo yakiendelea pamoja na ukosefu mkubwa wa ajira na sarafu kuporomoka viliwakasirisha Wamisri wengi, na wakosoaji wake - kutoka kwa watu wasio na dini na waliberali hadi wafuasi wa Mubarak wakisema aondoke ameshindwa kutimiza ahadi yake kwamba atatawala akiwa na msimamo wa wastani na kuboresha maisha.

### KIFO GEREZANI

Akiwa na miaka 67 alianguka mahakamani na kufariki hospitalini, Juni 19, ripoti za matibabu zilionyesha kuwa hakuwa na majeraha mwilini mwake.

Morsi alifariki alipokuwa akijibu mashtaka ya ujasusi na wakati huo alipewa kibali cha kuzungumza na hakimu na baada ya kesi kuahirishwa, rais huyo wa zamani alizimia na kufariki dunia na mwili wake ulipelekwa hospitalini.

Rais huyo alidaiwa kuwa na matatizo kiafya, ikiwa ni pamoja na kisukari na magonjwa ya ini na figo lakini pia kuteseka kutokana na kupuuzwa kwa matibabu yake wakati wa kifungo chake, ikichangiwa na hali mbaya ya jela, yote hayo yanadaiwa yalimuua..

**MITANDAO**




Kazi ya kuboresha baadhi ya barabara za mitaa ya Tandika, Manispaa ya Temeke Dar es Salaam ikiendelea jana, ili kuhakikisha zinapitika wakati wote. **PICHA: SABATO KASIKA**



Mhazini wa Benki ya Absa Tanzania, Idd Davis (wa pili kushoto), akisalimiana na mmoja wa wateja wa tawi la benki hiyo mjini Mbeya katika moja ya matukio ya kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja tawini hapo, hivi karibuni. Kushoto ni Meneja wa Absa Mbeya, Paul Mwambashi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mkurugenzi wa Uhusiano na Mawasiliano wa Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC Plc), Patricia Mhondo (kushoto), akikabidhi msaada wa vifaa vya usalama barabarani kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, ACP Mtatiro Kitinkwi, katika Kituo cha Polisi cha Oysterbay, Dar es Salaam juzi, ikiwa ni sehemu ya miradi ya kijamii ya kampuni hiyo. Kulia ni Ofisa Mnadhimu wa Polisi Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni, ACP Johari Said. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Meneja wa Wateja Maalum Tigo Pesa, Mary Ruta (kushoto), akikabidhi tiketi ya kwenda Qatar kushuhudia Kombe la Dunia kwa Solomon Wilfred baada ya kuibuka mshindi wa Promosheni ya Tigo ya Wakishua Twenzetu Qatar na Hisense, jijini Dar es Salaam jana, ambapo washindi watatu wamepatikana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mwanzilishi wa shirika linalojishughulisha na kupinga ukatili kwa watoto na wanawake la Lutogo Development Initiative Tanzania, Lulu Mwalubandu (mwenye nguo nyekundu) na Mkurugenzi wa Shirika la Himiza Development Organization, Prisca Ngweshemi na wanafunzi wakionyesha taulo za kike, baada ya kutoa msaada wa taulo hizo katika Shule ya Sekondari Kiparang'anda, wilayani Mkuranga, mkoani Pwani, kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike. **PICHA: SABATO KASIKA**



# Mbegu bora zaongeza uzalishaji maziwa Rungwe

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

UPATIKANAJI wa mbegu bora za madume ya ng'ombe kwa wafugaji wilayani hapo kumechochea ongezeko kwa uzalishaji wa maziwa kwa zaidi ya lita 200,000 kwa siku na kuingizwa sokoni.

Mwenyekiti wa Muungano wa Chama cha Wafugaji wilayani Rungwe (MUHAMARU), Asha Lukaja, alisema hayo walipokuwa wakipata elimu ya kutumia teknolojia za kisasa za ufugaji kwa kuwatumia maofisa ugani waliosambazwa wilayani humo na Kampuni ya Asas kwa kushirikiana na Serikali ya Denmark nchini Tanzania kwa lengo ya kuwawezesha wafugaji kuzalisha maziwa kwa tija na kuingiza katika mnyororo wa thamani.

Alisema kabla ya elimu hiyo walikuwa wakikabiliwa na tatizo la masoko na mbegu bora, kiwanda cha maziwa cha Asas kimewapatia madume ya mbegu bora za ng'ombe ambayo yamesaidia ongezeko la majike ambayo yamekuwa kichocheo kikubwa cha ongezeko la uzalishaji wa zao la maziwa.

"Licha ya ongezeko la uzalishaji wa maziwa na uwapo wa masoko ya uhakika, bado tatizo kwa baadhi ya wafugaji kuingiza sokoni maziwa yasiyokuwa na ubora jambo linalochangia kuchafua na kutia doa yanayozalishwa wilayani Rungwe," alisema Lukaja.

Fadhili Mbilinyi alisema kuwapo kwa kampuni ya ununuzi wa maziwa wilayani humo kumeleta tija kwa wafugaji kuongeza uzalishaji na kufuga kisasa. Alisema kwa sasa wanazalisha kiasi kikubwa cha maziwa na uhakika wa upatikanaji wa soko ndani na nje ya wilaya hiyo.

Ofisa Mifugo Wilaya ya Rungwe, Dk. Dennis Kamily, alisema wafugaji walio wengi hawapendi kuwatumia maofisa ugani ili kujifunza namna bora ya kuzalisha maziwa bila kutumia vyakula visivyo salama kwa ng'ombe.

Mkaguzi wa maziwa Wilaya ya Rungwe, Henry Mokiwa, alisema asilimia 20 ya maziwa yanayozalishwa na wafugaji wilayani humo yanakosa ubora kutokana na baadhi ya wafugaji kuongeza maji.

"Ukamuaji wa maziwa kiholela kwa baadhi ya wafugaji kunachangia kuzalisha bakteria 500 hadi 1,000 kila baada ya saa tatu na kusababisha madhara kwa watumiaji na kushauri wafugaji kuwatumia maofisa ugani ili kuboresha sekta ya maziwa nchini," alisema Mokiwa.

# RC aagiza watendaji waliotumia fedha za afua wachukuliwe hatua

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameagiza hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya watendaji wote wa halmashauri waliotumia fedha za afua za lishe kinyume na malengo yaliyokusudiwa.

Alisema tabia hiyo inakwamisha jitihada za kupambana na udumavu kwa watoto mkoani humo licha ya kufanikiwa kupunguza kiwango cha udumavu kutoka asilimia 33 hadi 22.9 kwa mwaka huu.

Homera alitoa agizo hilo jana wakati wa utiaji saini mkataba wa utekelezaji wa afua za lishe baina ya ofisi yake na halmashauri zote za Mkoa wa Mbeya.

Alisema mkataba huo ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kwa wakuu wa mikoa hivi karibuni waliotia saini mkataba wa afua za lishe na kutoa maelekezo kufanya hivyo kwenye maeneo yao ili kuongeza usimamizi katika mapambano dhidi ya utapiamlo na udumavu.

"Wakuu wa wilaya na wakurugenzi mmesaini mkataba huu wa afua za lishe ambao una vipengele 14 naomba mkateleze maana Rais kasema kila baada ya miezi mitatu tumpelekee ripoti, sisi Mbeya tunataka ripoti kupewa kila baada ya miezi miwili na nusu tuichakate kisha tumpelekee," alisema Homera.

Ofisa Lishe Mkoa wa Mbeya, Benson Sanga, alisema Sh. milioni 400 zimetengwa kuwajengea uwezo wananchi kukabiliana na tatizo la udumavu.

Alisema miongoni mwa mikakati ya kufanikisha utekelezaji wa afua za lishe ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi umuhimu wa lishe shuleni na vituo vya kutolea huduma za matibabu.

"Fedha tulizopokea ni sehemu ya utekelezaji wa afua za lishe yapo mambo mbalimbali ambayo tumepanga kutekeleza kama vile kuwaelimisha wajawazito kuzingatia mlo kamili na kuzingatia chanjo na huduma nyingine za matatibu ili kulinda afya ya mama na mtoto," alisema Sanga.

Akizungumzia utekelezaji huo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Ezekiel Magehema, alisema wanakwenda kuongeza fedha katika utekelezaji wa afua za lishe katika baraza lijalo.

Alisema kwa maelekezo ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, fedha zote zilizotolewa kwa ajili ya kufanikisha masuala ya lishe zitatumika ipasavyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Renatus Mchau, alisema wanakwenda kulifanya suala la lishe kuwa ajenda na kila mikutano na vikao mbalimbali suala hilo litazungumzwa.




Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kikatoliki (CUCoM), Taaluma, Prof. Euralia Temba (kushoto), akiendesha kongamano la siku ya kumbukumbu ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, jijini Mbeya jana, lenye mada kuhusu lugha ya kufundishia katika asasi za elimu Tanzania. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Ujenzi barabara Chimala-Kapunga sasa waiva

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

KATIKA kuhakikisha wananchi wananufaika na miradi mbalimbali ya maendeleo, serikali wilayani Mbeya, imepokea Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Chimala-Kapunga yenye urefu wa kilomita 26. Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema eneo la Kapunga ni miongoni mwa maeneo wilayani humo yenye wawekezaji wakubwa yakiwamo mashamba makubwa ya Kapunga Estate pamoja na wakulima wadogo na barabara hiyo ni muhimu.

"Kwa muda mrefu wananchi walikuwa wanaahidiwa kwamba barabara hii itaboreshwa, sasa tumeshapokea fedha hizi na tumeshatoa maelekezo kwa maofisa wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) ili waanze kuijenga," alisema Mfune. Aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa serikali ikiwamo kulinda vifaa vitakavyotumika kwenye ujenzi wa mradi huo ili visiibiwe pamoja na kukubali kupisha mradi huo kwa wale ambao watalazimika kuhamishwa.

Vilevile, alisema halmashauri hiyo imepokea Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu za wagonjwa kwenye Hospitali ya Wilaya inayojengwa katika eneo la Rujewa ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

Vilevile, alisema wanaendelea kushirikiana na wananchi kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa 127 ili kukabiliana na uhaba kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza wanaotarajia kuanza masomo mwezi Januari mwakani.





# Bil. 26.7/- kufidia waliopisha ujenzi wa mji wa serikali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema ulipaji wa fidia kwa wakazi 2,000 wa Kata ya Mtumba waliopisha ujenzi wa Mji wa Serikali utaanza ndani ya siku tatu huku Sh. bilioni 26.7 zikitarajiwa kutumika.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema tayari serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imechukua hatua kwa ajili ya kutoa fidia kwa watu hao ambao wanadai.

"Tayari serikali imechukua hatua kwa ajili ya utekelezaji wa zoezi hilo la utoaji fidia kwa walengwa wenye madai yao ya viwanja," alisema Mafuru.

Alisema ndani ya siku tatu ulipaji fidia utaanza kwa wale waliokidhi vigezo ili kuhakikisha wakazi wao wanapata stahiki yao kulingana na viwanja vyao.

Hivi karibuni, wakazi hao katika mkutano wao wa hadhara, walilalamikia serikali kuchelewesha kuwalipa fidia ya viwanja vyao walivyovitoa kupisha shughuli za kiserikali tangu mwaka 2020 baada ya kuahidiwa kulipwa mwaka 2021.

Mchungaji Kapange Kapange, alisema waliahidiwa kulipwa fedha hizo tangu mwaka jana, lakini mpaka sasa hawajatimiziwa hilo na kuiomba serikali kuwasaidia ili kuendeleza shughuli za kimaendeleo.

Kapange alisema wanaamini serikali yao itawasaidia wakazi wa kata hiyo ili kuhakikisha wanapata haki zao kutokana na kutoa viwanja kwa ajili ya kupisha shughuli za maendeleo kufanyika katika maeneo hayo.

Alisema wakipatiwa fidia hizo zitawasaidia kuwainua kiuchumi na familia zao kwa kuanzisha makazi mengine mapya.

Obed Mazuguni alisema wanaiomba serikali kuwasaidia ili walipwe fidia zao kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi.

Alisema fedha hizo zitasaidia kutatua changamoto zao za kuwasomesha watoto wao pamoja na kujenga makazi mapya.

Alisema maeneo yao yalikuwa yakitumika kama vitega uchumi vyao ambavyo vinawasaidia na familia zao.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, akionja maji walipofanya majaribio ya mradi wa maji Nzuguni, jijini Dodoma jana, unaotekelezwa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) na utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 4.8. Wengine ni Mbunge wa Dodoma, Anthony Mavunde (wa pili kushoto) na (kushoto) ni Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## FDH yazindua mradi kuboresha maisha wenye ulemavu

**Na Paul Mabeja,** MPWAPWA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Foundation for Disability Hope (FDH), limezindua mradi wa miezi minane utakaojihusisha na kuboresha maisha ya watu wenye ulemavu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma.

Mradi huo unalenga kuhamasisha upatikanaji wa elimu bora kwa watoto wenye ulemavu katika kata za Mpwapwa mjini na Mazae. Akizungumza wakati wa hafla fupi ya uzinduzi, msimamizi wa mradi Gabriel Muhuwa, alisema lengo jingine ni kuongeza uelewa wa jamii kuhusu haki ya kupata elimu kwa watoto wenye ulemavu.

"Pia kuongeza mwitikio wa serikali kuboresha mazingira ya ujifunzaji kwa watoto wenye ulemavu," alisema Muhuwa.

Alisema, mradi huo umeanza rasmi kutekelezwa mwezi Septemba 2022 na unatarajiwa kumalizika mwezi Aprili 2023.

Alisema, katika kipindi cha miezi minane ya utekelezaji wa mradi huo kazi zitakazofanyika ni pamoja na uzinduzi utakaohusisha kukutana na wadau mbalimbali wa masuala ya watu wenye ulemavu.

"Mikutano ya hadhara kwa ajili ya kujenga uelewa wa jamii kuhusu haki ya kupata elimu kwa watoto wenye ulemavu, mkutano wa kimkakati na wakuu wa shule na wajumbe wa kamati za shule, kujenga uwezo wa walimu."

"Kuendesha mkutano wa kimkakati wa ngazi ya wilaya kwa ajili ya utetezi na mipango ya utekelezaji juu ya taarifa zilizobainishwa na kufanya tathmini na ufuatiliaji," alisema.

Vilevile, wanatarajia baada ya mradi huo kutekelezwa jamii itabadilika na kuacha kuwaficha watoto wenye ulemavu ndani, kuwapeleka shule na serikali kuboresha miundombinu kwa ajili ya watoto hao.

Alisema, mradi huo unatokana na uchambuzi wa hali ya watu wenye ulemavu uliofanywa mwaka 2020 na Shirika la DID na kubaini kuwa watu wenye ulemavu nchini wana uwezekano mdogo wa kuhudhuria shule na kutojua kusoma na kuandika kuliko watu wasio na ulemavu.

"Hii inatokana na ukweli kwamba upatikanaji wa elimu kwa watu wenye ulemavu umekuwa ukikumbana na changamoto mbalimbali kama vile mazingira ya shule yasiyo rafiki pamoja na uelewa mdogo wa jamii kuhusu haki ya kupata elimu kwa watoto wenye ulemavu," alisisitiza.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mpwapwa, George Fuime, alisema mradi huo umekuja wakati mwafaka kwa kuwa wilaya hiyo bado inakabiliwa na matatizo mbalimbali ya utoaji elimu kwa watoto wenye ulemavu.

## DUWASA yabaini uwapo wa maji bonde Nzuguni

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), imebaini uwapo wa maji mengi katika bonde la Nzuguni na linategemewa litaongeza uzalishaji wa maji jijini humo.

Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, aliyasema hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa maji Nzuguni na kufanyika kwa majaribio ya uzalishaji kwa visima vitano vya maji vilivyochimbwa eneo hilo.

Alisema baada ya majaribio hayo limeonekana kuwa na maji mengi baada ya bonde la Mzakwe ambalo ndilo linategemewa kwa kuzalisha mengi kwa wakazi wa jiji hilo.

DUWASA iliamua kuchimba visima vitano pamoja na kujenga miundombinu ili kuyafikisha maji hayo haraka kwa wakazi wa Nzuguni, Ilazo, Swaswa na Kisasa na kuboresha hali ya upatikanaji wa maji jijini humo huku Sh. bilioni 4.8 zinatarajiwa kutumika kwa ajili hiyo.

Alifafanua kuwa mahitaji halisi ya maji kwa wakazi wa maeneo hayo ni lita 5,119,605 kwa siku, lakini baada ya mradi huo kuanza utazalisha lita 7,656,000 kwa siku.

Pia alisema mradi huo utaondoa mgawo wa maji uliokuwa ukiwasumbua wananchi wa maeneo hayo.

"Mradi huu utaongeza uzalishaji kutoka wastani wa lita milioni 67.8 kwa siku hadi lita milioni 75.5 sawa na ongezeko la asilimia 11.7 la uzalishaji wa sasa kwa Jiji la Dodoma," alisema.

Naye Mbunge wa Dodoma Mjini na Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alisema unahitajika utafiti zaidi ili kubaini maeneo mengine yenye majisafi kwa matumizi ya wananchi wa jiji hilo.

Mavunde alisema visima vilivyochimbwa maeneo ya Nala, Nzuguni na Ihumwa vitapunguza malalamiko ya wananchi kukosa maji kwenye maeneo hayo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, aliitaka DUWASA na wananchi wanaoishi maeneo yaliyochimbwa visima kuhakikisha maeneo hayo yanatunzwa.

Aliitaka DUWASA kuharakisha tathmini mapema ili kuwaondoa wananchi wanaoishi jirani na chanzo hicho kwa kushirikiana na uongozi wa jiji.



## Mariam Mwinyi ahimiza jamii umuhimu kuangalia afya ya akili

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi, ameitaka jamii kuendelea kwenda vituo vya afya wanapopatwa na tatizo la afya ya akili ili kupatiwa tiba.

Aliyasema hayo katika Viwanja vya Hospitali ya magonjwa ya akili, Kidongochekundu wakati akiwahutubia wananchi katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili Duniani iliyofanyika juzi.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Saada Mkuya Salum, alisema kuwa akili ni nyenzo muhimu kwa mwanadamu ambayo huitumia katika kufanya mambo yake hivyo ikitokea kuwa viashiria vya tatizo hilo ni vyema kuwahi hospitali mapema.

Alisema kuna baadhi ya watu wanawanyanyapaa na kuwabagua wagonjwa wa afya ya akili jambo alilosema ni kinyume na utaratibu.

"Unyanyapaa na ubaguzi unaoendelea kuwa tatizo kwa wagonjwa wa akili hivyo tuhakikishe kuwa tunawapatia matunzo wgonjwa wetu ili na wao wajisikie kuwa wanathaminiwa katika jamii yetu," alisema mama Mariam.

Aidha, alisema Zanzibar ina zaidi ya wagonjwa asilimia 6.8 kwa makisio ambao wanaishi na tatizo la afya ya akili kwa watu wazima, wanaume na wanawake jambo linaloshtusha na kwamba ipo haja kwa jamii kupatiwa elimu kuhusu tatizo hilo

"Wakati tunapopata takwimu sahihi ya matokeo ya sensa tutaweza kupata idadi kamili ya wagonjwa wa afya ya akili na kufanya mikakati ya kupata dawa na mambo mengine kwa uhakika," alisema.

Alisema tatizo la akili linasababisha kujiua hasa kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 25 na kupoteza nguvu kazi ya taifa.

Akitaja changamoto zinazowakabili, Mratibu wa Huduma za Afya ya Akili Zanzibar, Suleiman Abdi Ali, alisema wanakabiliwa na upungufu wa madaktari na wauguzi jambo linalohatarisha usalama wao kutokana na wagonjwa kuwapiga. Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Muhidini Abdi Mahamoud, aliahidi kuyafanyia kazi na kutatua changamoto zinazowakabili katika kitengo hicho.

# Waliopangishwa nyumba za serikali waonywa kuzigeuza madanguro

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHIRIKA la Nyumba Zanzibar limelaani kitendo cha baadhi ya watu waliopangishwa nyumba za serikali kuzitumia kinyume na mkataba wa makubaliano ya ukodishwaji.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, Mwanaisha Ali Said, alisema baadhi ya nyumba zinatumika kama madanguro na vijiwe vya matumizi ya dawa za kulevya.

Alisema nyumba za shirika hilo zinakodishwa kwa ajili ya makazi na sio ghala la kufanya biashara au ukahaba.

Alisema wamepokea malalamiko kuwa baadhi ya nyumba zinatumika kwa madanguro ikiwamo nyumba za Kikwajuni ambazo zilijengwa na Rais wa kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume pamoja na baadhi ya nyumba katika Mji Mkongwe.

Aliwataka wananchi waliokodishwa nyumba hizo, kusoma mikataba yao ya ukodishwaji kwa umakini na kufuata taratibu zilizowekwa ili kuepusha usumbufu utakaojitokeza pale shirika hilo litakapoamua kuchukua hatua.

Alisema ni lazima kila mpangaji kufuata vipengele vya mkataba na kuwa halali ili kuishi katika nyumba hizo kisheria.

Alisema, matumizi yasiyo sahihi ya nyumba hizo ni kinyume na sheria na linaendelea kukua na kuleta madhara kwa shirika na jamii.

Pia alibainisha kuwapo baadhi ya wapangishwaji wa nyumba hizo wanaweka reheni nyumba kwa kuchukua mikopo ya fedha katika taasisi za kibenki jambo ambalo ni kinyume na sheria.

"Wapo madalali wanaohusisha watendaji wa shirika nikiwamo mimi, wanauza nyumba ni kosa na atakayepatikana atanyang'anywa," alisema.

Alibainisha kuwapo baadhi ya watu wanaozikodisha nyumba hizo kwa ajili ya kulala wageni na kuzibadilisha matumizi.

Alisisitiza kuwa mambo hayo ni kosa kwa mujibu wa sheria na ni wajibu wao kufuata sheria zilizowekwa na shirika hilo halina nia ya kumdhalilisha, kumwonea, kumkashifu na kumnyang'anya nyumba mwananchi yeyote anayefuata sheria na taratibu zilizowekwa.

"Tunatoa onyo kali kwa wapangaji, watumiaji na wananchi wote wenye tabia hizo kuachana nazo mara moja ili kuepuka usumbufu na madhara yoyote yatakayojitokeza kutokana na hatua tutakazozichukua ikiwamo kuchukua nyumba zetu tumekupa nyumba kwa ajili ya kuishi na sio vinginevyo," alisisitiza.

Akizungumzia tukio la kutolewa mwananchi katika nyumba ya shirika inayorushwa katika mitandao ya kijamii katika eneo la Michenzani, alisema wamechukua hatua ya kumhamisha na nyumba hiyo iliuzwa na shirika lilivunja mkataba na mpangaji huyo.

Alisema shirika hilo limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 6 ya Mwaka 2014, kwa mujibu wa sheria hiyo limepewa mamlaka ya kusimamia sekta ya nyumba Zanzibar.

Alisisitiza shirika litaendelea kuchukua hatua kali dhidi ya mwananchi yeyote atakayegundulika kuvunja taratibu na masharti ya upangishwaji wa nyumba hizo na zoezi hilo litakuwa endelevu.



Wahudumu kitengo cha afya ya akili, wakifanya igizo maalum kuhusu changamoto zinazowakabili wakati wa utekelezaji wa kazi zao, kwenye maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili Duniani katika Hospitali ya Magonjwa ya Akili Kidongo Chekundu Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mtoto wa kike anavyokwamishwa ndoto ya elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKATI ikiadhimisha Siku ya Mtoto wa Kike, changamoto kubwa ni wasichana wengi kukabiliwa na vikwazo vya safari yao ya kuelekea utu uzima, huku mimba na ndoa za ututoni zikiwalazimisha kuacha shule na kukatisha ndoto zao.

Hayo yalielezwa jana na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Anna Athanas Paul, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya siku hiyo ambayo huadhimishwa kila mwaka, Oktoba 11.

Alisema wakati umewadia kwa sasa kuchukua hatua na kuwapa fursa watoto wa kike kutimiza ndoto zao na kuimarisha maisha yao.

Alisema takwimu zinaonesha jumla ya matukio 1,222 ya udhalilishaji yameripotiwa kwa mwaka 2021 kati ya hayo matukio 846 ni wasichana sawa na asilimia 79.2 na wavulana ni 222 sawa na asilimia 20.8.

Alisema mwaka huu wa 2022 kuanzia Januari hadi Agosti jumla ya matukio 695 ya udhalilishaji yameripotiwa kati ya hayo 481 ni wasichana.

"Kiwango cha matukio haya ni kikubwa ukilinganisha na idadi ya watu tulio nayo na hivyo miongoni mwa changamoto tunazokabiliana nazo ni kupoteza mwelekeo wa ndoto za watoto wetu," alisema.

Alisema kiwango cha utoro kwa wasichana shuleni bado kipo hasa kwa wanaosoma kidato cha kwanza hadi cha sita na jumla ya wasichana 610 kwa mwaka 2021 waliripotiwa kutoroka shule.

Alisema kiwango hicho sio kidogo kwa kuzingatia njia bora za uwekezaji kwa watoto.

Alisema kwa mwaka huu 2022 maadhimisho hayo yamejikita kuzungumza na wasichana na namna gani wadau na serikali wanaweza kutumia nafasi zao kuleta usawa wa kijinsia katika jamii pamoja na kumwezesha na kumwendeleza mtoto wa kike kufikia ndoto zake kwa kupata na kutumia vifaa vya kutunza na kuhifadhi heshima na utu wao ikiwamo taulo za kike.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni "Sauti Yangu, ni Usawa wa Baadaye". Ujumbe huo unatoa fursa kwa jamii na taasisi zinazoshughulikia masuala ya watoto kuzingatia sauti za watoto wa kike kwa kuwasikiliza na kutekeleza yanayowagusa ikiwamo maoni, ushauri, matumaini, mipango na vipaumbele vyao katika kufikia malengo yao.





# Diwani aangua kilio kwa kushinikiza mradi wa maji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

DIWANI wa Kata ya Sabasabini, Emmanuel Makashi, jana aliangua kilio kwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani na wananchi katika mkutano wa hadhara akiomba serikali kukamilisha ujenzi wa mradi wa maji wa Sabasabini - Mpunze ili wananchi wapate huduma hiyo.

Tukio hilo lilitokea katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji cha Bulima kata ya Mpunze Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, katika mkutano ulioitishwa na mbunge huyo kwa lengo la kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Alisema kipindi cha kiangazi wananchi wanapata shida ya maji na kunusurika kushambuliwa na fisi wakielekea kuchota maji kwenye mabwawa majira ya alfajiri.

"Kuna miradi ya maji kata jirani inajengwa kwa muda wa miezi sita na kukamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi, lakini mradi huu tangu ujenzi wake uanze mwaka 2017 mpaka sasa haujakamilika na kusababisha sisi kutumia maji na wanyama ambayo ni machafu,"alisema Makashi.

Aidha, alisema mradi huo ulianza mwaka 2017 lakini haujakamilika hali inayosababisha wananchi kununua ndoo moja ya maji kwa Sh.1,000 huku wakitembea umbali wa kilomita 10 kutafuta maji kwenye mabwawa yanayotumiwa pia na wanyama.

Amina Malunde ni mkazi wa Mpunze alisema kipindi cha kiangazi ndoa nyingi huvunjika kutokana na wenza wao kutowaamini wanapotumia muda mwingi kutafuta maji.

Akijibu malalamiko hayo, msimamizi wa mradi huo Mhandisi Bura John kutoka Kampuni ya Ndenengo alisema sababu ya mradi huo kutokamilika ni kuchelewa kwa malipo ya mkandarasi yaliyopaswa kufanywa na Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Alisema ujenzi wa mradi huo ulisimama baada ya aliyekuwa Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa kuagiza kupitiwa upya kwa mkataba wa ujenzi ambao thamani yake ni Sh.bilioni 1.2.

Alisema baada ya miaka miwili RUWASA iliwaagiza kuendelea na ujenzi lakini mpaka sasa haujakamilika kutokana na ukosefu wa fedha.

Akifafanua kuhusu mradi huo, Meneja wa RUWASA Wilaya ya Kahama, Mhandisi Maduhu Magili, alisema wako katika hatua za mwisho za maandalizi ya hati ya malipo na wakikamilisha mkandarasi atalipwa fedha ili kukamilisha mradi huo na wananchi kupata huduma ya maji.

Kwa upande wake, Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani aliwataka RUWASA kulipa fedha wanazodaiwa na mkandarasi huyo, ili mradi uweze kukamilika na kutoa huduma na kuwaondolea adha wananchi kutumia gharama kubwa kununua maji na kushambuliwa na fisi nyakati za alfajiri.



Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala (kulia), akipokea sehemu ya madawati 50 kwa Meneja wa Benki ya NBC Tawi la Mwanza, Thomas Lijaj (kushoto) jana, yaliyotolewa na benki hiyo, katika kusaidia jitihada za wilaya hiyo kukabiliana na changamoto ya uhaba wa madawati. Wanaoshuhudia ni maofisa waandamizi wa wilaya na wanafunzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Acharangwa mapanga, aporwa 10,000/-

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKAZI wa Kata ya Kizumbi, Manispaa ya Shinyanga, Baraka Mayala (24), amenusurika kifo kwa kucharangwa mapanga kichwani na sehemu mbalimbali za mwili wake na watu wasiojulikana akitoka kwenye harusi.

Akisimulia tukio hilo juzi, Mayala alisema Oktoba 7, mwaka huu, majira ya saa 4 usiku, kulikuwa na watu zaidi ya 10 wakimshambulia huku wakimtaka awape fedha na kwamba walimpekua wakachukua simu na Sh. 10,000.

"Watu hawa walinivamia njiani nikitoka kwenye harusi na kuanza kunikagua kwenye mifuko ya suruali, na wakati nikijitetea ndipo wakaanza kunishambulia kwa mapanga na kunipora kisha wakakimbia," alisema Mayala.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, Dk. Kambi Buteta, alithibitisha kumpokea kijana huyo hospitalini hapo na kubainisha kuwa wanaendelea kumpatia matibabu na afya yake inaendelea vizuri.

"Tulimpokea akiwa na majeraha kichwani na kwingine alijeruhiwa na kitu chenye kali, tulifanikiwa kumpatia huduma ya kwanza ili kuzuia damu zisiendelee kuvuja bado anaendelea na matibabu,"alisema Dk. Buteta.

Kwa upande wake Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Jackson Mwakagonda, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa polisi linaendelea na upelelezi ili kuwakamata wahusika.

**"Watu hawa walinivamia njiani nikitoka kwenye harusi na kuanza kunikagua kwenye mifuko ya suruali, na wakati nikijitetea ndipo wakaanza kunishambulia kwa mapanga na kunipora kisha wakakimbia," alisema Mayala.**

# Kanda ya Ziwa yapoteza asilimia 50 ya uoto wa asili

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SHUGHULI za kibinadamu katika mikoa ya Kanda ya Ziwa zimesababisha kupoteza uoto wa asili kwa asilimia 50, hali inayochangia kwa kiasi kikubwa mabadiliko ya tabia ya nchi ikiwamo kuwapo kwa ukame kwenye baadhi ya mikoa, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe wakati wa zoezi la upandaji miti katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Lugeye wilayani Magu mkoani Mwanza, Meneja wa Wakala wa Misitu Kanda ya Ziwa, Bakari Salim, alisema uoto wa asili kanda hiyo umepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli za binadamu.

Salim alieleza kuwa miongoni mwa shughuli hizo ni pamoja na ujenzi wa makazi na viwanda unaotekelezwa kila kukicha pamoja shughuli za uchimbaji wa madini katika maeneo mbalimbali, huku akiwataka wananchi kushirikiana na serikali kupanda miti katika maeneo yao ili kudhibiti ukame katika mikoa hiyo.

"Tunahitaji kupanda miti ya maua, matunda pamoja na ya kivuli katika mazingira yetu hii itasaidia kurudisha hewa ya ukaa pamoja na kukabiliana na tatizo hili la upotevu wa uoto wa asili unaoweza kusababisha jangwa katika mikoa yetu. Na sisi tupo tayari kutoa miti kwa watu binafsi, taasisi pamoja na mashirika ili kupambana na ukame," alisema.

Akifungua shughuli hizo za upandaji miti pamoja na ugawaji wa taulo za kike kwa wanafunzi wa shule hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima alisema ili kukabiliana na ukame mkoani humo watahakikisha wanapanda miche zaidi ya milioni tatu katika maeneo maalum.

"Maeneo mengi kwa sasa yamekuwa jangwa tunahitaji kuifanya Mwanza kuwa ya kijani kupitia upandaji miti na zoezi hili litatekelezwa kwa kipaumbele kikubwa katika maeneo na wazi pamoja na shule, tunaomba jamii kutoa ushirikiano katika utunzaji wa miti hiyo," alisema.

Katibu wa Shirikisho la Walimu Mkoa wa Mwanza, David Sulube, alisema waliamua kufanya shughuli za upandaji miti na kugawa taulo za kike, ili kuunga mkono serikali za utekelezaji wa elimu bure na utunzaji wa mazingira.

## HABARI KIMATAIFA

# Chad yapata Rais wa mpito

**N'DJAMENA,** Chad

MAHAMAT Idriss Déby ametawazwa rasmi kuwa Rais wa mpito nchini Chad, huku ikitajwa kuwa ni hatua mpya nchini humo baada ya mazungumzo ya kitaifa na jumuishi, ambayo yalikuwa yamesusiwa na sehemu kubwa ya upinzani na mashirika ya kiraia.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na RFI, wakati wa sherehe za uapisho Rais Mahamat aliambatana na majaji wawili wa mahakama ya juu nchini Chad, wakielekea katika ukumbi wa Ikulu ambapo walipokelewa kwa makofi kutoka kwa watu zaidi ya 1000 waliokuwa wakishuhudia suala hilo, akiwemo mmoja wa wageni Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari.

Pia ilielezwa kuwa Umoja wa Afrika (AU) haukuwakilishwa katika hafla hiyo, huku ikidaiwa kuwa Rais wa Tume ya Umoja wa Afrika, Moussa Faki, alikataa mwaliko aliotumiwa. **RFI**



Ofisa wa zimamoto akipita karibu na gari lililokuwa likiteketea kwa moto baada ya shambulio la Russia huko Kyiv, Ukraine, juzi. **PICHA: AP**

# Vita Russia na Ukrane bado mbichi

**KYIV,** Ukraine

MSURURU mwingine wa makombora ya Russia umeangushwa katika mji wa Zaporizhzhia kusini mwa Ukraine, huku huduma ya dharura nchini humo ikibainisha kuwa watu 19 wamefariki na wengine 105 kujeruhiwa katika shambulizi hilo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na VOA, makombora hayo yalipiga shule, kituo cha afya na nyumba zinazokaliwa na watu katika mji wa Zaporizhzhia, na kwamba mengine ya masafa marefu aina ya 12 S-300 yalipiga majengo ya serikali na kusababisha moto mkubwa katika sehemu hiyo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa makombora ya Russia yaliharibu mifumo muhimu mjini Kyiv na katika maeneo mengine 12 ya nchini Ukraine, jambo linalotajwa kusababisha zaidi ya miji 300 kukosa umeme, ikiwemo sehemu za mji wa Kyiv na Lviv, mpakani na Poland.

Aidha, ilieleza kuwa wanajeshi wa Ukraine wanaendelea kupambana na wanajeshi wa Russia na kwamba wamefanikiwa kuwarudisha nyuma.

Naibu waziri wa mambo ya nje wa Russia Sergei Ryabkov, alisema msaada wa nchi za magharibi kwa Ukraine, ikiwemo kutoa mafunzo kwa wanajeshi katika nchi wanachama wa NATO, na kutoa taarifa za ujasusi kuhusu sehemu ambazo Russia inalenga, ni dhihirisho kwamba mataifa ya magharibi yanahusika moja kwa moja na vita na kusaidia utawala wa Kyiv.

"Russia italazimika kuchukua hatua za kujibu zikiwemo zile zinazofanana, japo haina nia ya kujiingiza katika mgongano wa moja kwa moja na Marekani pamoja na NATO, tuna matumaini kwamba Washington na nchi zingine za magharibi zinajua hatari iliyopo ya vita kuendelea bila kudhibitiwa," alisema.

Ilielezwa kwamba kauli hiyo ya Ryabkov ilikuja baada ya Rais wa Belarus Alexander Lukashenko, kutangaza kuwa amekubaliana na Rais wa Russia Vladimir Putin kuunda jeshi la pamoja kukabiliana na kile alichodai kuwa uwezekano wa Ukraine kushambulia nchi yake.

Mkuu wa Jeshi la Ukraine alisema hajaona ushahidi wa wanajeshi kujikusanya nchini Belarus kwa ajili ya kutekeleza mashambulizi, huku akionya kwamba huenda Russia ikaendelea kushambulia majirani wake bila kuchokozwa, na kuharibu mifumo muhimu ya Ukraine kwa kutumia makombora ya masafa marefu.

"Adui hataacha kushambulia Kharkiv na Kherson, anajaribu kutishia watu wa Ukraine na kusababisha hofu," alisema.

Taasisi ya kuchunguza vita yenye makao yake mjini Washington, ilisema kwamba hakuna ishara kwamba jeshi la pamoja kati ya Belarus na Russia litatekeleza shambulizi dhidi ya Ukraine kutoka sehemu za kaskazini.

**KAULI YA PUTIN**

Naye Rais Putin, alisema shambulizi hilo lilikuwa jibu la shambulizi lililosababisha uharibifu kwenye daraja muhimu linalounganisha Crimea na Russia, huku akidai kwamba lilipangwa na wanajeshi maalum wa Ukraine.

Putin aliapa kwamba atajibu kwa nguvu zinazostahili iwapo Ukraine itaendelea kutishia usalama wa Russia, huku akilitaka baraza la usalama la nchi hiyo kutokuwa na shaka juu ya hilo, ambapo pia alitaja shambulizi dhidi ya daraja kuwa ni kitendo cha kigaidi.

Vile vile, Zelenskyy ametaka viongozi duniani kutangaza Russia kuwa nchi ya magaidi kutokana na hatua yake ya kushambulia raia na kutekeleza uhalifu wa kivita. **VOA**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya kifungu Na.19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni Na. 21(4) ya Kanuni za Mafuta (Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Reja Reja na Matumizi Binafsi), Gazeti la Serikali Toleo Na. 150 la 2022)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi la kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| **Jina la awali la kituo:** | Pray Anaseli Mushi - New Mlandizi Petrol Station |
| **Nambari Ya Leseni:** | PRL-2021-218 |
| **Mahali Kituo Kilipo:** | Kiwanja Na. 1, Eneo la Mlandizi, Wilaya ya Kibaha, Mkoani Pwani |
| **Jina Linalopendekezwa:** | Gudal (T) Company Limted |
| **Mmiliki Wa Awali:** | Pray Anaseli Mushi |
| **Mmiliki Mpya:** | Gudal (T) Company Limted |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;
Namba ya Bure 0800110030;
Barua pepe: **info@ewura.go.tz** Tovuti: **http://www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

217086202



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

**AGIZO LA KISHERIA KWA MAFUNDI UMEME WENYE LESENI**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inapenda kuutangazia umma hususani watu wanaofanya kazi za ufungaji wa mifumo ya umeme kuwa Kifungu cha 8(1)(2)(h) cha Sheria ya Umeme, Sura ya 131 na Kanuni ya 4(1) ya Kanuni za Umeme (Huduma za Ufungaji wa Mifumo ya Umeme) ya mwaka 2022 vinamtaka mtu yeyote anayefanya shughuli za ufungaji wa mifumo ya umeme Tanzania Bara kuwa na leseni ya umeme iliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

EWURA inawakumbusha Mafundi Umeme wote kufanya kazi kwa mujibu wa Kanuni za Umeme (Huduma za Ufungaji wa Mifumo ya Umeme) ya mwaka 2022 hususani Kanuni za 15, 16 na 17. Kwa kuhakikisha kuwa mifumo ya umeme inayofungwa inakidhi viwango vilivyoanishwa katika sheria, kanuni na taratibu mbalimbali katika tasnia ya umeme kabla ya kukabidhi kazi kwa mteja.

Kwa umuhimu, mafundi umeme wote wanapaswa kutoa "Cheti cha Ukamilifu wa Kazi" kwa mujibu wa kanuni ya 17(3) mara tu wanapokamilisha kazi za ufungaji wa mifumo ya umeme kwa mteja. Ukiukwaji wa takwa hili la kisheria ni kosa linaloadhibiwa na linaweza kupelekea kufutwa kwa leseni ya fundi umeme au kutozwa faini.

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

217086202

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya mwazo ya wilaya Bukoba**

**Kituo cha Bukoba Mjini Mkoa Kagera usimamizi wa mirathi Na. 54/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU Thomas Luangisa Rwaijumba wa Kitendaguro-Bukoba**

**Katika shauri la maombi ya kuteua msimamizi yaliyotolewa na**
1. **Rael Luangisa na**
2. **Yudes Luangisa.**

**TANGAZO**

**(Kanuni 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo )**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivya mnamo tarehe 28 mwezi 10 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

**Zingatia;**
Endapo kuna yoyote mwenye wasio wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
Imetolewa leo tarehe 22 mwezi 09 mwaka 2022

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE LAND ACT 1999 NO.4 OF 1999**
**RENEWAL OF RIGHT OF OCCUPANCY**
**Under Section 32**
**C.T. NO.................**
**LO NO..................**
**MBRL/9043**
**PLOT NO.1347 BLOCK X**
**MWAKIBETE AREA**
**MBEYA MUNICIPALITY**

**TO; DASTAN SIMON KAYANDA OF P.O.BOX 1441 MBEYA.**
**I,DICKLEY ENASS NYATO,** being Authorized Officer at Mbeya city Council of P.O.BOX 149, MBEYA,HEREBY CERTIFY that the right of occupancy registered under the above reference and which is due to expired on this date 30 day of june 2019 is not renewable on the same following terms and konditions.
1.Failure to develop the plot fo thirty six 36 years from commencement of your certificate of occupancy.
2. Failure to pay compensation to the native of occupier the right of occupancy shall expire on the ......day of ...2022
**Dated at Mbeya this......day of .....2022**

AUTHORIZED LAND OFFICER

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**SIRILI BAYYO SANKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye Index **Namba S1230-0183** kilichotolewa mwaka 2011 na Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) kupitia shule ya sekondari **MAGHANG**.
Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya polisi: **MAN/HAY/RB/742897/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HABIBU ALLY MHULA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T824DFD** aina ya **ALPHARD.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya polisi **DOM/RB/51183/2022**.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya MAKOLE**
**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 80/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU HADIJA SAIDI BENTA wa KONDOA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HAWA HAMZA MAFITA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 17 Mwezi 10 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo Tarehe 6 Mwezi 10 Mwaka 2022**

---

## TANGAZO LA MNADA

Work ethic company limited na Kiwirilauwo investment company Ltd Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Nyumba Na magari katika maeneo tofauti katika jiji la Dar es salaam Na Arusha ,Wateja wanashauriwa kulipa madeni yao ndani yasiku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe za Mnada Zinavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | Mahali dhamana ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Victoria Mduma Mwakalobo | TOYOTA RACTIS-T958DQJ | 26.10.2022 |
| JOHN NELSON MONGI | NYUMBA IPO LALASHE- ARUSHA | 17.10.2022 |

**Masharti ya Mnada.**
1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25%(au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%)litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa mawasiliano piga 0717956315(Work ethic) au 0752605575(Kiwirilauwo) au 0677014355 (Fanikiwa**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KAGERA LILILOPO BUKOBA**

**MAOMBI MADOGO NA. 50/2019**

**MELINES ATUGONZA CHRISTOPHER ..............MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**FADHIL MODEST MTAKA NA WENZAKE .....WAJIBU MAOMBI**

**KWA:- HAMDAN SULEIMAN MUSHEMA**
**JUMA SAMAYOMBO**

**MAJEMAJE AUTION MART & COURT BROKER**
**(POPOTE PALE MLIPO)**

Mnaarifiwa kuwa Maombi Na. 50/2019 yamepangwa kutajwa tarehe 16/11/2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, P.J. Makwandi saa 2:00 asubuhi.
Hivyo, mnaamuriwa kuhudhuria nyinyi wenyewe/mwakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 05/10/2022

MWENYEKITI
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**BUKOBA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MULEBA MKOA WA KAGERA**

**MAOMBI NA. 67/2022 (Yanayotokana na kesi Na. 2/2018 Baraza la kata Magata/Kalutanga)**

**SPENSIOZA SALAPION .........................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **STAIPHOD SALAPION**
2. **JENITHA SALAPION**
3. **TOROJESTA SALAPION** ..................**WAJIBU MAOMBI**
4. **EDMET SALAPION**
5. **JUSTA SALAPION**

**KWA : 1. STAIPHOD SALAPION**
**2. TOROJESTA SALAPION**
**3. JUSTA SALAPION – (POPOTE PALE WALIPO)**

Mnaarifiwa kuwa maombi Na. 67/2022 yamepangwa kutajwa tarehe 21/10/2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza J.K. Banturaki saa 2:30 asubuhi, mahali – Muleba (Mamlaka ya Mji Mdogo).
Hivyo, mnaamriwa kuhudhuria wenyewe/ wawakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 02/09/2022.

**MUHURI wa**

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MULEBA**

---

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LTD,** Kampuni ya **WHITE MIRACLES (T) LIMITED** tutauza kwa mnada wa hadhara Mali ya mdaiwa Sugu kama ilivyotangazwa gazetini

| Mdaiwa | Dhamana | Mahali dhamana ilipo | Tarehe ya Mnada |
|---|---|---|---|
| Peter Maniyo Phissoo | Kiwanja | Kitongoji cha Mifugoni (Msata ) - Bagamoyo | 26/10/2022 |

**Masharti ya mnada**
Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi.
Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
**Mawasiliano piga:-**
**White Miracles Auctioneers –**
**0754916444/0684937219**

---


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# TANGAZO

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY (TARURA)**

**ROADS TO INCLUSION AND SOCIOECONOMIC OPPORTUNITIES PROJECT (RISE)**

**IDA CREDIT NO. 6867 - TZ**

TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY
TARURA
P.O. BOX 11042, DODOMA.

## TENDER NO. AE.092/WB-RISE-P164920/260728/2022/23/W/01

## UPGRADING OF WENDA-MGAMA ROAD IN IRINGA DISTRICT AND MTILI-IFWAGI-MKUTA ROAD IN MUFINDI DISTRICT TO BITUMEN STANDARD (LOT 1 AND LOT 2)

## INVITATION FOR BIDS

1. This Invitation for Bids follows the General Procurement Notice for this Project that appeared in the United Nations Development Business (UNDB) No. WB-P890351- 12/21 of 14th December, 2021.

2. The Government of the United Republic of Tanzania has received a credit from the International Development Association (IDA) towards the costs of the Roads to Inclusion and Socioeconomic Opportunities Project (RISE) coordinated by the President's Office, Regional Administration and Local Government (PO-RALG) through a Project Coordination Unit (PCU) under the Tanzania Rural and Urban Roads Agency (TARURA). It is intended that part of the proceeds of this credit will be applied to eligible payments under the contract for **Upgrading of Roads to Bitumen Standard in Iringa and Mufindi Districts.**
   **LOT 1: Upgrading of Wenda-Mgama Road (19km) to Bitumen Standard in Iringa District**

   **LOT 2: Upgrading of Mtili-Ifwagi-Mkuta Road (14km) to Bitumen Standard in Iringa District**

3. The Chief Executive, Tanzania Rural and Urban Roads Agency (TARURA), an Agency of the Ministry under President's Office Regional Administration and Local Government (PO-RALG) on behalf of the Government of the United Republic of Tanzania now invites sealed bids from eligible bidders for

   **Lot 1: Upgrading of Wenda-Mgama Road (19km) to Bitumen Standard in Iringa District. The works must be completed within 18 months and**

   **Lot 2: Upgrading of Mtili-Ifwagi-Mkuta Road (14km) to Bitumen Standard in Iringa District. The works must be completed within 15 months.**

   **Table 1: Estimated Quantities for Major Items of Works**

| SN | GENERAL DESCRIPTION OF ITEMS | UNIT | Lot 1 QUANTITIES | Lot 2 QUANTITIES |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Clearing and grubbing including removal oftree and tree stumps. | Ha | 21 | 15.4 |
| 2 | Fill improved subgrade layer class G15 | Cu.m | 36629 | 26,250 |
| 3 | Fill material class G7 | Cu.m | 38,461 | 27,562 |
| 4 | Fill material class G3 | Cu.m | 77876 | 70,749 |
| 5 | Natural Gravel for subbase with minimumCBR 30 | Cu.m | 720 | 1,161 |
| 6 | Clashed aggregate class CRS | Cu.m | 32,661 | 18,666 |
| 7 | Stabilization layer material class CM (Lot 1)& C1 (Lot 2) | Cu.m | 46,146 | 32,569 |
| 8 | Prime coat (MC 30 cutback bitumen) | litres | 150,200 | 117,400 |
| 9 | Double Surface Dressing | Sq.m | 150,200 | 117,400 |
| 10 | 150mm Jointed Unreinforced ConcretePavement (JUCP) grade 37.5 | Cu.m | 720 | 1,161 |
| 11 | Concrete Pipe Culverts 900mm | M | 498 | 239 |
| 12(i) | Concrete Class 15 | Cu.m | 185 | 145 |
| (ii) | Concrete Class 20 | Cu.m | 1724 | 324 |
| (iii) | Concrete Class 25 | Cu.m | 1098 | 2646 |
| (iv) | Concrete Class 30 | Cu.m | 2415 | 1323 |
| 13 | Structural reinforcements for box culvertsand bridges | Tons | 384.16 | 310 |
| 14 | Streetlights | No. | 80 | 90 |

4. Bidders have the option to Bid for any one or more lots. Bids will be evaluated lot-wise, taking into account discounts offered, if any, for combined lots. The contract(s) will be awarded to the Bidder or Bidders offering the lowest evaluated cost to the Employer for combined lots, subject to the selected Bidder(s) meeting the required qualification criteria for lot or combination of lots as the case may be.

5. Bidding will be conducted through International Competitive Bidding (ICB) bidding procedures as specified in the World Bank's Procurement Regulation for IPF Borrowers 4th Edition of November 2020, and is open to all eligible bidders as defined in the Procurement Regulation.

6. Interested eligible Bidders may obtain further information from Office of the Procurement Management Unit (PMU), TARURA Headquarters, Attention: Project Coordinator, RISE Project, E-mail: pmurise@tarura.go.tz and inspect the bidding document during office hours from 07.30 to 15.30 hours' local time, Monday to Friday except public holidays.

7. Bidders should note that to qualify for award of the contract they are required to meet certain minimum qualifying criteria as provided in Section III (Evaluation and Qualification Criteria) of the Bidding Document, which includes but not limited to the following: -

| S/No. | CRITERIA | MINIMUM QUALIFICATION Lot 1 | MINIMUM QUALIFICATION Lot 2 | MINIMUM QUALIFICATION Both Lot 1 &Lot 2 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Average Annual Turnover calculated as total certified payments received for contracts in progress or completed, within the lastFive (5) years | US$ **13** Million | US$ **11** Million | US$ **24** million |
| 2 | Access to, or availability of, financial resources such as liquid assets, unencumbered real assets, lines of credit, and other financial means, other than any contractual advance payments to meet:<br>(i) cash-flow requirement<br>(ii) the overall cash flow requirements for this contract and its current commitments. | US$ **2.2**Million | US$ **1.8** Million | US$ **4.0** Million |
| 3 | A minimum number of similar contract that have been satisfactorily and substantially completed as a prime contractor, joint venture member, management contractor or sub-contractor between 1st January 2017 and application submission deadline each of minimum value | Less than or equal to 2 contracts, each of minimum value **USD 7.5 million** equivalent, but with total valueof all contracts equal or more than **USD 15million** equivalent. | Less than or equal 2 contracts, each of minimum value **USD5.0** equivalent, but with total value of all contracts equal or more than**USD 10 million** equivalent. | Must meet the aggregated requirement of two lots. i.e, Subject to compliance of the requirement for Lot1 and Lot 2 with respect to minimum value of single contractfor each lot, totalnumber of contracts is equal or less than 4 butthe total value of all such contracts is equal or more than **USD 25 million.** |

Further details and complete qualification requirements are provided in the Bidding Document.

8. A complete bidding document in English may be purchased by interested eligible Bidders upon the submission of a written application to the address below and upon payment of a nonrefundable fee of **Tanzanian Shillings Three Hundred Thousand Only (TZS 300,000.00)** or its equivalent in freely convertible currency. The method of payment will be by Banker's cheque, Bankers Draft or Cash to **Chief Executive TARURA, TARURA House, Government City – Mtumba, P.O. Box 11042 Dodoma, Tanzania or direct deposit or telegraphic transfer to the following bank Account:-**
   **Account Name : Tanzania Rural and Urban Road Agency**
   **Account Number 9925263161**
   **Bank Name : BoT**
   **Branch Name : Dodoma**
   **Swift Code : TANZTZTX**

9. Please note that the bidding documents are being provided in hard copies. However, only for the convenience of the bidders, in filling the various Forms and the Bills of Quantities, a soft copy in CD is also being given along with the hard copy. The bidders should note that in case of any difference in the hard and the soft copy, the one in hard copy only will prevail.

10. Bids must be delivered to **The Secretary, TARURA Headquarters Tender Board, Procurement Management Unit (PMU), TARURA House, Government City – Mtumba, Ground Floor, and P.O. Box 11042 Dodoma, Tanzania** on or before **10:00 am on Friday November 25, 2022,** Electronic Bidding will not be permitted. Late Bids will be rejected. Bids will be publicly opened in the presence of the Bidders' designated representatives and anyone who chooses to attend at the address below.
    **TARURA HQ Conference Hall, located at 2nd Floor**
    **P.O. Box 11042, Dodoma, TANZANIA Telephone: +255 026-2322929**
    **Fax: +255 026-2322929**
    **E-Mail Address: ceo@tarura.go.tz Web: www.tarura.go.tz**

11. All Bids must be accompanied by a **"Bid Security" of TZS 400,000,000.00 (Tanzanian Shillings Four Hundred Million Only)** for Lot 1 and **TZS 300,000,000.00 (Tanzanian Shillings Three Hundred Million Only)** for Lot 2 or an equivalent amount in freely convertible currency. The Bid Security shall be valid for **28 days beyond the bid validity period (i.e, 148 days after the bids submission deadline).** The Bid Security shall be Unconditional Bank Guarantee or Irrevocable Letter of Credit or Banker's Cheque clearly addressed to the Chief Executive, Tanzania Rural and Urban Roads Agency, TARURA House, Magufuli City, Mtumba, P.O. Box 11042, Dodoma, Tanzania.

12. Site visits and Pre-Bid meeting shall take place at **TARURA Iringa Regional Manager's Office, on 20th and 21st October 2022.**

13. Attention is drawn to the Procurement Regulations requiring the Borrower to disclose information on the successful bidder's beneficial ownership, as part of the Contract Award Notice, using the Beneficial Ownership Disclosure Form as included in the bidding document.

**Chief Executive,**
**Tanzania Rural and Urban Roads Agency,**
**P.O. Box 11042, Government City – Mtumba, Dodoma, TANZANIA**

217087502

# SERENGETI GIRLS KUPAMBANIA POINTI 3 KOMBE LA DUNIA LEO

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya umri wa miaka 17, Serengeti Girls kikishuka dimbani nchini India leo katika mchezo wa kwanza wa Fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Japan, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime, amesema itakuwa mechi ngumu lakini wapo tayari kupambania ushindi.

**Serengeti Girls wako nchini humo kushiriki fainali hizo za (FIFA U-17 2022), zilizoanza kutimua vumbi jana kwa kupigwa mechi nne ambapo Chile iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya New Zealand huku Brazil ikiichapa Morocco kwa bao 1-0.**

Mechi nyingine zilizotarajiwa kupigwa jana jioni ni kati ya Ujerumani na Nigeria na wenyeji India dhidi ya Marekani.

Tanzania (Serengeti Girls) ambayo itashuka dimbani majira ya saa 2:00 usiku katika michuano hiyo imepangwa Kundi D pamoja na Canada, Ufaransa na Japan.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu, Shime, alisema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri katika mechi yao ya kwanza leo dhidi ya Japan.

Alisema mechi haitakuwa rahisi kwa sababu wapinzani wao wamejiandaa kama ilivyo kwao kwa ajili ya kufikia malengo yao ya kusaka ubingwa katika mashindano hayo.

"Kila timu ni nzuri, hatuwahofii wapinzani wetu, tutaingia uwanjani kwa tahadhari kubwa kuhakikisha tunaanza vizuri mchezo wetu dhidi ya Japan," alisema Shime.

Alisema kila mchezaji anatambua umuhimu wa kufanya vizuri katika mashindano hayo, ukiacha kuiwakilisha nchi yetu pia wachezaji watakuwa wanajiuza wenyewe.

Nchi 16 zinazoshiriki mashindano hayo ni wenyeji India, China, Japan, Canada, Mexico, Marekani, Brazil, Chile, Colombia, New Zealand, Ufaransa, Ujerumani, Tanzania, Morocco, Nigeria na Hispania.

Tanzania ilifanikiwa kukata tiketi ya kushiriki fainali hizo baada ya kuitoa timu ya Cameroon kwa jumla ya mabao 5-1.

Serengeti Girls ilishinda mabao 4-1 ikiwa ugenini kabla ya kushinda bao 1-0 katika Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

**CHUMA...**



Kiungo 'chuma' wa Simba, Mdhamiru Yassin, akimiliki mpira dhidi ya wachezaji wa Primeiro de Agosto kwenye mechi ya mkondo wa kwanza ya Raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa nchini Angola mwishoni mwa wiki na Wekundu wa Msimbazi kushinda mabao 3-1. **PICHA: SIMBA**

# Mbuni FC haikamatiki Championship

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbuni FC imeendeleza ubabe wake kwenye Ligi ya Champioship baada ya kuwapigisha kwata Maafande wa Transit Camp kwa mabao 3-0 kwenye mechi iliyochezwa juzi Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Unakuwa ni ushindi wa nne mfululizo kwa timu hiyo yenye maskani yake jijini Arusha, ikionekana haitanii kwenye azma yake ya kutaka kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wakati huu ikiwa haijaruhusu bao lolote mpaka sasa.

Mabao ya washindi yalipatikana dakika ya 28 kupitia kwa Hassan Juma huku Athanas Mdamu akipachika bao la pili dakika ya 69 kabla ya Sadick Juma kufunga ukurasa kwa kutupia lingine dakika ya 74.

Kwa matokeo hayo, Mbuni FC bado inaendelea kuongoza ligi, ikiwa na ushindi wa asilimia 100, ikishinda mechi zote nne, mabao 13 ya kufunga, hivyo kujikusanyia pointi 12.

Mbuni FC inafuatiwa na Fountain Gate ambayo pia ina pointi 12 kwa kushinda mechi zote nne, lakini vijana hao wa Morogoro wana mabao sita ya kufunga na ikiwa imeruhusu bao moja, Kitayosce inashika nafasi ya tatu kwa pointi 10, Mashujaa ikiwa ya nne na pointi 10 pia, lakini imezidiwa idadi ya mabao ya kufunga.

Mechi nyingine iliyochezwa Jumatatu ilikuwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, timu ya Mbeya Kwanza ikishindwa kutumia vema dimba lake la nyumbani baada ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania.

Ni matokeo yaliyoifanya JKT Tanzania kukamata nafasi ya tano ikiwa na pointi tisa, huku Mbeya Kwanza ikiwa kwenye nafasi ya sita kwa pointi zake sita.

## Melis Medo amrithi Masoud Dodoma Jiji

**Na Adam Fungamwango**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa zamani wa Coastal Union, Melis Medo, ametangazwa rasmi kumrithi Masoud Djuma ambaye alitimuliwa juzi na Klabu ya Dodoma Jiji.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo imeeleza kuwa imechuakua hatua hiyo baada ya kusitisha mkataba na Masoud

"Uongozi unawaomba mashabiki wetu na wapenda michezo wote kumpa ushirikiano wa kutosha kocha Medo katika kipindi chote atakachohudumu kama kocha mkuu wa benchi la ufundi," ilieleza taarifa hiyo kwa vyombo vya habari.

Awali Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Johnson Fortunatus, alinukuliwa akisema wameamua kuachana kwa amani na Djuma baada ya kuona si tu kwamba timu haipati matokeo mazuri, lakini hata kiwango cha uchezaji hakiridhishi, hivyo wao kama viongozi wana jukumu la kuchukua hatua mara moja kabla hali haijawa mbaya zaidi.

"Tumefikia makubaliano ya kuachana kwa pande zote mbili kwa sababu kwanza hatupati matokeo, lakini hata kiwango chenyewe si cha kuridhisha, mechi sita tuna pointi tano tu na ligi inazidi kuyoyoma, tena ni ngumu sana, nia yetu si mbaya ni njema sana, nayo ni kujinusuru mapema, na sisi kama viongozi tuna wajibu wa kuhakikisha tunaweka sawa mambo kabla hayajafika kwenye hatua mbaya," alisema Fortunatus.

## Mwambusi ajipa mechi 5 Ihefu FC

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Mkuu wa Ihefu FC, Juma Mwambusi, amejipa mechi tano katika timu hiyo ili kukaa sawa baada ya kuanza kuona mabadiliko.

Mwambusi ameichukua Ihefu mikononi mwa Kocha Zuberi Katwila baada ya kutofanya vizuri wakati ikiburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na Nipashe, Mwambusi alisema kwa sasa kuna hatua anaiona ya mabadiliko katika kikosi chake baada ya sare mbili dhidi ya Tanzania Prisons na Mbeya City huku akijipa mechi tano kupata mwelekeo kamili.

"Kikosi changu kipo vizuri na nina majeruhi wanne, waliobaki wote wapo vizuri, kwa sasa tunakwenda kwenye mabadiliko na wachezaji naona wanaanza kunielewa kidogo kidogo.

"Naona wachezaji wanaanza kushika mbinu zangu kutokana na matokeo tuliyoyapata ya sare katika mechi mbili dhidi ya Prisons na Mbeya City, naamini baada ya mechi tano au sita nitapata mwelekeo wa timu na wachezaji wataanza kunielewa zaidi.

## ZISIKUPITE

### FIRMINO ATAKIWA ATLETICO

KLABU ya Atletico Madrid ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Liverpool na Brazil, Roberto Firmino mwenye umri wa miaka 31. ***(Todo Fichajes)***

### DE BEEK NA LEICESTER

LEICESTER City inamfuatilia kiungo wa kati wa Manchester United na Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 25. ***(Ekrem Konur)***

### MARTINELLI MKATABA MREFU

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Gabriel Martinelli mwenye umri wa miaka 21, amesema anataka kusaini mkataba mpya wa muda mrefu na Arsenal na yuko kwenye mazungumzo kuhusu kuongeza mshahara wake wa sasa wa pauni 50,000 kwa wiki. ***(Mirror)***

### LIVERPOOL YAMPOTEZEA MELO

LIVERPOOL hawana nia ya kuanzisha kipengele cha chaguo la kumnunua katika mkataba wa mkopo wa muda mrefu na Arthur Melo kutoka Juventus. Kiungo huyo wa kati wa Brazil mwenye umri wa miaka 26, anahitaji kufanyiwa upasuaji kutokana na jeraha alilopata akiwa mazoezini. ***(CBS Sports)***

### TONEY MKATABA MPYA

KLABU ya Brentford inatarajia kumpa mkataba mpya mshambuliaji, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 26, ili kuwazima Manchester United, Leeds, Newcastle na West Ham wanaomwania. ***(Mirror)***

### EVERTON KUMFUNGA IWOBI

EVERTON wameanza mazungumzo ya awali na kiungo wa kati wa Nigeria, Alex Iwobi mwenye umri wa miaka 26, kuhusu mkataba mpya. ***(Football Insider)***

### KANTE ATAKA KUBAKI

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 31, anataka kubaka Chelsea licha ya kuhusishwa na Paris St-Germain. ***(Le10 Sport)***

### JORGINHO HUYOOO BARCA

KIUNGO wa kati wa Chelsea na Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 30, huenda akajiunga na Barcelona pale Nou Camp kwa uhamisho wa bure msimu ujao. ***(Tuttomercato)***

### ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle bado inavutiwa na mchezaji wa Leicester na England, James Maddison mwenye umri wa miaka 25 na mshambuliaji wa Bayer Leverkusen na Ufaransa, Moussa Diaby mwenye miaka 23. ***(i News)***

### CARRICK NA MIDDLESBROUGH

KLABU ya Middlesbrough ipo kwenye mazungumzo na Michael Carrick kuhusu kuwa kocha wa klabu hiyo. ***(Football Insider)***

### EDWARD AWINDWA CHELSEA

CHELSEA imefanya mawasiliano mapya na Mkurugenzi wa zamani wa Michezo wa Liverpool, Michael Edwards ili kuchukua nafasi hiyo pale Stamford Bridge. ***(90 Minutes)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GRIEZMANN AKAMILISHA USAJILI WA KUDUMU ATLETICO MADRID

**MADRID,** Hispania

**Kwa nyongeza, mshambuliaji huyo wa Ufaransa ametia saini mkataba hadi Juni 2026...**

KLABU ya Atletico Madrid imethibitisha kuwa Antoine Griezmann amekamilisha uhamisho wa kurejea wa kudumu katika klabu hiyo akitokea Barcelona.

**Mfaransa huyo alijiunga na Atletico kwa mara ya kwanza mwaka 2014 akitokea Real Sociedad na kuwa mmoja wa wachezaji mashuhuri katika historia ya kisasa ya klabu hiyo, hasa akiwasaidia kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2016 na kushinda Ligi ya Europa mwaka 2018.**

Baada ya kuhusishwa sana na kuhamia Barca mwaka 2018, hatimaye alibadilisha mji mkuu wa Madrid na kutua kule Katalunya mwaka 2019, ingawa alionekana kuwa mchezaji mzuri, alirudishwa kwa mkopo Atletico mwanzoni mwa msimu uliopita kwa mkataba wa miaka miwili.

Na 'Los Rojiblancos' hao walithibitisha Jumatatu mchana kwamba, sasa wamekamilisha usajili wa kudumu wa Griezmann.

"Atletico de Madrid na FC Barcelona wamefikia makubaliano ya uhamisho wa Antoine Griezmann, ambaye tangu msimu wa majira ya joto wa 2021 na hadi sasa aliichezea klabu yetu kwa mkopo kutoka Barca," ilisema taarifa ya Atletico.

"Kwa nyongeza, mshambuliaji huyo wa Ufaransa ametia saini mkataba utakaomuweka katika klabu yetu hadi Juni 30, 2026."

Atletico walikosolewa na Barcelona mwanzoni mwa msimu huu walipojaribu kuzunguka kuwezesha kipengele cha kumnunua moja kwa moja kilichozidi euro milioni 40 kwa kumchezesha Griezmann kwa muda mfupi tu wa michezo.

Rais wa klabu ya Barcelona, Joan Laporta amethibitisha kuwa Atletico italipa euro milioni 20 pamoja na nyongeza ya euro milioni 4 kwa Griezmann.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,039,5
MECHI KALI
BARCELONA
VERSUS
INTER
1 | 1.45
X | 4.46
2 | 5.94
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CHELSEA WAPAMBANA KUMBAKIZA MOUNT



**LONDON,** England

CHELSEA bado ipo kwenye mazungumzo na kiungo, Mason Mount kuhusu mkataba mpya, kwa mujibu wa 90min, huku 'The Blues' hao wakiamini makubaliano yatafikiwa.

Mustakabali wa Mount ulionekana kuwa na wasiwasi mkubwa, lakini baada ya kuwasili kwa Todd Boehly katika klabu hiyo, mmiliki mwenza huyo wa Marekani alikuwa na nia ya kumpa mkataba mpya nyota huyo mwenye umri wa miaka 23 na mlinzi wa kulia, Reece James, 23.

James tayari amesaini mkataba mnono wa miaka sita na kwa hiyo lengo sasa liko kwa Mount, ambaye mazungumzo naye yanaendelea vizuri.

Vyanzo vimeithibitishia 90min kwamba, Chelsea hawana wasiwasi licha ya mazungumzo na kiungo huyo kuchukua muda mrefu kuliko yale ya James, na viongozi wa klabu bado wanalenga kukamilisha mkataba mpya wa Mount ifikapo mwisho wa mwaka msimu huu.

Baada ya ushindi wa 3-0 wikendi dhidi ya Wolves, ambao Mount alitengeneza mabao mawili ya kwanza, kocha Graham Potter aliweka wazi kuwa kiungo huyo ni muhimu katika mipango yake.

"Sina shaka na Mason Mount hata kidogo," alisema bosi huyo. "Ni kama kitu chochote, wakati mwingine timu haifanyi kazi vizuri na kwa hiyo watu binafsi hawafanyi kazi vile vile ... mchezaji mdogo anajua mpira wa miguu ni wa kupanda na kushuka, kuna wakati hauendi sawa.



# *Liverpool kumkosa Diaz hadi Desemba*

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL wamepata pigo jipya kwa habari mbaya kwamba, Luis Diaz atakuwa nje ya dimba hadi Desemba mwaka huu kutokana na jeraha la goti.

Mchezaji huyo raia wa Colombia aliondoka kwenye Uwanja wa Emirates kwa magongo baada ya 'Wekundu' hao kufungwa mabao 3-2 na Arsenal wiki iliyopita, huku kocha Jurgen Klopp akikisia kwamba jeraha hilo linaweza kuwa baya.

Kwa bahati nzuri, inaonekana kuwa jeraha hilo si baya zaidi na hatahitaji upasuaji.

Diaz atakosa mechi kumi zijazo za Liverpool kabla ya mapumziko ya Kombe la Dunia, akianza na mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Rangers wiki hii.

Watakuwa na matumaini, kwamba atakuwa fiti tena msimu wa Ligi Kuu England utakapor... jea Desemba 26, waka... Wekundu watakaposa... ri kucheza na Aston Vill...

"Tulilazimika kubad... lika kabla ya (muda w... mapumziko). Ni jerah... la goti, si zuri," alisem... Klopp baada ya kichap... kutoka kwa Arsenal.

"Atafanyiwa uchu... guzi halafu tutajua zaid... Sijui juu ya kiwango r... juu ya hilo hali ya Tren... (Alexander-Arnold) ... mbaya kwani ameum... kifundo cha mguu."

594,915/-

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.15/10/22 | 19:00 | Torino vs Juventus | 3.11 | 3.11 | 2.37 |
| 02.15/10/22 | 19:30 | Mallorca vs Sevilla FC | 2.77 | 2.97 | 2.72 |
| 03.15/10/22 | 21:00 | GO Ahead Eagles vs SC Heerenveen | 2.89 | 3.29 | 2.41 |
| 04.15/10/22 | 21:45 | Watford vs Norwich City | 2.64 | 3.24 | 2.64 |
| 05.15/10/22 | 22:00 | Athletic Bilbao vs Atletico Madrid | 2.45 | 3.23 | 2.88 |
| 06.15/10/22 | 22:00 | Cambuur vs Vitesse Arnhem | 2.60 | 3.39 | 2.60 |
| 07.16/10/22 | 13:15 | Sparta Rotterdam vs NEC Nijmegen | 2.33 | 3.44 | 2.89 |
| 08.16/10/22 | 14:30 | Standard Liege vs Royal Antwerp | 2.95 | 3.45 | 2.30 |
| 09.16/10/22 | 15:00 | Celta Vigo vs Real Sociedad | 2.54 | 3.19 | 2.79 |
| 10.16/10/22 | 16:00 | Spezia vs Cremonese | 2.48 | 3.18 | 2.88 |
| 11.16/10/22 | 16:00 | Southampton vs West Ham | 2.79 | 3.38 | 2.44 |
| 12.16/10/22 | 16:00 | Troyes vs AC Ajaccio | 2.25 | 3.13 | 3.28 |
| 13.16/10/22 | 16:00 | Rennes vs Lyon | 2.26 | 3.51 | 2.92 |
| 14.16/10/22 | 17:00 | Hull City vs Birmingham | 2.50 | 3.20 | 2.85 |
| 15.16/10/22 | 17:15 | Real Madrid vs Barcelona | 2.42 | 3.45 | 2.77 |
| 16.16/10/22 | 17:45 | AZ Alkmaar vs Feyenoord | 2.43 | 3.48 | 2.74 |
| 17.16/10/22 | 18:30 | Union Berlin vs Borussia Dortmund | 2.93 | 3.38 | 2.31 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO- 12/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2711 | Vissel Kobe vs Shonan Bellmare | 2.17 | 3.11 | 3.16 |
| 13:00 | 3116 | Yokohama F Marinos vs Jubilo Iwata | 1.22 | 5.83 | 8.94 |
| 13:00 | 5585 | Kawasaki Frontale vs Kyoto Sanga | 1.39 | 4.35 | 6.58 |
| 13:00 | 5754 | FC Tokyo vs Cerezo Osaka | 2.79 | 3.18 | 2.35 |
| 13:30 | 3929 | Suwon City vs Seongnam Ilhwa | 1.88 | 3.45 | 3.60 |
| 13:30 | 4082 | Suwon Samsung vs Daegu | 2.44 | 3.08 | 2.74 |
| 13:30 | 4982 | FC Seoul vs Sangju Sangmu | 1.97 | 3.41 | 3.36 |
| 13:30 | 5241 | Urawa Red Diamonds vs Consadole Sapporo | 1.82 | 3.64 | 3.64 |
| 14:00 | 2774 | Bangkok Glass vs BEC Tero Sasana | 1.31 | 4.78 | 7.99 |
| 15:00 | 2626 | Villarreal B vs Ponferradina | 2.36 | 3.31 | 2.82 |
| 15:00 | 4401 | Shahrdari Astara vs Esteghlal Khuzestan | 3.90 | 2.55 | 2.40 |
| 15:30 | 3705 | KS Lechia Zielona Gora vs Jagiellonia | 11.67 | 7.39 | 1.14 |
| 16:00 | 1118 | Mekelakeya vs Arba Minch Kenema | 2.63 | 2.78 | 2.78 |
| 16:00 | 1489 | Espoir FC vs Rutsiro FC | 2.68 | 2.83 | 2.68 |
| 16:00 | 3153 | Gorilla FC vs Musanze | 2.59 | 2.83 | 2.78 |
| 16:30 | 1595 | Cape Town All Stars vs Ajax Cape Town | 2.12 | 2.92 | 3.50 |
| 16:30 | 2679 | Uthongathi vs JDR Stars | 2.32 | 2.73 | 3.31 |
| 17:00 | 1203 | East Bengal vs FC Goa | 3.88 | 3.59 | 1.77 |
| 17:15 | 1490 | FC Andorra vs Burgos | 2.48 | 2.98 | 2.93 |
| 17:15 | 3993 | Leganes vs Malaga | 1.78 | 3.36 | 4.55 |
| 17:30 | 1308 | Zemplin Michalovce vs Sport Podbrezova | 2.77 | 3.26 | 2.31 |
| 17:50 | 5511 | AL Sahel SC vs Ohud Medina | 2.55 | 2.95 | 2.95 |
| 18:00 | 3568 | Zrinjski Mostar vs Velez Mostar | 1.34 | 4.39 | 8.01 |
| 18:05 | 1370 | Alshoulla vs AL Khlood | 2.44 | 2.74 | 3.08 |
| 18:10 | 2539 | Al Faisaly (KSA) vs AL Qaisoma | 1.51 | 3.74 | 5.82 |
| 18:15 | 2913 | Plaza Colonia CD vs Torque | 2.78 | 3.07 | 2.41 |
| 19:00 | 1277 | Al Jabalain vs Al Orubah | 1.76 | 3.20 | 4.56 |
| 19:00 | 1989 | AB Gladsaxe vs Aarhus | 9.35 | 5.84 | 1.22 |
| 19:00 | 2195 | Viking vs Kristiansund | 1.47 | 4.38 | 5.25 |
| 19:30 | 1921 | Real Oviedo vs Huesca | 2.40 | 2.97 | 3.07 |
| 19:30 | 4370 | Alaves vs Albacete Balompie | 2.06 | 3.22 | 3.52 |
| 19:30 | 4736 | Tenerife vs FC Cartagena | 2.34 | 3.22 | 2.92 |
| 19:30 | 5926 | APR FC vs Marines FC Gisenyi | 1.14 | 6.44 | 14.63 |
| 19:45 | 2096 | Napoli vs Ajax | 1.54 | 4.45 | 4.84 |
| 19:45 | 3472 | Atletico Madrid vs Brugge | 1.41 | 4.46 | 6.93 |
| 20:00 | 1983 | Aldosivi vs Banfield | 3.11 | 3.06 | 2.21 |
| 21:45 | 2520 | Tiverton Town vs Salisbury City | 2.17 | 3.79 | 2.67 |
| 21:45 | 3205 | Truro City vs Swindon Supermarine | 1.86 | 4.07 | 3.15 |
| 21:45 | 3935 | Bristol City vs Preston | 2.36 | 3.18 | 2.93 |
| 21:45 | 5914 | Kingstonian vs Brightlingsea Regent | 1.99 | 3.45 | 3.25 |
| 22:00 | 1154 | Sporting Lisbon vs Marseille | 2.30 | 3.42 | 2.83 |
| 22:00 | 1739 | Viktoria Plzen vs Bayern Munchen | 15.89 | 7.94 | 1.12 |
| 22:00 | 2582 | Racing Santander vs Zaragoza | 3.12 | 2.97 | 2.37 |
| 22:00 | 3847 | Bayer Leverkusen vs Porto | 2.11 | 3.57 | 3.07 |
| 22:00 | 4019 | Rangers vs Liverpool | 7.11 | 5.14 | 1.34 |
| 22:00 | 4217 | Barcelona vs Inter | 1.45 | 4.46 | 5.94 |
| 22:00 | 4511 | Lugo vs Las Palmas UD | 3.32 | 3.12 | 2.18 |
| 22:00 | 5291 | Tottenham vs Eintracht Frankfurt | 1.49 | 4.27 | 5.75 |
| 22:30 | 4528 | Sarmiento Junin vs Boca Juniors | 3.75 | 3.02 | 1.99 |
| 23:00 | 3497 | Tacuary Asuncion vs Club General Caballero Jlm | 2.21 | 3.11 | 3.06 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SERIKALI YAIZAWADIA MAMILIONI TEMBO WARRIORS KOMBE DUNIA

**Na Saada Akida**

SERIKALI imetimiza ahadi yake ya kuwakabidhi zawadi Timu ya Taifa ya Soka ya Watu wenye Ulemavu (Tembo Warriors), fedha taslimu kiasi cha Sh. milioni 40 baada ya kuiwezesha Tanzania kuingia katika nafasi ya saba ya viwango vya dunia kwa mchezo huo.

Hatua hiyo imekuja kutokana na serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, awali kutoa ahadi hiyo kwa Tembo Warriors kabla ya kwenda nchini Uturuki kwenye michuano ya Kombe la Dunia ambapo waliahidi endapo ikifika hatua ya robo fainali na kuitangaza vema nchi watatoa fedha kama hamasa.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Waziri wa Wizara hiyo, Mohamed Mchengerwa, aliwapongeza wachezaji wa Tembo Warriors kwa hatua waliyofikia kwa kulipambania taifa kuwa nafasi ya saba katika viwango vya dunia katika mchezo wa soka la watu wenye ulemavu.**

Alisema wamewafungulia milango timu zingine za taifa kutokana na kwenda kupambana katika mashindano ya Kombe la Dunia na hatimaye kutolewa katika hatua ya robo fainali.

"Nimefanikiwa kuwaona walivyocheza, wamepambana sana, nimeona mechi yao walijitoa na kucheza kwa ajili ya kutetea taifa, wanastahili pongezi na leo tunawakabidhi ahadi yao tuliyoahidi," alisema Mchengerwa.

Alisema serikali haitaitupa timu ya taifa endapo zitapambana na wachezaji kujitoa zaidi kwa ajili ya kulitangaza Taifa katika michezo husika.

Mchengerwa alisema kufanya vizuri kwa Tembo Warriors kumeifungulia timu ya Wanawake Serengeti Girls ambayo leo inashuka dimbani katika michuano ya Kombe la Dunia, dhidi ya Japan, katika fainali hizo zilizoanza kutimua vumbi jana nchini India.

## Mgunda aishusha presha Simba SC

INATOKA UKURASA 32

ya mechi hiyo ya kuachana na propaganda hizo," alisema Mgunda.

Kwa mujibu wa Meneja wa Idara Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, wanaendelea na maandalizi yao kwa ajili ya kumalizia dakika 90 za pili kwenye mchezo huo wa marudiano.

Alisema maandalizi yameanza rasmi jana katika Uwanja wa Mo Simba Arena lengo likiwa ni kuhakikisha wanapata ushindi ili kufuzu hatua ya makundi.

Alisema wameshinda ugenini, lakini hawajafuzu, hivyo wanaendelea na maandalizi kwa ajili ya kufikia malengo yao ya kucheza makundi na baada ya hapo kusonga mbele.

"Tumeshinda lakini hatujafuzu... lazima tufanye maandalizi mazuri katika mechi ya marudiano ili tufuzu, mashabiki wasiwe na wasiwasi kwa sasa timu iko chini ya mwalimu Juma Mgunda kwa siku zijazo za mbele... kikubwa tunaing'oa De Agosto na kusonga mbele," alisema Ahmed.

**ACHA WAJE...**



Wachezaji wa Simba, mshambuliaji Moses Phiri (mbele) na kiungo Pape Sakho wakiwa mazoezini na Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Suleiman Matola. Simba itaikaribisha Primeiro de Agosto ya Angola katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili wiki hii kwenye mechi ya mkondo wa pili ya Raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: SIMBA**

# *Serikali yaigeukia Yanga mechi CAF*

INATOKA UKURASA 32

matokeo yake yanakuja kuonekana wakati kama huu," alisema Ahmed.

Katika hatua nyingine Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ameanza kuwapa mpango mpya wachezaji wake lengo likiwa ni kuhakikisha anapata matokeo chanya katika mechi dhidi ya Al Hilal itakayopigwa nchini Sudan Jumapili wiki hii.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema maandalizi wanayofanya ni kufanyia kazi mapungufu yao katika kila safu ikiwamo ya ulinzi na ushambuliaji, kujilinda na kutafuta ushindi ugenini.

Alisema mechi itakuwa ya ushindani mkubwa na mikakati inapangwa kuelekea mchezo dhidi ya Al Hilal kwa sababu kila mmoja wao anahitaji kupata ushindi ili kufuzu hatua ya makundi ya michuano hiyo.

"Tumepata sare nyumbani mechi ya kwanza haina maana tumeondolewa, bado tuna nafasi ya kufanya vizuri katika dakika 90 za kipindi cha pili, tunaendelea na mipango yetu ya kuandaa kikosi kutafuta matokeo mazuri nchini Sudan," alisema.

Jumatano Oktoba 12, 2022
Nipashe

# Michezo



Liver kumkosa Diaz hadi Des. UKURASA 30

MAANDALIZI...



Wachezaji wa Yanga, mshambuliaji Fiston Mayele (kushoto) na kiungo Yannick Bangala wakiwa mazoezini. Yanga inajiandaa na mechi ya mkondo wa pili ya Raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal ya Sudan itakayopigwa nchini humo Jumapili wiki hii. **PICHA: MAKTABA**

## Mgunda aishusha presha Simba SC

**Na Saada Akida**

KAIMU Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amewashusha presha mashabiki wa klabu hiyo baada ya kuweka wazi kuwa bado yupo sana kuendelea kukinoa kikosi hicho kuelekea mchezo wao wa marudiano wa mkondo wa pili wa Raundi ya Kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Primeiro de Agosto nchini Angola.

Kauli hiyo ya Mgunda imekuja baada ya tetesi kwamba yupo kwenye rada za kutakiwa huduma yake na Klabu ya Daraja la Kwanza nchini Saudi Arabia, Abha FC ambayo hivi karibuni imemtimua Kocha wake Mkuu, Sven Vandenbroeck kutokana na matokeo mabavu kwa timu hiyo.

Simba itakuwa wenyeji wa De Agosto katika mchezo wa marudiano utakaopigwa Jumapili wiki hii saa 10 alasiri katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam baada ya ule wa awali nchini Angola kushinda kwa mabao 3-1.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda alisema hana taarifa hizo na hajapata ofa yoyote kutoka klabu ya nje wala ndani ya nchini na badala yake akili na nguvu zake anazielekeza kwenye maandalizi ya mechi ya marudiano dhidi ya De Agosto.

Alisema kwa sababu ya kufanya vizuri katika mechi ya kwanza ugenini kutakuwa na mambo mengi yakuleta mshtuko ili kuwaondoa mchezoni.

"Hizi taarifa sina, niko Simba sana kwa sasa haturuhusu hayo maneno zaidi ya kujikita kufanya maandalizi ya mechi yetu dhidi ya De Agosto ili kupata ushindi mnono zaidi ya tuliopata kwao.

"De Agosto si wabaya ila tuliweza kutumia mapungufu yao kwa kupata ushindi, lazima tuwe makini kwenye maandalizi yetu kwa ajili

INAENDELEA UK. 31

# Serikali yaigeukia Yanga mechi CAF

**Na Saada Akida**

● ● ● Yaitaka kwenda kupindua meza Sudan kama Simba ilivyofanya Angola, yatoa....

WAKATI Yanga ikiendelea na maandalizi mazito kuelekea mechi yao ya mkondo wa pili ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal ya Sudan, serikali kupitia kwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, ameitaka timu kwenda kufanya kile walichokifanya watani wao wa jadi, Simba kwa kupata ushindi ugenini kwenye michuano hiyo.

**Mwishoni mwa wiki Simba iliibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya wenyeji wao, Primeiro de Agosto nchini Angola huku Yanga ikilazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Al Hilal katika mechi ya michuano hiyo iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Kwa matokeo hayo, Simba sasa inahitaji sare ya aina yoyote, ushindi ama kutokubali kufungwa zaidi ya mabao 2-0 ili kutinga hatua ya makundi, wakati Yanga yenyewe ikilazimika kushinda au kutoka sare ya zaidi ya mabao mawili ili kusonga mbele.

Mchengerwa alitoa kauli hiyo Dar es Salaam jana, wakati akikabidhi zawadi kwa Timu ya Taifa ya Soka ya Watu wenye Ulemavu (Tembo Warriors), kutokana na kuiwezesha Tanzania kuingia katika nafasi ya saba ya viwango vya dunia kwa mchezo huo ilipokuwa ikishiriki Kombe la Dunia nchini Uturuki.

Mchengerwa alisema Simba wamefanikiwa kuipeperusha vema bendera ya Tanzania katika michuano ya kimataifa kwa kupata ushindi ugenini na Yanga iliyoanzia nyumbani sasa inatakiwa kwenda kupambana na kushinda mechi hiyo ya ugenini mwishoni mwa wiki hii.

Alimuagiza Rais wa Yanga, Hersi Said, timu yao kwenda kupambana nchini Sudan kwa ajili ya kupata matokeo na kwamba anaamini wachezaji wakijitoa watafanikiwa kupindua meza.

"Klabu zinapofanya vizuri katika mchezo hii, sifa inakuwa kwa taifa, tumeona Simba ilivyofanya nchini Angola na sasa tunataka Yanga waende kufanya kile kilichofanywa na 'Wekundu wa Msimbazi,'" alisema Mchengerwa.

Aidha, waziri huyo aliwataka viongozi wa Shirikisho la Soka nchini (TFF) na wengine kushirikiana na klabu zinazokwenda kushiriki michuano ya kimataifa kwa kuwasaidia mbinu ya kulitangaza taifa.

Alisema msaada huo ni pamoja na kuweka mikakati itakayosaidi kupiga hatua bila kubagua.

"Serikali ina mpango wa kuandaa michuano ya AFCON na ili kufanikisha hilo lazima klabu zetu zifanye vizuri waonekane na muwatie moyo," alisema Mchengerwa.

Hata hivyo, wakati Mchengerwa akiyasema hayo, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, amesema mafanikio yao yametokana na maandalizi makubwa waliyoyafanya mwanzoni mwa msimu.

"Tulijiandaa mapema kucheza mechi za kimataifa, tulikwenda nchini Misri kuweka kambi ya mwanzo wa msimu, tukacheza mechi mbalimbali ikiwamo dhidi ya Haras El Hodood, hatukwenda huko kwa ajili ya mechi za Ligi Kuu au Ngao ya Jamii, baadaye tukaenda Sudan kucheza dhidi ya Al Hilal na Asante Kotoko.

"Ili kucheza mechi za kimataifa inafaa ucheze mechi za kirafiki za kimataifa ili ujione wapi ulipo na upandishe kiwango au kukirekebisha, lakini ukijifungia na kucheza mechi unazotaka mwenyewe ili uzifunge, ufurahishe mashabiki wako,

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >